# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA PILI

**Kikao cha Saba – Tarehe 15 Februari, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 71

**Ziara ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**MHE. ANNE K. MALECELA** aliuliza:-

Kwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anachaguliwa na wananchi wote wa Tanzania waishio kwenye maeneo ya tambarare na milimani na kwa kuwa mara kwa mara ziara zake kwenye maeneo zinaishia kwenye maeneo tambarare tu. Je, Serikali haioni kwamba haiwatendei haki wananchi wake waishio milimani hasa wa Wilaya ya Same ambao ni takriban asilimia 60 ya wakazi wa Wilaya hiyo wanaoishi milimani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ziara za Mheshimiwa Rais Mikoani zimekuwa zikiratibiwa na viongozi Wakuu Mikoani. Ziara hizi zimekuwa zikiandaliwa kufuatana na malengo maalum. Mara nyingi ziara huandaliwa kwa lengo la kutembelea au kuzindua miradi ya maendeleo inayoendeshwa kwa nguvu za wananchi na mashirika au Taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais anapopata mialiko kwa ajili ya shughuli mbalimbali huhudhuria bila kujali eneo au mradi husika ulipo ikiwa ni milimani au tambarare kulingana na muda unavyoruhusu. Hivyo, si kweli kwamba mara zote ziara za Mheshimiwa Rais zinaishia sehemu tambarare tu, kwani miradi ya maendeleo na wananchi waliomchagua hawapo maeneo ya tambarare tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu akiwa madarakani alitembelea maeneo mbalimbali Wilayani Same kwa ajili ya kupata taarifa mbalimbali na kutembelea miradi ya maendeleo na kuhudhuria sherehe za kusimika viongozi wa dini. Kwa mfano, tarehe 22/2/2002, Rais alifanya ziara katika Wilaya ya Same na alitembelea Suji kuona miradi ya maendeleo milimani ambapo aliweka jiwe la msingi kwenye shule ya sekondari inayomilikiwa na Wasabato, alizindua zahanati na kukagua barabara iliyotengenezwa kwa nguvu za wananchi. Ziara za Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu ni kielelezo tosha kuwa Mheshimiwa Rais anapofanya ziara Mikoani, haishii maeneo tambarare tu kwani hata miradi iliyopo sehemu za milimani imekuwa ikitembelewa na Rais kulingana na ratiba ya ziara zake Mikoani.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba Rais alikuja Suji. Naomba kuuliza maswali yangu madogo mawili ya nyongeza.

Kwanza, Same ina Majimbo mawili, Same Mashariki na Magharibi, kwa kuwa tangu tumepata uhuru mwaka 1961 kusema kweli hajafika Rais yeyote Same Mashariki milimani na kwa kuwa wanaotayarisha ziara za Rais anapokwenda Mikoani ni Wakuu wa Mikoa na nimefanya utafiti mara kwa mara Wakuu wa Mikoa wanapotayarisha ziara zile wanampeleka Mheshimiwa Rais sehemu ambazo hazina matatizo ya kufikika na mara kwa mara ni sehemu za tambarare. Je, Serikali haioni kwamba wakati Rais anapofika Mikoani ni vema na sisi Wabunge tukahusishwa kwenye kutayarisha zile ziara ili katika kipindi cha miaka kumi Rais atakapokuwa madarakani aweze kuona wananchi wa nchi yake nzima?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi kwamba Rais hachagui bali inategemea na ratiba zinazopangwa na Mikoa husika. Mimi nawaomba Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa wapo karibu na Wakuu wa Mikoa wakati wa kupanga ziara za Rais wawe karibu na Wakuu wa Mikoa ili sehemu ambazo hazijatembelewa zitembelewe. Nina uhakika kwa kasi aliyoanza Mheshimiwa Rais atatembelea hata Vitongoji ambavyo havijafikika.

Na. 72

**Marekebisho na Ubinafsishaji wa *National Microfinance Bank (NMB)***

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa Bunge lilipitisha Sheria ya Kurekebisha na Kubinafsisha *NMB* kwa maana kwamba hisa nyingi zimo mikononi mwa Watanzania:-

(a) Je, mgawanyo wa hisa sasa ukoje?

(b) Je, ununuaji wa hisa umekwishaiingizia Serikali fedha kiasi gani hadi sasa?

(c) Je, ni benki ipi ina uwezo wa fedha kuliko benki nyingine hapa nchini na wenye hisa ni nani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Hezekia Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua ya kwanza Serikali imeuza asilimia arobaini na tisa ya hisa zake kwenye *NMB* kwa kundi la wawekezaji linaloongozwa na *Rabobank* Nederland. Mgawanyo wa hisa kwa sasa ni kama ifuatavyo:-

(a) (i) Serikali imebakia na asilimia 51.
*(ii)* *Rabobank* ya Uholanzi ina asilimia 34.9.
(iii) *NICO* ina asilimia 6.6.
*(iv)* *Exim* Bank asilimia 5.8.
(v) *TCCIA Investment Company Limited* ina asilimia 1.7. Kwa ujumla umilikaji wa hisa uliopo mikononi mwa Watanzania ikiwa ni pamoja na hisa za Serikali ni asilimia 65.1.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, hisa hizo ziliuzwa kwa kiasi cha Dola za Kimarekani 29.4 milioni ambazo ni sawa na shilingi 33.0 bilioni.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Desemba, 2005 benki inayoongoza kwa uwezo wa kifedha yaani mtaji mkubwa ni *NMB*. Mtaji wake ambao unajumuisha faida isiyogawiwa ni takriban shilingi 61 bilioni. Wenye hisa wa *NMB* ni kama nilivyokwishaeleza katika sehemu (a).

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa imedhihirika wazi kwamba *NMB* inafanya kazi vizuri sana na ina wateja wengi sana je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna haja ya kuongeza matawi hasa ukiangalia wateja ambao ni watumishi wengi wa Serikali na vyombo vyake katika Tawi la *Bank House* ambapo kuna watu wengi sana na wanatumia muda mrefu. Je, si wakati sasa wa kuongeza matawi ili watu wasitumie muda mrefu pale? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye na kwa kuanzia benki mwaka huu inaongeza matawi matano Dar es Salaam peke yake. *(Makofi)*

**MHE. PHILLEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Naibu Waziri amesema *NMB* ndio benki kubwa kuliko zote je, anaweza kutuambia kwamba ina madeni au ina faida tu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Naibu Spika, *NMB* haina madeni ina faida tu. (*Makofi*)

**MHE. RICHARD S. NYAULAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Waziri ameeleza kwamba Serikali ina hisa asilimia 51 na mwekezaji ana asilimia 49, je, kufuatana na uzoefu wa huko nyuma kwamba mara nyingi inapokuwa mwekezaji anakuwa na hisa ndogo uendeshaji wa makampuni huwa unakuwa na matatizo Waziri anaweza kututhibitishia kitafanyika kitu gani ili kuhakikisha kwamba benki yetu haitaingia katika matatizo kwa sababu wawekezaji wana hisa ndogo kuliko Serikali? (*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa *NMB* Serikali ndiyo yenye hisa kubwa asilimia 51 na hisa 49 sio za Serikali. Kwa hiyo kama tulivyosema ni kwamba hisa hizi zitaanza kuuzwa na zitauzwa kwanza hisa asilimia 21 kwa wananchi na baadaye hisa zitakazobakia zitauzwa kidogo kidogo. Lakini hatujapanga mpango wa kuziuza hizo lakini zile ambazo tunajua zitauzika ni zile asilimia ishirini na moja.

Na. 73

**Ushuru wa Forodha na Kodi ya Mapato**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED** aliuliza:-

Kwa kuwa Sheria ya Ushuru wa Forodha na Kodi ya Mapato inasimamiwa na *TRA*:-

Je, kuna tofauti gani ya utekelezaji wa sheria hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mbunge wa Wawi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utozaji wa Ushuru wa Forodha na Kodi ya Mapato unasimamiwa na Sheria mbili tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia Januari 2005, Ushuru wa Forodha unasimamiwa na Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki *(The East African Customs Management Act,* 2004). Sheria hii inatekeleza Itifaki ya Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*Protocol for the Establishment of the East African Customs Union*). Kabla ya hapo kila nchi ilikuwa na sheria yake ambapo nchini Tanzania ilitumika Sheria ya Ushuru wa Forodha yaani *Customs Excise Ordinance (Cap.403).*

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti zilizopo katika utekelezaji ni kwamba Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki husimamia kanuni na taratibu zote za forodha katika uingizaji wa bidhaa kutoka nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo viwango vyake vya ushuru vinafanana kwa nchi zote wanachama. Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 inasimamia utozaji wa Kodi ya Mapato hapa nchini.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Sheria ya Ushuru ya *East African* kama alivyoielezea Mheshimiwa Naibu Waziri kwa upande wa Tanzania inatekelezwa sawasawa katika sehemu zote za Tanzania je, ni kwa sababu gani viwango vya ushuru vinavyotozwa Bandari ya Dar es Salaam ni tofauti na Tanga, Zanzibar na mahali pengine?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuwa utaratibu huo ni mmoja, kuna sababu gani wanaoleta bidhaa kutoka Zanzibar wanachajiwa tena upya ushuru wanapofika Dar es Salaam?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala ambalo ameliuliza Mheshimiwa Hamad Rashid ni suala ambalo kwa kweli limekuwa linazungumzwa mara nyingi sana na hata kwenye Bunge hili Tukufu na kwa maana hiyo tumeamua kwamba suala hili liangaliwe na watendaji wa TRA. Wiki mbili zilizopita walikuwa Zanzibar kuliangalia suala hili. Kwa hiyo baada ya hapo ndio tutakuwa na majibu sahihi. (*Makofi*)

Na. 74

**Uboreshaji wa Miundombinu ya Barabara**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Kwa kuwa kati ya Kata 19 kwenye Wilaya ya Kilombero ni Kata mbili tu za Mlimba na Chisano zenye barabara ya lami na lami yenyewe ni ya vipande vipande na kwa kuwa hali hiyo inasababisha kupanda kwa nauli ya mabasi bila mpango hivyo wakulima kushindwa kusafirisha mazao yao:-

Je, Serikali ina mipango gani ya kuimarisha au kuboresha miundombinu ya barabara hasa kwenye maeneo ya Wilaya ya Kilombero?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilombero ina jumla ya kilomita 79 za barabara kuu na kilomita 206.04 za barabara za Mkoa ambazo zipo chini ya Wizara yangu na zinahudumiwa na Wakala wa Barabara, Mkoa wa Morogoro.

Kati ya kilomita 79 za Barabara Kuu, kilomita 10 zimejengwa kwa kiwango cha lami nyepesi (*otta seal*) na kilomita 69 zilizobaki zipo katika kiwango cha changarawe. Kwa upande wa barabara za Mkoa, jumla ya kilomita 24.17 zipo katika kiwango cha lami, kilomita 126 zipo katika kiwango cha changarawe na kilomita 55.72 zipo katika kiwango cha udongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005 na 2005/2006, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Uswisi kupitia Shirika lake la SDC imefanya matengenezo yafuatayo katika barabara za Wilaya ya Kilombero.

Ukarabati wa kiwango cha lami nyepesi sehemu korofi ya Kiberege hadi Sagamaganga kilomita kama kumi katika barabara ya Kidatu hadi Ifakara kwa gharama ya shilingi bilioni 1.568. Ukarabati huu utakamilika Februari, 2006.

Katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, jumla ya kilomita 20 katika maeneo mbalimbali ya barabara kati ya Kidatu na Kibaoni yalifanyiwa matengenezo kwa kiwango cha changarawe kwa gharama ya shilingi milioni 281.247 zilizotolewa na Serikali ya Uswisi. Katika mwaka wa fedha 2004/2005, maeneo mbalimbali ya barabara ya Kidatu na Sagamaganga yenye urefu wa kilomita 26 yalifanyiwa matengenezo ya muda maalum (*periodic maintenance*) kwa gharama ya shilingi milioni 256.320 kutoka Mfuko wa Barabara.

Aidha, Serikali inatarajia kujenga madaraja ya Kiberege na Sagamaganga. Ujenzi wa daraja la Kiberege, Mkandarasi ameshapatikana na ujenzi upo katika hatua za awali na utachukua mwaka mmoja kukamilika. Gharama za ujenzi wa daraja hili ni shilingi bilioni 1.014. Ujenzi wa daraja la Sagamaganga uko katika hatua za kumtafuta Mkandarasi. Fedha kwa ajili ya madaraja hayo zitatolewa na Serikali za Uswisi na Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2005/06, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara inaifanyia matengenezo ya kawaida *(routine/recurrent maintenance)* na matengenezo ya sehemu korofi (*spot improvement)* barabara ya Ifakara hadi Taweta. Jumla ya shilingi milioni 102 zitatumika ili kuimarisha sehemu kubwa ya

barabara hiyo ili iweze kupitika mwaka mzima. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kuchonga barabara, kufukua mifereji na makalvati na kuziba mashimo. Fedha kwa ajili ya kazi hizo zimetoka kwenye Mfuko wa Barabara. Aidha, shilingi milioni 80 kutoka Mfuko wa Maendeleo zitatumika kwa kazi za ukarabati kilomita nane za barabara hiyo. Utekelezaji wa kazi hizo unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Serikali kwa sasa haina mpango wa kujenga barabara hizo kwa kiwango cha lami kutokana na ufinyu wa bajeti, bado itaendelea kuhakikisha barabara zinapitika wakati wote kwa kuzifanyia matengenezo mbalimbali kadri bajeti ya Serikali itakavyoruhusu ili wananchi wa Wilaya ya Kilombero wapate mahitaji yao muhimu muda wote.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali la nyongeza. Je, atakubaliana na mimi kwamba katika barabara hiyo sehemu ya Mpanga – Taweta haijaguswa kabisa tangu mwaka 1994 katika kuikarabati wakati kuna madaraja mawili makubwa yaliyojengwa kwa shilingi milioni mia tano? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika maelezo yangu ya awali nimeeleza juhudi mbalimbali ambazo Serikali inachukua katika kutengeza sehemu korofi za barabara hizi na kuendelea kutengeneza barabara kadri fedha zinavyopatikana za ndani na za nje. Katika sehemu hiyo aliyotaja, Serikali inaahidi kwamba kwa mpango ambao nimeuelezea itaendelea kutekeleza ahadi yake ya kutengeneza sehemu hiyo na namwomba awasiliane na *Manager* wa *TANROADS* wa Mkoa wa Morogoro ili kuangalia uwezekano wa kutengeneza sehemu hiyo ambayo anasema haijawahi kuguswa hata siku moja.

Na. 75

**Tatizo la Usafiri Kanda ya Magharibi**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mikoa ya Kanda ya Magharibi yaani Kigoma, Rukwa na Tabora ina tatizo kubwa sana la usafiri na kwa kuwa barabara nyingi hazipitiki kwa miaka mingi sasa:-

Je, Serikali ina mpango gani kushughulikia tatizo hilo sugu?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanywa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua tatizo la usafiri katika Mikoa ya Kigoma, Rukwa na Tabora. Kutokana na sababu hiyo, Serikali imechukua hatua za makusudi zenye lengo la kuboresha barabara katika Mikoa hiyo kwa kuzifanyia matengenezo makubwa na madogo kama ifuatavyo:-

- Barabara ya Mpanda – Uvinza yenye urefu wa kilomita 187 imefanyiwa matengenezo makubwa kwa gharama ya shilingi milioni 889.7 kuanzia mwaka wa fedha wa 2003/2004 hadi 2005/2006.

- Barabara ya Uvinza – Ilunde – Malagarasi yenye urefu wa kilomita 55 imefanyiwa matengenezo makubwa kwa gharama ya shilingi milioni 1,263.70 tangu mwaka wa fedha 2001/2002 hadi 2004/2005 na mwaka wa fedha 2005/2006 imetengewa shilingi milioni 2,500 kwa madhumuni hayo.

- Barabara ya Urambo – Kaliua – Nguruka yenye urefu wa kilomita 120 inaendelea kukarabatiwa kwa kiwango cha changarawe hivi sasa kwa gharama ya shilingi milioni 2,752.13 ambazo ni mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)*.

- Barabara ya Mpanda – Iyonga – Koga yenye urefu wa kilomita 236 ilifanyiwa matengenezo kwenye sehemu korofi katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 kwa gharama ya shilingi milioni 127 zikiwa ni fedha za mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)*.

- Barabara ya Tabora – Kigwa – Itigi yenye urefu wa kilomita 164 imekuwa ikifanyiwa matengenezo kwenye sehemu korofi tangu mwaka wa fedha 2001/2002 hadi 2004/2005 kwa gharama ya shilingi milioni 669 na mwaka wa fedha 2005/2006 imetengewa shilingi milioni 344.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine maandalizi kwa ajili ya kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami, yako katika hatua mbalimbali za utekelezaji kwa barabara za Tunduma – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma hadi Nyakanazi, barabara ya Tabora – Malagarasi – Kigoma na barabara ya Nzega – Tabora.

Aidha, barabara ya Mwandiga – Manyovu yenye urefu wa kilomita 58 inaendelea kuimarishwa kupitia bajeti ya Serikali ya Maendeleo kwa kuijenga kwa kutumia lami nyepesi (*otta seal*) na changarawe. Katika mwaka huu wa fedha wa 2005/2006, jumla ya shilingi milioni 800 zimetengwa wakati katika mwaka wa fedha wa 2004/2005 shilingi milioni 400 zilitumika kwa ajili hiyo. Mwaka ujao wa fedha (2006/2007), Serikali itatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuendeleza mradi huu kwa kiwango cha lami kuunganisha nchi yetu na nchi ya Burundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za Kipili hadi Kitongoro, Chala hadi Kibondo, Ntendo hadi Muze, Sumbawanga hadi Chala na Chala hadi Mpanda

zitaboreshwa kupitia Mpango wa Matengenezo ya Kipindi Kirefu unaogharamiwa na fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Chini ya taratibu za mradi huu, barabara husika zitapata huduma ya matengenezo kwa viwango vinavyostahili kwa muda wa miaka mitano mfululizo chini ya Mikataba maalum na makandarasi  Taratibu za zabuni za kuwapata makandarasi kwa ajili ya kazi hizi zinaendelea baada ya kutangazwa mwishoni mwa mwaka jana mwezi Desemba, 2005. Pamoja na hatua mbalimbali nilizozieleza hapo juu, Serikali itaendelea kuzifanyia matengenezo ya kawaida barabara zote ili ziweze kuendelea kupitika. (*Makofi*)

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo yanaonyesha nia thabiti ya Serikali ya kufungua Mkoa wa Kigoma, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Barabara ya kutoka Kigoma mpaka Kasulu kilomita karibu 92 kwa sasa barabara ni mbaya sana na tunatembea kilomita hizo chache kwa masaa matatu. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha hiyo barabara sasa nayo inafanyiwa marekebisho mazuri ili iweze kupitika katika kipindi kifupi?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali kwa kweli ni kujenga barabara hiyo aliyoitaja Kigoma kwenda Kasulu kwa kiwango cha lami lakini wakati Serikali ikiendelea kutafuta fedha kwa sasa inafanya taratibu za mwanzo za kuijenga barabara hiyo, lakini pindi zitakapopata fedha za kutosha zitaijenga kwa lami. Lakini kabla ya kupatikana kwa fedha hizo Serikali itaendelea kuboresha barabara hii katika kiwango cha changarawe ili watu waweze kuendelea kutumia barabara hiyo bila usumbufu mkubwa na fedha kwa ajili ya kutengeneza barabara hiyo katika kiwango hicho tayari zipo kwenye bajeti.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa swali la msingi linaelezea tatizo la barabara za Magharibi na Mikoa hiyo iliyotajwa kutokuwepo na kwamba ni mbaya lakini Serikali imekuwa ikiahidi muda wote kwamba barabara inayotoka Tunduma kwenda Sumbawanga hadi Mpanda katika awamu ya kwanza hadi ya pili itatengenezwa. Je, barabara hii ya Tunduma fedha zake zipo na kama zipo inaanza lini maana yake kila siku ni ahadi na wananchi wanatuuliza kila siku barabara hii inaanza lini au bado ni maneno matupu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):**Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi ya Serikali si maneno matupu, ni azma ya Serikali kujenga barabara hiyo na kwa kweli barabara hiyo ya Tunduma kuja mpaka Mpanda aliyoitaja ni barabara ambayo kwa sasa ni kipaumbele cha Serikali na ndio maana hatua za awali za upembuzi yakinifu unaendelea kufanywa katika barabara hiyo. Ingekuwa kwamba maneno ya Serikali ni maneno matupu isingeweza hata kutoa hizo fedha za kuanza hizo hatua za awali za kufanyia upembuzi yakinifu lakini kama unavyojua baada ya kufanya upembuzi yakinifu ndipo Serikali itaweza kuwa sasa na kitu cha kuweza kupata fedha za ujenzi wa barabara hiyo. Kwa hiyo ahadi ya Serikali iko

pale pale na ni dhamira ya Serikali kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami ndani ya miaka mitano hii ijayo.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni nia ya Serikali kuinua uchumi wa Mikoa ya Rukwa, Kigoma na Tabora kwa njia zote za miundombinu, kwa njia ya barabara, ndege na pale inapowezekana ya gari moshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilikaa kwa muda karibu saa mbili na Wabunge wa Mkoa wa Kigoma nikiwaeleza kwa undani mpango huu. Nikawaeleza kwamba kazi hii imekwishaanza kama ambavyo tumekwishajibu hapa wiki hii na wiki iliyopita na kwamba itaendelea kwa Kasi mpya, Ari mpya kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Mimi binafsi nitaisimamia kwa sababu naelewa sana hili tatizo. Katika suala hili tunashirikisha sio tu Mikoa hii ya Magharibi lakini pia nchi ya Rwanda na Burundi na kazi zote zimekwishaanza. Ningependa Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa hiyo waamini kwamba Serikali ina nia thabiti na itafanya kila liwezekanalo kuhakikisha kwamba jambo hili linakuwa historia. (*Makofi*)

Na. 76

**Mitambo ya Simu za Mkononi**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:—

Kwa kuwa, kwa muda mrefu wananchi wa Kata ya Wino, Mahanje na Kata ya Muhukuru katika Jimbo la Peramiho wamekuwa wakipeleka maombi mbalimbali ya kupatiwa mitambo ya mitandao ya simu za mkononi kwenye Kampuni mbalimbali; na kwa kuwa, eneo la Madaba sasa ni eneo lenye shughuli nyingi za kibiashara na linatarajiwa kupata umeme na maji; na kwa kuwa, Serikali ina mpango wa kujenga Daraja la Umoja Na. 2 katika eneo la Muhukuru kuvukia Msumbiji. Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya mara nyingi ya kuwezesha suala la mawasiliano katika maeneo tajwa hapo juu?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mawasiliano ni muhimu katika shughuli za kijamii na kiuchumi sehemu yoyote. Simu za mikononi ni chachu ya maendeleo kwani zinawawezesha wananchi kuwasiliana popote walipo na ndiyo maana Makampuni ya Simu za Mikononi yana mipango inayolenga kupeleka huduma zao hadi vijijini.

Kwa hiyo, napenda kuchukua fursa hii kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Kampuni binafsi ya Simu ya *VODACOM* itajenga mitambo katika maeneo ya

Wino, Mahanje na Kata ya Mhukuru katika Jimbo la Peramiho. Kazi hii inatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka 2006. Wataalamu wa Kampuni hii *(VODACOM)* wamemaliza kuyapitia na kuyafanyia tathmini maeneo aliyoyaeleza Mheshimiwa Mbunge.

Kwa upande wa Kampuni ya Simu ya *MOBITEL*, yenyewe itapeleka mawasiliano katika sehemu za Kifanya, Madaba, Peramiho, Tunduru, Namtumbo na Mkongo. Kwa mujibu wa Kampuni hiyo, kazi hii inatarajiwa kukamilika katika kipindi kisichozidi miezi mitatu kuanzia sasa. Kwa hiyo, kabla ya mwezi Juni 2006 mawasiliano tunaamini yatakuwa yamefika sehemu ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja.

Kampuni ya *CELTEL* inatarajia kujenga minara Madaba, Hanga, Mbesa, Michiga na Imalinyi kabla ya mwisho wa mwaka huu wa 2006. Minara hiyo itatoa huduma katika barabara ya Njombe - Songea pamoja na vijiji vya Wino, Madaba na Mahanje.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jenista Mhagana kwa kufuatilia kwa karibu sana tatizo la simu za mikononi kwa maeneo aliyoyataja na kumshauri tuendelee kufuatilia katika Kampuni ambazo nimezitaja. Wizara yangu itashirikiana naye na Kampuni husika hadi simu zitakapowafikia wananchi wa sehemu hizo za Jimbo la Peramiho. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jenista na mimi nimefaidi hapo. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri na mazito na yenye kuleta moyo wa kazi mpya na ari mpya ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kumwuliza swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa ametoa maelezo mazuri sana ya mipango hiyo ya wananchi wa Jimbo la Peramiho na wewe mwenyewe utafaidi na watu wengine wote katika maeneo hayo. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari sasa kuja yeye na Waziri wake na Naibu mwingine kushughulikia suala la uzinduzi wa mitambo hiyo wao wenyewe ili kuwapa moyo zaidi wananchi hao? (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mhagama kama tulivyokuahidi jana kwamba tutaendelea kuwa nawe katika shughuli hizi na kwanza mwenzangu Mheshimiwa Makongoro ataanza na mimi nitafuatia. (*Makofi*)

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la simu la Madaba linafanana kabisa kimiundombinu na tatizo la simu kule Lituhi Wilaya ya Mbinga Magharibi. Je, Serikali itaunganisha mipango ya Jimbo la Peramiho na ile ya Lituhi kule Mbinga? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu utafiti umeshafanyika katika maeneo husika, napenda tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutalipeleka ombi lake kwa Kampuni husika ili tuone namna gani wanaweza kufikisha huduma zaidi.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa vile huduma hiyo sasa itapatikana katika barabara ya Njombe/Songea na kwa vile wote tunaelewa umuhimu wa machimbo ya Liganga, je, inawezekana huduma hiyo sasa ikachepuka kutoka Madaba na kuingia Mundindi kwenye machimbo ya Chuma?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema hapo awali kwamba ni kweli kupitia Njombe kwenda Songea kutapita mawasiliano ya simu. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutapeleka maombi yake kwa Kampuni za Simu aone ni namna gani wanaweza kutoa mchipuo kupeleka katika maeneo husika ambayo Mheshimiwa Mbunge yanamkera ya simu.

Na. 77

**Ongezako la Ujambazi wa Kutumia Silaha za Moto**

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALUM** aliuliza:-

Kwa kuwa, ongezeko la wimbi la ujambazi wa kutumia silaha za moto umekithiri sana hapa nchini na umekuwa ukiathiri sana sifa ya Tanzania hasa katika kisiwa cha Amani na kuwafanya raia kuishi kwa mashaka juu ya maisha na mali zao:-

(a) Je, ni matukio mangapi ya ujambazi wa kutumia silaha za moto umezikumba Benki zetu hapa nchini, Maduka ya Kubadilisha Fedha za Kigeni; na ni kiasi gani cha fedha kilichoibiwa kuanzia Januari, 2005 hadi swali hili linapojibiwa?

(b) Je, ni wahalifu wangapi wa matukio ya ujambazi wamepatikana na idadi ya silaha zilizopatikana toka kwa wahalifu hao na ni kutoka maeneo gani ya Tanzania hadi sasa?

(c) Tangu ujambazi wa aina hiyo uanze; Je, ni Askari wangapi na raia wangapi wameuawa kuanzia Januari, 2005 hadi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Salum, Mbunge wa Mtambile, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia Januari, 2005 mpaka tarehe 31 Januari, 2006 kumekuwepo na matukio tisa (9) ya ujambazi wa kutumia silaha za moto ambayo yametokea katika Benki zetu ambayo yamejitokeza katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza na Mara. Katika matukio hayo kiasi cha fedha zilizoibiwa kwa kipindi chote hicho ni Tshs. 16,782,172,419.00.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, wahalifu ambao wamekamatwa mpaka hivi sasa ni arobaini na sita (46) kati yao kumi na wawili (12) ni raia wa Kenya. Aidha, katika matuko hayo ya ujambazi katika Mabenki na maduka ya kubadilisha fedha za kigeni hakuna silaha zote zilizokamatwa mpaka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio rahisi kubainisha wahalifu hao wametoka katika maeneo gani hapa nchini, hii inatokana na mwingiliano wa makabila na uhuru wa makazi ndani ya nchi. Hata hivyo kwa matukio ya Mkoa wa Kilimanjaro na Dar es Salaam wahalifu, raia wa Tanzania walikamatwa katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro na Singida.

(c ) Mheshimiwa Naibu Spika, tangu ujambazi wa aina hiyo uanze raia watatu (3) wameuawa na hakuna Askari yeyote aliyeuawa kutokana na ujambazi huo.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Yussuf Makamba ametangaza zawadi ya shilingi 500,000 kwa wale ambao watatoa maelezo yatakayopelekea kukamatwa kwa majambazi. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa zawadi kama hizo au zaidi ya hizo kwa ile Mikoa ambayo imekumbwa na matatizo ya ujambazi? Je, usalama wa hao watakaotoa maelezo kama utakuwaje ? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumfahamisha Mheshimwa Salum kwamba hata Mkuu wa Mkoa ni sehemu ya Serikali. Kwa hiyo hizo fedha anazipata Serikalini na sisi tunaandaa mipango mizuri ya kutoa zawadi nzuri kwa wale ambao watatupa taarifa sahihi za kupambana na ujambazi.

Mheshimiwa Waziri wangu jana hapa wakati akitoa ufafanuzi kwenye Bunge hili Tukufu alielezea suala zima la usiri wa wale ambao watatoa taarifa na namna ambavyo watalindwa. Kwa hivyo nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge mtupe taarifa na hivi sasa tunapata taarifa nyingi kutoka kwa wananchi na zinashughulikiwa. Hata Waziri Mkuu katika hotuba yake alieleza suala hilo, kwa hivi nawahakikishieni kwamba mtalindwa wananchi wote, tunaomba sana wananchi watupe taarifa ili tufanye kazi zetu vizuri. (*Makofi*)

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niulize swali moja dogo la nyongeza.

Katika ujambazi unaotokea kwenye Mabenki na hata Maduka ya Kubadilishia Fedha je, Serikali inachukua hatua gani katika kuwasaidia wale raia wote wanaopoteza fedha zao na hata kupoteza maisha yao wakiwa kwenye maeneo hayo.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika Mheshimiwa Kirigini jana alikuwepo hapa wakati Mheshimiwa Waziri akieleza hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali kupitia Jeshi la Polisi ili kulinda Benki zetu kwa nia ya kupunguza kupoteza mali za wananchi wetu. Kwa wale ambao kwa bahati mbaya wametokea kuibiwa ndani ya Mabenki kwa kweli hayo itakuwa ni dhamana ya wale wenye Mabenki si kwa upande wa Serikali. Kwa msingi huo, tutaomba Benki wazidishe ulinzi ili kuepuka kuibiwa wananchi wetu katika sehemu hizo. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona, nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wa Maziwa matatu hasa Ziwa Victoria, Tanganyika wamelia kwa muda mrefu juu ya ujambazi majini wananchi wamepoteza maisha yao. Kasi hii ya kupambana na majambazi itakuwa na mkakati maalum kwa ajili ya maeneo haya ya Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika pamoja na kasi ya sasa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba wakati huu tunakarabati boti kwa ajili ya kufanya za kupambana na wahalifu katika Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika.

Namwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba kasi yetu itaendelea kwa nguvu zote na kama alivyosema Rais, maadam sisi tunatafuta haki basi dhuluma itashindwa. (*Makofi*)

**MHE. JUMA H. KILIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini ningeomba niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa wimbi la ujambazi limeongezeka sana ili kujenga ufanisi ndani ya Jeshi la Polisi kuna kitu kilikuwa kinaitwa *Criminal Investigation Fund* ambayo ndani yake kulikuwepo *Detective Allowance*. Je, Naibu Waziri atatueleza kwamba Serikali itakuwa tayari kurudisha hiyo motisha kwa Polisi ili kuongeza ufanisi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine Mheshimiwa Mbunge ni siri na hata ninyi hapa Bungeni mlituambia mipango yetu mingine tuifanye siri. Kwa hiyo, naomba muendelee kutupatia nafasi ya kufanya siri. (*Makofi*)

Na. 78

**Utoaji wa Elimu Bora kwa Watoto/Vijana**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE (k.n.y. MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, ili kuondoa umaskini kwa dhati tunahitaji kuanza kutoa elimu nzuri na tena ya Sekondari kwa watoto/vijana wetu; na kwa kuwa, hivi sasa watoto wetu walio wengi wanapata Elimu ya Msingi ambayo haiwezi kukidhi matakwa ya kuondoa umaskini na kutokana na umuhimu huo wa elimu kuwa ndio msingi mkuu wa kuondoa umaskini:-

Je, Serikali itakubaliana na wazo la kufanya Elimu ya Msingi iwe mpaka Darasa la Kumi na mbili na ya Sekondari iwe Kidato cha Tano mpaka Sita kwa watoto wote?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mbunge wa Kwela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeza Mheshimiwa Dr. Mzindakaya kwa kuchaguliwa tena na wananchi wa Jimbo la Kwela kuwa Mbunge wao. Nampongeza pia kwa juhudi zake za kufuatilia masuala ya elimu katika jimbo lake na michango yake mbalimbali katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge naomba kwanza kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 imeweka bayana ngazi mbalimbali za Elimu zinazotakiwa katika nchi yetu. Ngazi ya kwanza ni Elimu ya Awali ambayo hutolewa kwa watoto wa miaka mitano (5) na sita (6). Ngazi ya pili ni Elimu ya Msingi ambayo hutolewa kwa watoto wa miaka saba (7) hadi kumi na tatu (13) na ngazi ya tatu ni Elimu ya Sekondari ambayo hutolewa kwa Kidato cha kwanza hadi cha nne (K1 - K4) kwa vijana wa miaka 14 - 17 na Kidato cha Tano hadi cha Sita (K5 - K6) kwa vijana wa miaka 18 - 19. Utoaji wa Elimu huzingatia mitaala iliyoandaliwa kwa kila rika na ngazi ya Elimu. Kutokana na sera hiyo Wizara yangu ilibuni programu wa Kuboresha Sekta ya Elimu yaani *(Education Sector Development Programme (ESDP)* ambayo ndiyo iliyozaa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) 2002 - 2006 wenye lengo la kuboresha na kuongeza nafasi za Elimu ya Msingi ili ifikapo 2006 kwamba watoto wote wa rika lengwa (miaka 7 - 13) wawe wameandikishwa na kuhudhuria hadi kuhitimu Elimu ya Msingi. Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) wa miaka mitano (5) (2004 - 2009) una lengo la kuboresha na kuongeza nafasi za Sekondari ili asilimia 50 ya watoto wanaohitimu Elimu ya Msingi waweze kuendeleza na Elimu ya Sekondari ifikapo 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa maendeleo ya Taifa lolote hutegemea sana ubora wa elimu inayotolewa kwa raia wake. Aidha, elimu ni nyenzo muhimu katika mkakati mzima wa kupunguza umaskini na kukuza uchumi wa nchi yetu. Pamoja na kukubaliana huko, Elimu ya Sekondari kwa wote inahitaji rasilimali kubwa na maandalizi makubwa ambayo hatujafikia kutokana na uwezo mdogo wa kifedha. Kwa sasa tunajitahidi kuwapa watoto wetu wote Elimu ya Msingi ya miaka 7 na tutaendelea na juhudi za kuongeza nafasi zaidi katika Shule za Sekondari kulingana na uwezo wetu kiuchumi. Wakati huu pia tunafanya jitihada za kutoa mafunzo ya ufundi katika ngazi mbalimbali.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri.

Kwa kuwa ni zaidi ya asilimia 50 ya wanafunzi waliofaulu mtihani wa darasa la 7 hawakupata nafasi ya kujiunga Kidato cha Kwanza. Je, Serikali ina mkakati gani wa dharura kuhakikisha kwamba wanafunzi hao wanapata nafasi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi chote tulichokuwepo hapa Wizara ya Elimu imekuwa ikielezea mikakati iliyoandaliwa kwenye MMES. Hata Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshatoa maelekezo kuwa Wakuu wa Mikoa wote, Maafisa wa Elimu wa Mikoa namna ambavyo wataweza kulitatua tatizo hili na kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inakazana kwa juhudi kubwa kutafuta kiasi cha fedha ili kuweza kuzipeleka kwenye Mikoa kumalizia madarasa ya MMES katika chaguo la pili ambayo ni *Second Selection* wanafunzi hao waweze kwenda kwenye mashule ya Sekondari. Madhumuni yetu ni kuondoa idadi hii ya wanafunzi asilimia 50 waweze kupata nafasi za Sekondari. *(Makofi)*

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya mimi ya kuuliza swali dogo la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Kwa kuwa mara nyingi wanafunzi ambao wamehitimu darasa la 7 wanakuwa na tatizo la kujua lugha ya Kiingereza. Serikali ina mpango gani wa kufundisha lugha ya Kiingereza kwa uzuri kabisa katika shule zetu za msingi ili kuwaandaa wanafunzi wanaoingia Sekondari ukizingatia masomo ya Sekondari yote yanafundishwa kwa lugha ya Kiingereza, tunawaandaa vipi wanafunzi wetu kutoka katika Elimu ya Msingi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimhakikishie kwamba somo la Kiingereza limepewa kipaumbele, mtaala wake umeboreshwa, Walimu wameshapatiwa semina fupi fupi na ndefu na

kwamba tuna uhakika kabisa watafanya vizuri. Kwa kuthibitisha hilo vijana wetu kwenye Shule za Sekondari hushiriki katika kuandika *essay* mbalimbali na wanashinda. (*Makofi*)

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nataka kuishukuru Serikali kwamba Ntobola tumepata chakula ingawaje kuna mtu mmoja amejaribu kuiba na wananchi wamemdhibiti inavyopaswa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Ilichukua miaka 43 toka mwaka 1961 - 2002 kwa Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi kujua kuwa kwamba tuna tatizo la watoto kutoingia darasa la kwanza mpaka la saba. Walipopata habari hiyo ndiyo katika miaka miwili au mitatu tumeweza kuingiza watoto zaidi ya milioni 7.5. Sasa swali. Watoto ambao wako katika Shule za Sekondari ni 500,000 tu na watoto wanarudishwa wakiwa na miaka 13 nyumbani. Ni lini Serikali itagundua kuwa wanawakosesha haki ya msingi watoto hawa wa Tanzania na mara moja waanze kuwa na mpango wa *Universal Secondary School* kwa kila mtoto wa Tanzania apate haki ya kumaliza darasa la 12?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nimkumbushe Bwana Cheyo kwamba nchi hii ilianza mikakati yake ya kutaka vijana wote wapate elimu mwaka 1978 tulipokuwa na *Universal Primary Education*. Kwa hiyo, kurudia tena mwaka 2000 si kwamba tulisahau.

Pili, ni lengo la nchi yoyote ile kuhakikisha kwamba vijana wake au watoto wake wanapata elimu bora kutokana na hali ya uchumi kujipanga ni muhimu. Nchi hii imeweka kipaumbele kwamba wote wapate Elimu ya Msingi na tunajipanga vizuri kwamba itakapofika mwaka 2010 wanafunzi wote wapate elimu. Kwa kuzingatia hilo, Mheshimiwa Rais Awamu ya Nne ameongezea Wizara ya Elimu, Mafunzo ya Ufundi na hapo watoto hawa wenye umri mdogo ambao wataishia darasa la saba wachache wao watapata Stadi za Maisha na wale watakaoendelea Sekondari watapata zaidi. (*Makofi*)

Na. 79

**Uwakilishi Unaolingana**

**MHE. GRACE S. KIWELU** aliuliza:-

Kwa kuwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Tatu alipokuwa na baadhi ya Viongozi wa Vyama vya Upinzani alisema kuwa yapo mambo yanayoweza kuzungumzika kama suala la "*Proportional Representation*" pamoja na muundo wa Muungano:-

Je, Serikali ya Awamu ya Nne inasemaje kuhusu jambo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria napenda kujibu swali la Mheshimiwa Grace Sindatu Kiwelu, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano Awamu ya Tatu kuahidi kulizungumzia suala la kuanzisha Wabunge wa Viti vya Uwiano, Serikali ilileta mapendekezo ya Mabadiliko ya Katiba ya Nchi, na Bunge lilifanya Mabadiliko ya Kumi na Nne ya Katiba ya Nchi ambayo yanawezesha Wabunge Wanawake wa Viti Maalum, kuchaguliwa kwa kuzingatia uwiano wa kura. Kwa mujibu wa Mabadiliko hayo, Ibara ya 78 ya Katiba sasa inaweka masharti kuhusu utaratibu wa kuwachagua Wabunge wa Viti Maalum.

Kutokana na utaratibu huu, ni dhahiri kwamba Wabunge wote wa Viti Maalum Wanawake wanachaguliwa kwa utaratibu wa uwiano wa kura. Aidha, Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mabadiliko hayo ya Kumi na Nne ya Katiba idadi ya Wabunge wa Viti Maalum Wanawake imeongezwa hadi kufikia asilimia thelathini ya Wabunge wote. Kwa hiyo, ahadi ya Mheshimiwa Rais ya Awamu ya Tatu kuhusiana na suala hili tayari imeanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuzungumzika kwa hoja ya muundo wa Muungano, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba kwa muda mrefu kumekuwepo na mawazo na hoja tofauti kuhusu muundo wa Muungano kama ifuatavyo:-

* Kwanza, waasisi wa Muungano wenyewe waliamini kwamba muundo wa Muungano wenye Serikali mbili ndiyo unaofaa

* Pili, mwaka 1992 Tume ya Jaji Nyalali ilipendekeza kwamba muundo wa Muungano wenye Serikali tatu ndiyo unaofaa.

* Tatu, zaidi ya 88.87% ya wananchi wote waliotoa maoni yaliyoratibiwa na Kamati ya Jaji Kisanga, (Kamati ya Kuratibu Maoni Kuhusu Katiba), walipendelea muundo uliopo wa Serikali mbili uendelee. Hata hivyo, kwa upande wake, Kamati ya Jaji Kisanga ilishauri kuanzishwa muundo wa Serikali tatu.

* Nne, vipo baadhi ya Vyama vya Siasa vinavyotaka mfumo wa Muungano wenye Serikali tatu. Aidha wapo wananchi wanaopendelea mfumo wenye Serikali moja na kila mmoja anaotoa hoja ana sababu nzuri tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mgongano wa maoni uliopo kuhusu muundo wa Muungano, na pia kwa kuzingatia ukweli kwamba pendekezo la wananchi walio wengi ni muundo wa Muungano wenye Serikali mbili, Serikali bado inaona umuhimu wa kuendelea na mjadala na tafakari zaidi kuhusu hoja ya kubadili muundo wa Muungano wenye Serikali mbili. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina swali moja dogo la nyongeza.

Katika hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne alipolihutubia Bunge alisisitiza umoja wa Kitaifa. Je, Waziri haoni sasa ni kipindi mwafaka suala hili la uwiano wa uwakilishi kuzungumzwa na kutekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uwakilishi hasa huu wa uwiano wa kura ni suala ambalo lina sehemu nyingi sana. Kuna namna nyingi sana ya uwiano na zote hizo zinazungumzika. Zinazungumzika vizuri tu lakini zina namna nyingi sana. Sasa sisi tulichagua hii ya wanawake kwa sababu ya kuwakilisha maslahi maalum kwa kundi maalum. Lakini hizo zingine kama Mheshimiwa Mbunge anazifahamu na mimi nazifahamu zipo karibu tano na zote zinazungumzika. Lakini hili kwetu sisi ni muhimu kutokana na hali yetu.

**MHE. HAZARA P. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tatu na Awamu ya Nne inatambua suala hili la uwiano yaani *proportional representation* hasa kwa wanawake tena katika mihimili yote mitatu ya uongozi yaani Bunge, Serikali na Mahakama. Je, Serikali inaweza ikatueleza ni mafanikio gani ambayo yamepatikana hadi leo hasa kwa wanawake kwa mujibu wa utaratibu huu wa uwiano?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge sasa hivi tumefikia asilimia 30 kwa viti hivyo vya uwiano na nafikiri na hili ni ongezeko kubwa. Kwa Mahakama tuna Majaji wengi sasa wameteuliwa wanawake na hii pia ni hatua kubwa sana kwenye Serikali. Ushahidi ni juzi tu hapa Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu na Wakurugenzi mbalimbali wanawake wameteuliwa katika Serikali na Mawaziri. (*Makofi*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa mfumo wa Serikali haupaswi kuwa ni Sera za Chama chochote kile cha siasa ni suala ambalo wananchi wanakuwa na mfumo, hawaoni kwamba muda umefika sasa Watanzania kutoa mfumo hasa wa Serikali ambao vyama vyote vya siasa vitafuata mfumo huo badala ya sasa chama kimoja kinasema Serikali mbili, kimoja tatu, kingine moja. Je hatuwezi kuitisha kura ya maoni ili kupata maoni ya wananchi juu ya mfumo bora wa Serikali? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumpongeza Naibu Waziri wa Katiba na Sheria kwa majibu mazuri aliyoyatoa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa Serikali mbili sio wa mfumo wa chama tawala peke yake. Kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri katika jibu la msingi kwamba kulikuwa na Tume ya Jaji Nyalali na Tume ya Jaji Kisanga, na hawa hawakutokana na chama, wametokana na Serikali na maoni waliyokuwa wanaratibu ni ya wananchi. Kama alivyoeleza Naibu Waziri katika jibu lake la msingi kwamba wananchi

asilimia 88 wanataka Muungano wa Serikali mbili na si vinginevyo. Kwa hivyo ni maoni yangu kwamba Mheshimiwa Mbunge akubaliane na maoni ya wananchi walio wengi kwamba Muungano unaofaa hivi sasa ni wa Serikali mbili sio wa Serikali tatu na kwamba maoni yale ya wananchi yalitokana na wananchi wa vyama mbalimbali na sio wananchi wa chama tawala peke yao.(*Makofi*)

Na. 80

**Uchimbaji wa Madini**

**MHE. SAID AMOUR ARFI (k.n.y. MHE. KABWE ZUBERI ZITTO)** aliuliza:-

Kwa kuwa uchimbaji wa madini ni shughuli nyeti katika uchumi wa nchi yoyote duniani; na kwa kuwa Mkoa wa Kigoma ni mmoja ya Mikoa inayotajwa kuwa na hazina ya madini:-

(a) Je, ni kampuni gani kutoka nchi ya Australia iliyopata kibali cha kuchimba madini ya *nickel* Mkoani Kigoma?

(b) Je, kampuni hiyo inatafuta madini hayo katika Wilaya ipi, Kata ipi na kijiji kipi Mkoani Kigoma?

(c) Je, wananchi wa Kigoma wanafaidika vipi na uchimbaji wa *nickel* Mkoani kwao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mkoa wa Kigoma kiolojia upo kwenye ukanda wenye miamba ambayo ina madini ya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na *base metals kama nickel, copper, cobalt; platinum group of minerals (PGM);* dhahabu na madini ya chokaa.

Kutokana na hali hiyo, katika eneo hilo kuna leseni zipatazo sitini za utafutaji mkubwa wa madini ambazo zimetolewa kwa kampuni mbalimbali, leseni nyingi kati ya hizo ni kwa ajili ya utafutaji wa madini ya *base metals* ambayo yanahusisha pia madini ya *nickel* Mkoani Kigoma. Kwa sasa hakuna leseni kubwa ya uchimbaji wa madini hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo haayo mafupi naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya *Goldstream* ya Australia iliingia ubia na kampuni ya *Nyati Mining Tanzania Limited* ya Tanzania na kuchukua leseni za kutafuta madini Mkoani Kigoma. Kampuni hii haijaanza kuchimba madini ya *nickel* bali inatafuta madini hayo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni hiyo inatafuta madini katika maeneo ya Mibango, Kapalagulu, Kusini mwa Mkoa wa Kigoma.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa utafutaji wa madini bado unaendelea Mkoani Kigoma. Pindi uchimbaji utakapoanza kwa kadri ya matokeo ya utafutaji huo, wananchi wa Kigoma watafaidika na ajira, huduma za Hospitali, elimu na maji kwa vijiji vinavyozunguka mgodi tarajiwa, soko la mazao na biashara mbalimbali. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa sekta ya madini imekuwa ikilalamikiwa kwa makampuni madini ya nje yanayochimba madini hayalipi kiwango kinachoridhisha kwa Taifa kulingana na mikataba iliyowekwa.

Je, Serikali ina mpango wowote wa kuthaminisha madini yetu kabla na inapoingia mkataba wa uchimbaji na kuweka sharti ili mchimbaji anapochimba aweze kujua cha kulipia ni thamani ya madini yetu yaliyo ardhini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, jana hapa Bunge tulieleza kwamba kampuni ya *Alex Stewart Assayers* imechukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kufanya utafiti katika migodi mbalimbali ambayo inachimba madini hapa nchini kutokana na kazi ambayo inafanya kampuni hiyo tunaweza tukafahamu ni kiasi gani cha madini ambayo yanachimbwa na makampuni hayo kwenye migodi yetu na kiasi gani kinapelekwa nje ya nchi.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza ingawa sehemu kubwa alikuwa amelijibu. Kumekuwa na malalamiko sana juu ya uchimbaji madini hasa kwa makampuni makubwa hapa nchini na tangu mwaka juzi iliundwa Tume kwa ajili ya kufuatilia matatizo yaliyopo na yakaonekana kuna matatizo mengi na kunahitajika marekebisho. Je, Serikali ni lini sasa itafanya hima kurekebisha sheria hiyo ya madini na kuanza kuangalia mikataba hiyo ili wananchi wapate haki yao kwa sababu sasa hivi wanaendelea kuchimba na madini hayo yanakwisha?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kwamba Serikali iliunda Tume maalum ambayo Mheshimiwa Mbunge alikuwa ni mmoja wa wajumbe. Pili, Serikali sasa hivi inaandaa utaratibu wa kuhakikisha kwamba maoni yaliyotolewa katika Kamati ile iliyoongozwa na Dr. Jonas Kipokola yanafanyiwa kazi.

Ningemwomba Mheshimiwa Mbunge atupe muda ili tuyafikishe haya ndani ya Serikali na baada ya hapo ndiyo tutaendelea na utaratibu mzima. Kama nilivyosema jana

ni kwamba suala zima la madini na thamani gani nchi inapata kutoka kwenye madini ni suala ambalo tunalifanyia kazi hivi sasa. *(Makofi)*

Na. 81

**Mahitaji ya Umeme - Singa na Nkungi**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Shirika la Ugavi wa Umeme *TANESCO* lina jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa umeme unawafikia walengwa na walengwa wanaoulipia umeme huo wanapatiwa huduma hiyo kwa uhakika;

(a) Je, kwa nini kijiji cha Singa kilichoko Iramba Mashariki kisipatiwe umeme ambao unapita kijijini hapo kwenda Hospitali ya Nkungi?

(b) Je, kwa nini wananchi wa Nkungi hadi leo hawajapatiwa umeme wakati upo watu ambao tayari wameshalipa umeme huo na wengine wanazo fedha tayari kulipia?

(c) Kwa kuwa, wananchi wa Singa na Nkungi wameshalipia gharama za kupelekewa umeme kwenye nyumba zao. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo;-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umeme *TANESCO* wameandaa mipango thabiti ya kuvipatia umeme vijiji vilivyoko kando kando ya laini ya umeme katika sehemu mbalimbali za nchi yetu. Ili huduma hiyo ya umeme iweze kuwafikia wananchi walio wengi. Vijiji vilivyotajwa na Mheshimiwa Mbunge ni kati vijiji vingi ambavyo vinapatiwa na njia za umeme na viko kwenye mpango huo wa kupatiwa umeme kadri ya upatikanaji wa fedha na vifaa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Singa ni mojawapo ya vijiji ambavyo viko kando kando ya njia ya umeme wa msongo kilovoti 33 kutoka Mtinko hadi Nkungi ambavyo vitapatiwa umeme kutoka katika laini hii ya umeme. Kazi ya kukipatia umeme kijiji hiki imeshaanza. Nguzo 10 za laini ndogo tayari zimepelekwa hapo kijijini. Vifaa vingine kwa ajili ya kutekeleza kazi hii vinasubiri kununuliwa pindi hali ya kifedha ndani ya Shirika itakapokuwa nzuri.

(b) Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Nkungi kina jumla ya wateja 27 ambao tayari wamepatiwa umeme na *TANESCO*. Wateja 3 bado hawajajengewa *service line;* utaratibu unakamilishwa ili wateja hawa waweze kuunganishwa umeme. Wateja 14 wamenunua fomu za maombi ya awali ya kupatiwa umeme na kazi ya kuwaunganisha wateja hawa 14 inatarajiwa kugharimu shilingi za Kitanzania Milioni 12. Kazi hii inasubiri kuidhinishwa kwa bajeti ya Shirika la Umeme *TANESCO*, na inatarajiwa kuanza mara moja bajeti itakapoidhinishwa.

(c) Mheshimiwa Spika, Shirika linafanya utaratibu wa kukusanya vifaa ili wateja watatu wa kijiji cha Nkungi wafungiwe umeme kabla ya mwisho wa mwezi Februari, 2006. Upatikanaji wa vifaa ndiyo unaokwamisha utekelezaji wa kazi hii kwani vifaa ni vichache na vinanunuliwa kidogo kidogo kutokana na hali mbaya ya kifedha ya Shirika la *TANESCO*.

**MHE. MGANA I. MSINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize swali moja la nyongeza. Nimeridhaka na maelezo ya Naibu Waziri lakini napenda nimuuleze. Je, katika vifaa ambavyo vitanunuliwa mapema ni pamoja na *transformer* ambayo sasa hivi watu wa Singa wanaisubiri kwa hamu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo, *transformer* ni kati ya vifaa ambavyo vitanunuliwa. *(Makofi)*

**MHE. DR. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza, nakupongeza kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Naibu Spika

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa niulize swali dogo la nyongeza. Katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba sera ya *TANESCO* ni kuwaunganishia watu umeme mle ambamo umeme unapita, ninaelewa maana yake ni pamoja na gridi ya Taifa. Sasa kuna umeme unaotoka Mtera unakuja mpaka Dodoma, Manyoni mpaka Singida. Je, ni lini *TANESCO* itawakumbuka hawa watu waliomo humu njiani na vijiji vingi na vingine vimepeleka maombi lakini bado havijapatiwa umeme? Ningependa nijue mkakati ambao Wizara itafanya kutekeleza usemi wao huu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kwamba ni sera ya Serikali na kwa maana hiyo *TANESCO* inatekeleza kwa niaba ya Serikali kusambaza umeme kwenye maeneo yaliyo kando kando na njia kuu za umeme. Lakini sera hiyo hiyo inatoa kipaumbele, kwanza kufikisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya na halafu ndiyo hayo maeneo mengine yakiwemo yale yalikuwa kandokando; na kwa sababu ya umuhimu wa nishati hii ya umeme katika maendeleo ya nchi, Serikali ilileta hapa Bungeni na kupitisha sheria na kuunda taasisi ya umeme vijijini na *fund* maalum ya umeme vijijini. Pia pana mpango wa upelekaji umeme vijijini ili kubadilisha hali ya maisha, *energizing for rural transformation*. Miradi hii yote ndiyo ambayo inatarajiwa kwa kiwango kikubwa kukidhi haja ya kufikisha nishati hii muhimu kwa wananchi ili waweze kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Malecela kwamba kwa upande wa mfuko na taasisi hii ya nishati vijijini tunatarajia kwamba itaanza kazi katika mwaka wa fedha huu unaokuja. Sasa hivi tayari katika bajeti iliyopita ilitengewe fedha ya kuunda na katika bajeti ijayo tunatarajia kwamba shughuli hizi zitaanza. Kwa kadri itakavyowezekana na kadri fedha zitakavyopatikana basi kazi hii ya kififikisha umeme vijijini itakuwa ni kazi ambayo inapewa kipaumbele.

Na. 82

**Ujenzi wa Soko La Kisasa**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBERI (k.n.y. MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, moja kati ya azma nzuri ya Serikali ni kujenga soko la Kimataifa, lililopo Kariakoo soko ambalo hivi sasa halikidhi haja hata kidogo kutokana na ongezeko kubwa la wafanyabiashara na watumiaji.

Je, Serikali haioni kwamba wakati umefika wa kubuni mpango mwingine wa ujenzi wa soko ambalo litaonekana kweli ni la kisasa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa soko lililoko Kariakoo hivi sasa limekuwa dogo ikilinganishwa na mahitaji ya wafanyabiashara na watumiaji. Hali hiyo imefikiwa kwa sababu soko hilo lilijengwa mwaka 1974 wakati Jiji la Dar es Salaam likiwa na wakazi takribani 450,000 tu. Hivi sasa Jiji la Dar es Salaam linawakazi wapatao milioni tatu. Aidha, kwa sasa idadi ya wafanyabiashara na watumiaji wa soko la Kariakoo inakadiriwa kuwa kati ya 250,000 na 300,000 kwa kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inachukua hatua zifuatazo za kupunguza msongamano wa watu katika soko la Kariakoo:-

(i) Kuidhinisha mpango wa Shirika la Masoko Kariakoo wa kupanua Soko la Kariakoo kwa kujenga jengo la gharofa tatu mashariki mwa Jengo Kuu la Soko hilo. Michoro ya Jengo hilo inaandaliwa na itakamilishwa mwaka 2006/2007 na hivyo kuwezesha Shirika kutafuta wawekezaji wa kufanikisha ujenzi huo.

(ii) Kuridhia mpango wa Shirika la Masoko Kariakoo wa kuendeleza viwanja vyake vilivyoko Tabata vyenye ukubwa wa eneo la mita za mraba 5,800 ili kujenga *"Shopping Centre"* pamoja na soko dogo (*mini supermarket)*.

(iii) Serikali pia inahimiza Halmashauri za Manispaa ya Ilala, Kinondoni na Temeke kuwa na mipango ya kuboresha masoko yote yaliyo chini ya Halmashauri hizo, hususani ujenzi wa majengo mapya au ukarabati majengo yaliyopo, kuboresha sehemu za kuegesha magari, vyoo na vitendea kazi vingine. Kwa mfano, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala imekamilisha upembuzi yakinifu wa kujenga upya soko la Kisutu ili likidhi mahitaji ya wafanyabiashara na watumiaji.

Mazungumzo baina ya Halmashauri hiyo na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Serikali za Mitaa *(LAPF)* pamoja na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* yanafanyika ili kutekeleza mpango huo kwa ubia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaamini kuwa utekelezaji wa miradi kama niliyoieleza hapo juu ndiyo utatoa ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la msongamano wa watu katika Soko la Kariakoo.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwa vile Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kuwa msongamano ni mkubwa wa Kariakoo na anasema upo mpango wa kufanyia ukarabati jengo lililipo hivi sasa si bora kuliacha kabisa kujenga upya mahali ambapo pametengwa hivi sasa kuhakikisha linakuwa kubwa zaidi kuliko pale Kaliakoo ambapo kuna msongamano mkubwa zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli busara ingeonyesha kwamba afadhali kujenga sehemu nyingine kuliko kujenga pale. Lakini lile jengo lilivyo na eneo ambalo ni la jengo lile liko katikati na tunaweza kusema ni *strategic* kwa sababu watu walio wengi wapo pale karibu na Kariakoo. Ili kutoweza kutoa misongamano katika maeneo mengine, nimekwishasema kwamba maeneo mengine ya Ilala, Temeke na Tabata yatajengwa ili kusudi na watu wa pale katikati ambapo wageni wengi wanafika Kariakoo inabidi wakute soko la kisasa ambalo litakuwa kioo cha Taifa. Kwa hiyo na lenyewe itabidi kuliboresha ili lifanane na masoko mengine ya Kimataifa.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa sababu hizo hizo ambazo zimetajwa katika jibu la msingi, tuna sababu gani la kulifanya soko la Kijitonyama ambalo tayari linajengo zuri na mazingira mazuri mpaka sasa hivi halitumiwi kikamilifu eti kwa sababu lile eneo la kupitishia mabasi ya daladala halijafunguliwa? Je Serikali itaisaidiaje Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni kufanya soko hili la Kijitonyama ambalo ni nzuli kukamilisha azma yake?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kweli si vyema kutumia rasilimali yetu ndogo tuliyonayo tukajenga kitu

kama soko la Kijitonyama halafu likakaa wazi. Matatizo aliyoyazungumza Serikali tunayafahamu na tutayafanyia kazi kusudi liweze kutumika ili rasilimali yetu iweze kuwanufaisha Watanzania.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatana na suala msingi ambalo limeulizwa, ningependa tu kuuliza kuhusu soko la umeme. Mheshimiwa Waziri pamoja na majibu yake mazuri ana mpango gani kututafutia soko la umeme katika migodi ambayo kwa mfano kule Tarime kampuni ya mgodi inatumia fedha nyingi sana za kigeni kununua mafuta Kenya zile fedha zingeweza kutumika kwa matumizi mengine endapo soko la umeme wa *TANESCO* ungeweza kupelekwa pale kwenye mgodi?

**NAIBU SPIKA:** Nilivyoelewa mimi ni soko la kununua mahitaji ya nyumbani kama nyanya na vitu vingine sio umeme.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa soko la Kariakoo hutumia barabara za Mtaa wa Pemba na Sikukuu, Pemba na Swahili kutokea Mtaa wa Mkunguni hutumiwa kwa kupakia na kupakuliwa mazao ya nazi ambayo mengi yanatoka Wilaya ya Mafia, Rufiji, Kilwa, Lindi na Tanga na kwa kuwa maeneo yale yako wazi na nazi ni zao ambalo likipata jua hukatika na kupungua thamani na ikinyeshewa na mvua huwa inaharibika kwa kuoza. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha eneo lile la Mtaa wa Pemba ama kuzinunua nyumba zile zilizokuwa kati ya Pemba na upande wa pili wa soko la Kariakoo ili waweze kulitanua soko hilo na kuweza kulijengea paa ambalo litaweza kuhifadhi mazao ya nazi na mazao mengine yatakayofika hapo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika katika jibu langu la msingi, nimeeleza mipango ya kupanua soko la Kariakoo na kulifanya la kisasa ni pamoja na kuzingatia hayo kwamba hizo nafasi ambazo alikuwa anazizungumzia kweli huwa na magari yanateremshia nazi na wakati mwingine inakuwa hata msongamano wa magari mengine ya abiria kule njiani. Tunaamini kwamba kwa kumaliza huu mpango wa Kariakoo ambao ni wa kisasa na kuwa na masoko mengine yakatayojengwa kandokando ya Jiji yatapunguza msongamano na kupata nafasi ya nazi mahali ambapo patakuwa pametengewa.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa watu wanaofanya kazi Dar es Salaam wengine huishi Kibaha au Mkuranga au wanaofanya kazi Mkurunga huishi Dar es Salaam na kwa kuwa mazao mengi yanatokea Bara kupitia Kibaha na yanayotoka Kisiju hupitia Mkuranga. Je, haoni sasa ni wakati mwafaka badala ya kuifanya Dar es Salaam imejaa tutumie maarifa sasa ya kuwa na masoko kama hayo Kibaha au Mkuranga?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tunatambua kwamba hatutaki masoko yote yawe Dar es Salaam.

Kuna mipango maalum ambayo ni mipango miwili ya kuboresha masoko ya vijijini. Mpango mmoja ni *AAMCDP* ambao ulikuwa ni ubia kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ufarasa ambao tumeumaliza mwaka 2003. Umeunganisha program ya haya masoko ambayo mmeyaona kama hili la Kibaigwa.

Sasa kuna mpango mwingine ambao ulikuwa unaendelea mpaka sasa hivi ambao wenyewe unaangalia hivyo hivyo kuboresha masoko ya vijijini kusudi si kuleta Dar es Salaam tu hata wenyewe huko vijijini tuwe na masoko ambayo ni rahisi yanakuwa kama *mini markets* ambayo wakulima wenyewe wanaweza kuyafikia kwa urahisi ili wasiweze kudhulumiwa kwa kutumia m-*agent* kwa sababu sio kila mkulima anaweza kufika Jijini Dar es Salaam.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda umekwisha, naomba nitoe matangazo machache.

Kwanza kabisa kuhusu taarifa ya vikao. Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, anatangaza kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira wakutane saa tano asubuhi katika Ukumbi wa Erasto Mang'enya, chumba 231, ghorofa ya pili Jengo la Utawala.

Kikao kingine, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mwenyekiti wa *TAPAC,* Chama cha Wabunge na Mambo ya UKIMWI, anatangaza kwamba Wabunge wote wanachama wa Umoja wa Wabunge wa kupambana na UKIMWI, *TAPAC*, watakuwa na kikao cha wanachama wote wapya na wa zamani mara baada ya kuahirisha Bunge leo mchana katika ukumbi huu, maana yake ni baada ya saa saba. Wale wanaotaka kujiunga na *TAPAC* na waliokuwepo watakuwa na mkutano wao humu ndani saa saba.

Tangazo lingine; ninawatangazia wale wote ambao wananuia kununua magari kupitia Kampuni ya Toyota; wakutane na watu wa Toyota hapo nje ili wakamilishe taratibu zinazohusika na wale ambao wanataka kununua pia waende na wale wanaotaka kununua wakati wa mwaka wa fedha mpya nao wajiorodheshe kusudi waanze kuagiza magari hayo kama mnataka. Kwa hiyo, mnatangaziwa kwamba watakuwa hapo nje. Mnaanza kufanya maandalizi pesa itajulikana huko huko. (*Kicheko*)

Tangazo la mwisho, kuna mtu amesahau simu yake. Ameshapatikana.

Baada ya hapo Katibu endelea!

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Kusimamia Maeneo Maalum ya Uwekezaji Rasilimali (*The Special Economic Zones Bill 2006)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa na wananchi wa Urambo Mashariki kuwawakilisha katika Bunge hili katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Aidha, nampongeza kwa kuchaguliwa kwa kauli moja kuwa Spika wa Bunge hili Tukufu. Chini ya uongozi wake nina hakika Bunge hili litakuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 kwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya. Pia nakupongeza Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuchaguliwa kwa kauli moja kuwa Naibu Spika wa Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo furaha pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa na wananchi kuwawakilisha katika Bunge hili katika kipindi cha miaka miatano. Nawashukuru Watanzania wenzangu kipekee kwa kukipatia Chama Cha Mapinduzi ushindi mkubwa katika uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005, hivyo kuonyesha imani kubwa kwa uongozi wa Chama chetu na uongozi wa Mheshimiwa Jakaya Kikwete Rais wetu mpendwa wa Awamu ya Nne. Nampongeza sana Mheshimiwa Kikwete kwa ushindi wa kihistoria tangu tuingie katika Mfumo wa Vyama vingi vya Siasa. Nawapongeza pia Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Edward Lowassa, Mbunge wa Monduli, Waziri Mkuu na Mawaziri wenzangu wote na Manaibu Waziri wote kwa kupata nyadhifa walizonazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana wapiga kura wa Jimbo la Ulanga Magharibi kwa kunipa ushindi wa kishindo sasa ikiwa mara yangu ya tatu. Nawaahidi nitawatumikia kwa makini, mahiri, bidii na heshima kwa uwezo wangu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mswada wa Sheria ya Usimamizi na Uendelezaji wa Maeneo maalum ya Uwekezaji Rasilimali yaani *Special Economic Zones* ya mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika adhima ya kupiga vita umaskini, Serikali iko katika awamu ya pili ya kutekeleza mpango wa kupunguza umaskini nchini chini ya mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Katika awamu ya kwanza, Tanzania iliweza kupata mafanikio kadhaa hasa katika maeneo yafuatayo:-

Mosi, kuandaa sera na mipango mizuri ya maendeleo na kupunguza umaskini. Mipango hiyo ni Dira ya Taifa ya Mandeleo ya 2025 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA).

Pili, kutengamaza Uchumi Mkuu (*Macro-Economic Stability)* na kufikia kiwango cha ukuaji cha asilimia 6.7 mwaka 2004 na kudhibiti ongezko la bei kutoka asilimia 27.1 mwaka 1995 hadi asilimia 4.2 Desemba 2004.

Tatu, kuboresha na kuendeleza mazingira ya sekta binafsi na uwekezaji. Nne, kuweka mazingira ya utawala bora na uwajibikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yaliyokwishapatikana hadi sasa bado tunakabiliwa na changamoto katika kufikia haraka zaidi malengo ya dira ya Taifa ya maendeleo 2025. Changamoto kubwa zinazolikabili Taifa letu ni kama zifuatazo:-

1. Kuongeza kasi ya ukuaji wa pato la Taifa hadi kufikia asilimia 8 hadi asilimia 10, viwango vinavyohitajika ili kupiga vita umaskini.

2. Kuongeza kiwango cha mauzo nje ili kuongeza kiasi cha mapato ya fedha za kigeni.

3. Kuongeza wastani wa kipato cha Mtanzania ili kufikia *Middle Income Status* ifikapo mwaka 2025 kama Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inavyotuelekeza.

4. Kuongeza nafasi ya ajira kujibu tatizo la ukosefu mkubwa wa ajira kwa wananchi wetu hasa vijana.

5. Kujenga uchumi wenye uwezo wa ushindani, kikanda na Kimataifa.

6. Kujenga miundombinu ya kiuchumi na kijamii, na

7. Kuongeza elimu, ujuzi na utaalam ili kuongeza tija na ufanisi kwa kutumia maarifa zaidi katika uzalishaji na utoaji huduma kwa jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hii, Taifa linahitaji mikakati ya ziada ili kuongeza kasi ya ukuaji uchumi kama msingi wa kuongeza wastani wa kipato cha Mtanzania, kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma nchi za nje, kupanua nafasi za ajira nchini na hatimaye kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kukabiliana vizuri zaidi na tatizo la umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa kutoa majibu kwa changamoto hizi, Serikali imetayarisha Mpango Maalum wa Kuharakisha Maendeleo ya Tanzania (Ta*nzania Min-Tiger Plan 2020)* kwa kuzingatia uzoefu na mafanikio ya nchi za Kusini Mashariki mwa Asia. Uzoefu wa nchi hizi unafaa kwa maendeleo ya Taifa letu kwa kuwa kiasi cha miaka 40 iliyopita baadhi ya nchi hizo zilikuwa sawa na Tanzania kimaendeleo na nyingine hata kuwa nyuma lakini pamoja na hatua nyingine kwa kuanzisha mipango maalum iliyobuniwa kuwavutia wawekezaji, nchi hizi zimeweza kupiga hatua kubwa sana ya maendeleo wakati nchi nyingi za Afrika hazijaweza kufanya hivyo. Nchi hizi ni pamoja na Jamhuri ya Korea, Malaysia, Thailand, Indonesia, Taiwan na China. Aidha, India, Vietnam na Cambodia nazo zinasonga mbele kwa kasi kubwa na zimeongeza uwekezaji na mauzo nje kwa viwango vikubwa vya kuigwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliokuwemo kwenye Bunge lililopita, watakumbuka kwamba Serikali iliandaa semina maalum juu ya mpango huu kwa Wabunge wote tarehe 7 Julai, 2005 hapa Dodoma. Katika semina hiyo, Waheshimiwa Wabunge walichambua kwa undani mpango huu na kuitaka Serikali iandae taratibu za utekelezaji bila kuchelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muhtasari; mambo makubwa tunayojifunza kutoka nchi hizi za Asia Kusini Mashariki na ambayo yalikuwa chachu ya maendeleo yao makubwa na ya haraka ni pamoja na haya yafuatayo:-

1. Nchi za Kusini Mashariki mwa Asia zilitekeleza kwa makusudi mipango yao ya kukaribisha na kuharakisha uwekezaji wa sekta binafsi kutoka ndani na nje ya nchi zao.

2. Mipango hiyo ilikuwa ndio agenda kubwa kwa kila nchi husika na ilisimamiwa na viongozi wakuu wenyewe wa nchi hizo.

3. Nchi zote zilitumia maeneo maalum ya uwekezaji rasilimali ili kuvutia wawekezaji. Hii ilisaidia kuzalisha kwa gharama nafuu na hivyo kuhimili ushindani wa Kimataifa. Wananchi wa nchi hizo walinufaika kupitia ongezeko la ajira, mapato ya fedha za kigeni na ukuaji wa uchumi kwa ujumla.

4. Wadau wote ikiwa pamoja na viongozi wa ngazi zote waliheshimu mipango na maamuzi yao. Kila mmoja alitekeleza wajibu wake kwa ufanisi, maarifa na bidii ya hali ya juu.

5. Nchi hizi ziliweza kuondoa ile dhana ya "*can't do*" - haiwezekani na kujijengea mtazamo wa "*can do*" - inawezekana.

6. Nchi hizo zilitoa kipaumbele katika kwanza kutafiti mahitaji ya soko kabla ya kuzalisha kwani wazalishaji wanaofanikiwa ni wale wanozalisha baada ya kufahamu kinachohitajiwa na soko ikijumulisha viwango vya ubora wa bidhaa na siyo wale wanaozalisha kwanza ndipo watafute soko.

7. Ili tutoke katika umaskini, ni muhimu tuongeze wingi na ubora wa mazao yetu ya kilimo na pia tujenge viwanda vya kusindika mazao na matunda ili kuyaongezea thamani (*Value Addition).* Hii itaongeza tija na kipato. Ni muhimu pia tuongeze uhakika na ubora wa huduma za ndani na pia tusababishe na tuwezeshe ongezeko la tija katika sekta ya kilimo.

8. Hatua zilizochukuliwa na Serikali hizo zilienda sambamba na kutoa kipaumbele katika elimu, miundombinu, sera bora za uchumi, uwekaji amana (*savings*) na mauzo nje.

Tanzania tunahitaji kuhamasisha na kuendeleza yote haya kwa vitendo kwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango Maalum wa Kuharakisha Maendeleo ya Tanzania (T*anzania Min-Tiger Plan 2020*), unakusudia kuiwezesha Tanzania kufikia malengo yafuatayo kufikia mwaka 2020:-

1. Kuongeza pato la Taifa hadi kufikia dola za Kimarekani 40 bilioni kwa mwaka kutoka dola za Kimarekani 10 bilioni kwa sasa

2. Kuongeza mchango wa sekta ya viwanda kwenye pato la Taifa kutoka asilimia 8 ya sasa kufikia silimia 15 – 25 ifikapo mwaka 2020 kwa mwaka.

3. Kuongeza mapato ya fedha za kigeni yatokanayo na bidhaa zinazouzwa nje kutoka dola za Kimarekani 1.2 bilioni kwa mwaka hadi kufikia dola za Kimarekani bilioni 20.

4. Kufikia wastani wa ukuaji wa uchumi wa asilimia 8 hadi 10 kwa mwaka kutoa asilimia 6.7 kwa mwaka 2004, viwango ambavyo vitatuwezesha kupunguza umaskini nchini mwetu.

5. Kuongeza pato la wastani la Mtanzania kwa mwaka kutoka dola za Kimarekani 286 hadi kufikia dola za Kimarekani 1000.

6. Kuongeza ajira mpya kati ya 2,000,000 na 3,000,000 ifikapo 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati huu, Mpango Maalum wa Kuharakisha Maendeleo ya Tanzania 2020, ni kuhakikisha Tanzania inapata sehemu kubwa zaidi ya uwekezaji rasilimali duniani ambao una uwezo wa kuleta manufaa yanayolengwa na nchi yetu. Hii ni kwa kutambua kuwa wawekezaji wengi wapo tayari kuwekeza katika nchi mbalimbali zikiwemo nchi zinazoendelea ili tu mradi yawepo mazingira mazuri. Mazingira yanayohitajiwa na wawekezaji wote ni pamoja na haya yafuatayo:-

1. Hali ya Utawala Bora unaozingatia mahitaji ya usalama, utawala wa sheria na upigaji vita rushwa. Kwa ujumla Tanzania ina sifa nzuri katika eneo la utawala bora na usalama. Tunawajibika sasa kuendelea kupiga vita rushwa kwa kasi na nguvu zaidi.

2. Sera nzuri za uchumi mkuu; Tanzania imefanikiwa sana katika eneo hili.

3. Miundombinu ya uendeshaji na inayounganisha wazalishaji na masoko. Baadhi ya miundombinu hiyo ni barabara, nishati na maji. Kwa eneo hili, Tanzania ipo nyuma kama ilivyo kwa nchi nyingi zinazoendelea. Sehemu nyingi za nchi yetu hazina barabara nzuri na zinazopitika mwaka mzima. Aidha, sehemu nyingi za nchi yetu zina uhaba wa nishati na maji, hasa kwa ajili ya matumizi ya kilimo na viwanda.

4. Nguvu kazi yenye ujuzi *(Skilled Labour),* Tanzania ina nguvu kazi nyingi na yenye ujuzi lakini juhudi zaidi zinahitajika kiziimarisha ili kuinua tija, maarifa na ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya mpango huu, mazingira mazuri yatawekwa kwa:-

1. Kuchukua hatua za makusudi za kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji Rasilimali *(Special Econimc Zones)* kwa sekta na maeneo yenye fursa kubwa nchini. Maeneo haya yatakuwa na miundombinu inayohitajika kuwafanya wazalishaji wa bidhaa na huduma kuwa na tija na ufanisi unaotosheleza ushindani wa kikanda na Kimataifa. Hii ndiyo sababu ya

kutayarisha Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Maeneo Maalam ya Uwekezaji Rasilimali kwa mwaka 2006.

2. Kuimarisha uwezo wa kutangaza fursa za Tanzania ndani na nje ya nchi hasa kwa kuwa tutakuwa na maeneo maalum ya kuwekeza na sheria ya kusimamia na kuendeleza maeneo hayo. Hii inahitaji ushiriki na msukumo wa viongozi wa ngazi zote nchini tukiongozwa na Rais wetu.

3. Kuweka mfumo wa Usimamizi na uendeshaji wenye ufanisi wa hali ya juu na wenye uwezo wa kutatua kwa haraka matatizo yanayojitokeza kukwamisha uwekezaji nchini. Hii itahitaji kuboresha sheria, taratibu za kiutawala na nguvu kazi. Kwa kuwa mpango huu utahusisha sekta zote na kwa kuwa maamuzi mengi yatahitaji kufanyika haraka, ni muhimu jukumu hili lisimamiwe na Mheshimiwa Rais mwenyewe.

Mheshimiwa Nabu Spika, mbinu muhimu iliyotumiwa na nchi za Asia Kusini Mshariki katika kuvutia wawekezaji, ni kuanzisha kwa maeneo maalum (*Special Economic Zones)* kwa ajili ya uwekezaji wa ndani na nje. SEZ ni eneo kubwa ambalo limetengwa rasmi na kuendelezwa kwa lengo la kuvutia shughuli za kiuchumi chini ya sheria na taratibu maalum hasa kuhusiana na masuala ya kodi, ajira na biashara. Katika nchi za Kusini Mashariki mwa Asia inakadiriwa kuwa asilimia 80 hadi 90 ya vitega uchumi vyote vimewekwezwa katika maeneo haya.

Mhshimiwa Naibu Spika, *SEZ* zina wigo na mtazamo mpana zaidi kuliko *Export Processing Zones (EPZ)* ambazo zina lenga kukuza sekta ya viwanda kwa haraka zaidi *(Fast Tracking Industrialization)* ambayo tunahitaji sana, kwani zinatoa uwezekano wa kuhusisha sekta zote za kuvutia vitega uchumi vinavyolenga kuuza bidhaa zake katika soko la ndani na soko la nje katika eneo moja. Kwa njia hii *SEZ,* zina uwezo mkubwa wa kupunguza gharama za uzalishaji kwa kuwa na wawekezaji wengi wanaochangia kulipia gharama za huduma za jumla (*Common Services*) kumaliza ujenzi wa barabara, kuunganisha umeme, kuunganisha simu, kuvuta maji, kuondoa maji taka, usalama na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa kutumia dhana ya *SEZ* unatokana na ukweli kwamba kwa nchi maskini kama yetu ni vigumu kuweka miundombinu inayohitajika kwa ajili ya uzalishaji kote nchi katika kipindi kifupi. Jawabu la kuanza na maeneo maalum kwa vile hatuna uwezo wa kuweka Miundombinu katika nchi yote kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la mpango ni kuanzisha maeneo maalum kiasi cha 25 – 30 nchini ifikapo mwaka 2020. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, lengo ni

kuanzisha maeneo maalum manne kwa ajili ya shughuli za viwanda, kilimo, utalii, upandaji miti, *ICT (Science Cyber Parks)* n.k. Tumeanza na kujenga eneo moja maalum katika sehemu ya *RTD External Service* Mabibo Dar es salaam. Eneo hili la kuanzia limechaguliwa kwa kuzingatia ukaribu wake na barabara ile Mandela *Express Way*, Bandari ya Dar es salaam, Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Mwalimu Julius K. Nyerere na upatikanaji wa miundombinu mingine, hususan maji na umeme. Litakapokuwa tayari, eneo la Mabibo litakuwa na uwezo wa kutoa ajira mpya zisizopungua 20,000.

Kwa heshima na kwa kutambua mchango na msukumo mkubwa wa Rais wa Awamu ya Tatu, eneo hili linalojengwa *SEZ* la kwanza nchini linaitwa *Benjamin William Mkapa Special Economic Zone. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifano ya baadhi ya rasilimali zinazoweza kuendelezwa kwa utaratibu wa *SEZ.* Wakati wa kutayarisha mpango huu wataalam wetu walikishirikiana na wataalam kutoka *Japan Development Institute,* walitembelea Zanzibar na baadhi ya Mikoa ili kubaini fursa ambazo zinaweza kuwavutia wawekezaji.

Mikoa iliyotembelewa ni pamoja na Dar es salaam, Mwanza, Arusha, Kilimanjaro, Kigoma, Tanga Morogoro, Iringa, Mbeya na Mtwara. Kwa ujumla Mikoa ilionyesha utayari mkubwa na fursa nyingi zilidhihirika katika sekta za kilimo, ufugaji, misitu, uvuvi, madini, viwanda, utalii na *ICT.* Baadhi ya maeneo mahsusi yenye uwezo wa kuvutia wawekezaji kwa kutumia maeneo maalum ni haya yafuatayo:-

1. Kilimo cha maua, mboga na matunda na kilimo cha mazao mapya kama *Soya beans* na *bamboo shoots.* Wakati tunaendeleza mazao asilia, ni muhimu kuanzisha kilimo cha mazao mapya kwa kuzingatia zaidi mahitaji ya sasa ya soko la ndani na la Kimataifa.

   Mwenendo wa biashara duniani unaonyesha kwamba, mazao ya maua, *Soya beans, Bamboo Shoots,* mboga, mahindi, mpira, matunda *(apple, pears na plumbs*) yataendelea kuwa na soko zuri. Tanzania itanufaika kwa kubainisha maeneo mazuri ya kuvutia wawekezaji ili kuzalisha aina ya bidhaa hizi zinazotakiwa kwa ubora wa Kimataifa na kwa bei nzuri.

2. Kilimo kwa ajili ya nishati mbadala; Kwa kuwa mkataba wa Kyoto kuhusu Mazingira *(Kyoto Protocol on Climate Change* wa mwaka 1997) umeanza kutumika mapema mwaka 2005. Kwa kuzingatia kuendelea kuongezeka kwa bei ya mafuta ya petroli duniani, uzalishaji wa *Ethenol* na *Bio-diesel* kwa ajili ya kuchanganywa na petroli na dizeli, umekuwa na faida kibiashara duniani.

Mazao yanayofaa kuzalisha bidhaa hizi ni pamoja na miwa, mafuta ya michikichi, alizeti na jatrofa. Kinachotakiwa ni kuendeleza uzalishaji wa mazao haya na kuweka sera na sheria zitakazoendeleza matumizi yake. Kiwanda cha Sukari Kagera kimeonyesha nia ya kupanua kilimo cha miwa kwa ajili ya lengo hili. Aidha, wapo wakulima wa jatrofa Mkoani Arusha na wawekezaji kutoka nje ambao wameonyesha nia ya kuendeleza uwekezaji huu.

3. Upandaji miti na viwanda vya mbao na bidhaa za mbao. Kwa sasa kuna mahitaji makubwa ya maeneo ya kupanda miti kwa ajili ya uzalishaji wa *woodchip*, *palm* na karatasi duniani, na Tanzania inaweza kutumia fursa hii kwa ajili ya maendeleo yake. Mbali na faida za kibiashara, misitu itaboresha mazingira katika maeneo ambayo miti itapandwa.

4. Viwanda vya nguo, viatu, vifaa vya ujenzi, kusindika mazao ya chakula, ngozi na samaki.

5. Ujenzi wa *Boti* za uvuvi. Tanzania inahitaji kuvutia uwekezaji katika kutengeneza boti za uvuvi zinazotumia injini za magari zilizotumika. Kwa sasa uvuvi wa Tanzania una tija ndogo sana kwa sababu ya matumizi ya teknolojia duni. Aidha, Tanzania inayo nafasi nzuri ya kuwa muuzaji wa boti za aina hii katika Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika.

6. Vivutio vya kurekebisha magari na zana za kilimo kwa soko la ndani na Kanda ya Afrika ya Kati na Mashariki *(Reconditional).* Ipo fursa nzuri ya kuanzisha vituo vya kuagiza magari na kutengeneza magari *(Reconditional)* hapa nchini ili kukidhi soko la ndani na soko la nchi jirani.

   Kituo cha aina hii kitawanufaisha Watanzania kwa kuagiza magari na mashine mbali mbali kwa wingi na hivyo kupunguza bei na kuyafanyia reconditioning magari na zana hapa nchini kwani kwa wakati huu tija hasa vijijini ni duni sana kutokana na ukosefu wa zana magari madogo madogo ya kubebea mazao.

   *Reconditioning* itapunguza pia gharama za kuendesha magari hayo; kwa mfano, upatikanaji wa vipuri ambao utafanyika hapa hapa nchini. Uwekezaji wa aina hii utaifanya Tanzania kuwa kitovu cha kusambaza magari na zana za kilimo kwa nchi za jirani za Malawi, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Rwanda, Burundi, Msumbiji, Uganda na

Kenya. Tayari muwekezaji amekwishapatikana na ameishaanza utekelezaji wa adhima hii.

7. Utalii, maeneo maalum ya uwekezaji yanaweza kuanzishwa katika fukwe za Pwani kwa kutumia Dar es Salaam na Zanzibar kama vivutio vikuu vya kuingilia watalii.

   Pili, kuendeleza utalii wa ndani Mijini kwa kuanzisha *Tourist Centres* zenye vivutio kama wanyama ambao si wakali, tamaduni za makabila ya Tanzania, uzalishaji wa bidhaa ndogo ndogo, biashara na burudani mbali mbali.

   Tatu, kwa kuanzisha maeneo maalum yanayounganisha uwekezaji katika shughuli za utalii, uzalishaji wa maua na ukataji na usafisaji wa madini ya Tanzanite. Hii itaongeza biashara na sababu ya ndege nyingi kutua katika Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Kilimanjaro *(KIA)* moja kwa moja na hivyo kupunguza gharama za usafiri wa ndege.

8. Kukata na kusafisha madini; Tanzania ina nafasi nzuri ya kutumia dhana ya maeneo maalum kuendeleza uzalishaji na kuongeza faida ipatikanayo na madini yake, kwa mfano Dhahabu, Almasi ,*Tanzanite* na kadhalika kwa kuvutia wawekezaji wa kukata na kusafisha vito vya thamani wawekeze nchini Tanzania. Hatua hii itaongeza ajira na itaongeza thamani ya madini yetu *(Value Addition through Processing)* hivyo kupata bei nzuri zaidi tukiuza nje ya nchi yetu.

9. *ICT Data Call Centre Project,* Kwa kutumia uzoefu wa nchi kama India, Philippines na Ghana, Tanzania ina nafasi nzuri ya kuanzisha mradi huo. Chuo Kikuu cha Dar es salaam kwa kushirikiana na wadau wengine kinasukuma mbele wazo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ni baadhi tu ya fursa nzuri za kuendelezwa na sekta binafsi kwa kuzingatia malighafi zinazopatikana hapa nchini, kuwepo kwa ardhi nzuri ya kilimo, vivutio vya utalii, soko la ndani na la nje, nguvu kazi iliyoandaliwa vizuri pamoja na mazingira mazuri yaliyowekwa na Serikali kwa njia ya sera sheria na miundombinu kwa kutumia utaratibu wa *SEZ* na kwa kuwa na mfumo mahsusi wa kusimamia na kuendeleza mikakati mbali mbali.

Mfano wa sheria nina uwasilisha mbele ya Bunge hili Tukufu unalenga kufanikisha mpango huu wa maeneo maalum ya uwekezaji rasilimali nchini mwetu, sheria ya uanzishaji maeneo maalum ya uwekezaji rasilimali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo ya mpango maalum wa kuharakisha maendeleo ya Tanzania na fursa zilizopo, naomba sasa nifafanue vipengele muhimu vya Muswada wa sheria ninaouwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu kama ifuatavyo: -

Kwanza ni kuhusu mfumo wa usimamizi na uendeshaji wa *SEZ.* Ili dhana ya *SEZ* ifanikiwe, ni muhimu kuwa na mfumo wa usimamizi na uendeshaji utakaowezesha utekelezaji wa mpango huu kwa haraka, maarifa, tija na ufanisi. Kwa kuzingatia uzoefu wa nchi nyingine na upana wa zoezi hili, inapendekezwa kuanzisha mamlaka ya *SEZ* itakayokuwa chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Rais. Wajumbe wa Mamlaka hii ni Mawaziri wanaoshughulikia masuala ya uwekezaji raslimali, viwanda, fedha, ardhi, Serikali za Mitaa, jinsia, miundombinu, maji, kazi na mazingira pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu Kiongozi na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, wajumbe wengine ni Mwenyekiti wa *Tanzania Private Sector Foundation* na wajumbe wawili watakaoteuliwa na Rais kutoka sekta binafsi. Mamlaka itakuwa na majukumu ya kusimamia masuala yote ya kisera, utaratibu wa jumla wa *SEZ,* kutangaza eneo la ardhi kwa *SEZ* na kuidhinisha fedha kwa ajili ya ujenzi na uendelezaji wa maeneo ya *SEZ.* Aidha, inapendekezwa pawepo na ofisi ya Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya *SEZ.* Ofisi hii itaongozwa na Mkurugenzi Mtendaji atakayeteuliwa na Rais. Hii ndiyo ofisi itakayosimamia majukumu ya kila siku ya utekelezaji wa sheria ya *SES* ikiwa ni pamoja na: -

(a) Kubaini na kutathmini maeneo ya kuanzisha *SEZ* na kuyaendeleza baada ya kupata kibali cha Mamlaka ya *SEZ.*

(b) Kutayarisha na kutekeleza program ya kutangaza *SEZ* ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji Raslimali Tanzania *(Tanzania Investment Centre).*

(c) Kuchambua mapendekezo ya kuanzisha *SEZ* kutoka sekta binafsi na kuyawakilisha kwenye Mamlaka ya *SEZ.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusu utaratibu wa kubaini na kutangaza eneo kuwa *SEZ,* eneo lenye uwezo wa kuchochea maendeleo haraka litatangazwa kuwa *SEZ* baada ya kufanyiwa uchambuzi na Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya *SEZ* kwa kushirikiana na Waziri anayeshughulikia masuala ya Serikali za Mitaa pamoja na Waziri anayeshughulikia masuala na ardhi na baada ya kupata kibali cha Mamlaka ya *SEZ.* Wizara na Taasisi zinazosimamia miundombinu zitashirikishwa katika maandalizi ya *SEZ* toka mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kuhusu utaratibu wa kutoa leseni kwenye *SEZ,* leseni za kuwekeza katika *SEZ* zitatolewa na Mamlaka za udhibiti husika. Leseni zitatolewa kwa vitega uchumi vipya ambavyo thamani yake haitapungua Dola za Kimarekani milioni 5 kwa wawekezaji wa kutoka nje na Dola za Kimarekani milioni 1 kwa wawekezaji wa ndani. Kwa kuwa Serikali itawekeza kiasi kikubwa katika kuandaa

maeneo maalum, ni muhimu wawekezaji watakaofaidika na huduma hizo wawajibike kuwekeza kiasi kikubwa pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nne ni kuhusu vivutio kwa waanzishaji wa *SEZ* na wawekezaji raslimali. Kwa kuwa suala la kuvutia wawekezaji ni lenye ushindani mkubwa Kikanda na Kimataifa, inapendekezwa kuwepo na vivutio maalum kwa makundi matatu yatakayohusika katika kuanzisha *SEZ* na kuwekeza raslimali ndani ya *SEZ.* Aidha, vivutio hivyo vitatolewa kwa vitega uchumi vipya tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni vivutio kwa wajenzi wa *SEZ* (*Category A)* yaani *SEZ Developers*. Ili kuhamasisha Taasisi za umma na sekta binafsi kuanzisha *SEZ* zenye miundombinu ya kisasa, uwekezaji ambao unahitaji kiasi kikubwa cha fedha inapendekezwa vivutio vifuatavyo vitolewe.

(a) Msamaha wa kodi na ushuru wa forodha kwa vifaa na mashine za ujenzi wa *SEZ.*

(b) Msamaha wa kodi ya mapato ya makampuni, kodi ya gawio la salio na riba na *Property Tax* kwa kipindi cha miaka 10 ya kwanza.

(c) Msamaha wa kodi ya forodha, kodi ya ongezeko la thamani na kodi nyingine kwa gari moja la utawala, magari ya wagonjwa, vifaa na magari ya zimamoto na mabasi yasiyozidi mawili ya kusafirisha wafanyakazi.

(d) Ruhusa ya kuingiza nchini wataalam wasiozidi watano, mahitaji ya wataalam zaidi yatafuata Sheria ya Uhamiaji ya mwaka 1994.

(e) Msamaha wa *Stamp Duty* na kodi ya ongezeko la thamani kwenye hati maalum za kisheria.

(f) Ukaguzi wa mizigo chini ya utaratibu wa forodha ufanyike ndani ya *SEZ* husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni vivutio kwa wawekezaji watakaouza zaidi ya asilimia 20 ya bidhaa na huduma kwenye soko la ndani *(Category B).* Kwa wawekezaji wa kundi hili vivutio vifuatavyo vinapendekezwa:-

(a) Kuwepo kwa huduma nzuri za kisasa na zinazokidhi mahitaji ya ushindani.

(b) Kuondolewa kwa kodi za ushuru wa forodha, kodi ya ongezeko la thamani na kodi nyingine kwenye malighafi na vifaa kwa ajili ya uzalishaji ndani ya *SEZ* na kwenye gari moja la utawala, gari

moja la wagonjwa, vifaa na magari ya zimamoto na mabasi yasiyozidi mawili ya wafanyakazi.

(c) Msamaha wa *Withholding Tax* kwenye riba ya mikopo kutoka nje ya nchi.

(d) Ruhusa ya kupewa *visa* ya kibiashara ya miezi miwili kwa wataalam muhimu mahali wanapoingilia.

(e) Kuruhusiwa kuingiza nchini wataalam watano kutoka nje. Wataalam wa ziada watafuata Sheria ya Uhamiaji ya mwaka 1995.

(f) Kutokukaguliwa mizigo kabla ya kuingizwa nchini.

(g) Ukaguzi wa mizigo toka nje chini ya utaratibu wa forodha ufanyike ndani ya *SEZ* husika.

(h) Mwisho, kuwepo na uhuru wa kuhamisha mali inayotokana na faida au gawio na inayotokana na mapato ya kuuza au kufilisi kitega uchumi husika. Aidha, uhuru wa kuhamisha mali utolewe kwa ajili ya kulipia gharama za teknolojia na kulipia wafanyakazi kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, ni vivutio vya wawekezaji watakaouza bidhaa nchi za nje *(Category C).* Hili ni kundi la wawekezaji ambao watauza nje kiasi ambacho si chini ya asilimia 80 ya bidhaa au huduma watakazozizalisha. Kwa maana nyingine, hili ni kundi linalolenga kuzalisha kwa ajili ya soko la nje. Kwa kuwa ni muhimu kuhamasisha mauzo nje, vivutio vifuatavyo vinapendekezwa kwa wawekezaji wa kundi hili.

(a) Upatikanaji wa huduma za miundombinu ya kisasa.

(b) Msamaha wa ushuru wa forodha, kodi ya ongezeko la thamani na kodi zingine kwenye malighafi na vifaa vya uzalishaji.

(c) Msamaha wa kodi ya makampuni, kodi ya gawio la salio na riba na kodi za Serikali za Mitaa kwa kipindi cha miaka 10 ya kwanza.

(d) Msamaha wa kukaguliwa mizigo kabla ya kuingizwa nchini.

(e) Ukaguzi wa mizigo chini ya utaratibu wa forodha ufanyike ndani ya *SEZ* husika.

(f) *Visa* za kibiashara zitolewe kwa wafanyabiashara muhimu kwa kipindi cha miezi miwili mahali wanapoingilia nchi yetu.

(g) Msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwa gharama za huduma na *wharf age charges.*

(h) Kuruhusiwa kuingiza toka nje ya nchi wataalam wasiozidi watano, wataalam zaidi watafuata Sheria ya Uhamiaji ya mwaka 1995.

(i) Wawekezaji wapewe nafasi ya kuweza kupata dhamana ya mikopo kwa ajili ya kuuza bidhaa nje ya nchi yetu *(Credit Guarantee Schemes).*

(j) Kuruhusiwa kuhamasisha faida na gawio pamoja na mapato kutokana na kuuza na kufilisi kitenga uchumi husika. Uhuru wa kuhamisha mali utatolewa pia kwa ajili ya malipo ya mikopo, gharama za kiteknolojia na mishahara ya wafanyakazi kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ni vitutio vinavyohusiana na sheria za kodi ambavyo vitatolewa kwa kufuata taratibu za sheria husika za kodi za nchi yetu. Aidha, karibu vivutio vyote vinavyohusiana na kodi tayari vimetolewa chini ya Sheria ya *TIC* ya mwaka 1997, Sheria ya *EPZ* ya mwaka 2002 au *Customs Management Act* ya mwaka 2004.

Kama ilivyoonyeshwa katika kiambatanisho ‘A’ katika hotuba ambayo mmegawiwa, kivutio kipya cha kodi ‘O’ ni kimoja ambacho ni kwa ajili ya wajenzi wa miundombinu ya *SEZ* tu. Chini ya utaratibu wa *SEZ,* vivutio ambavyo kwa sasa vinatolewa kwa viwanda chini ya Sheria ya *EPZ* ya mwaka 2002 vitatolewa pia kwa wazalishaji wa sekta nyingine ambao watatimiza masharti ya kuuza nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mifano ya nchi zinazotoa vivutio kwa *SEZ* na *EPZs* ni kama ifuatavyo: -

(i) *Philippines,* hakuna kodi ya Serikali Kuu wala Serikali za Mitaa (*National and Local Government Taxes)* kwa wawekezaji wa ndani wa *SEZ.* Asilimia 5 ya pato *(gross income)* litokanalo na biashara ndani ya *SEZ* linakwenda Serikalini.

(ii) *Egypt,* msamaha wa kodi *(Taxes and Duties)* hutolewa kwa kipindi cha miaka 50 kwa wawekezaji kwenye *SEZ.*

(iii) India, msamaha wa kodi ya ushuru wa forodha hutolewa kwa waagizaji wa *Capital Goods, Raw Materials, Consumables, Spares etc*. Vile vile, *Exercise Duty* haitozwi kwa ununuzi wa vifaa hivyo kutoka kwenye soko la ndani na kuna 100% *Income Tax Exemption for 5 years.*

*(iv)* *Beijing Municipality SEZ*, msamaha wa kodi zote hutolewa kwa kipindi cha miaka mitano.

(v) Jordan, msamaha wa ushuru wa forodha na kodi nyinginezo hutolewa kwa uagizaji wa bidhaa. Vile vile, kodi za mauzo *(Sales Tax),* mapato *(dividends),* ardhi na majengo husamehewa.

(vi) Ingawa Kenya haijaanzisha *SEZ,* lakini ina *EPZs* na inatoa msamaha wa kodi ya mapato kwa kipindi cha miaka 10 ya mwanzo pamoja na *Withholding Tax.* Vile vile, inatoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani na kodi ya *stamp*. Miundombinu yote huwekwa na kutunzwa na Serikali. *(Makofi)*

(vii) Ghana hutoa vifuatavyo:-

(a) Msamaha wa kodi kwa kwa bidhaa zinazoagizwa kwa ajili ya uzalishaji na uuzaji bidhaa nje ya nchi.

(b) Msamaha wa kodi kwa asilimia 100 kwa bidhaa zinazoingizwa kwa ajili ya uzalishaji na uuzaji bidhaa nje ya nchi.

(c) Msamaha wa asilimia 100 ya kodi ya mapato kwenye faida kwa kipindi cha miaka 10 na baada hapo kodi ya mapato isiyozidi kiwango cha asilimia 8 hutozwa.

(d) Msamaha wa jumla kwa *Withholding Tax* zitokanazo na gawio kwenye *SEZ.*

(i) Thailand. Serikali ya Thailand hutoa vivutio vifuatavyo kwa wawekezaji:-
(a) Msamaha wa kodi ya ushuru wa forodha na kodi ya ongezeko la thamani kwa vifaa vya mashine na vya ujenzi wa viwanda kwenye *SEZ;*

(b) Msamaha hutolewa kwa kodi ya ushuru wa forodha na kodi ya ongezeko la thamani kwa waagizaji wa malighafi;

(c) Msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwa matumizi ya bidhaa za soko la ndani zilizotumika kwenye uzalishaji; na

(d) Msamaha wa kodi hutolewa kwa bidhaa zinazouzwa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifano hii ya uzoefu wa baadhi ya nchi duniani inasaidia kuelewa zaidi misingi ya mapendekezo ya vivutio kwa wawekezaji wa *SEZ* yaliyomo katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhusiano na sheria nyingine, Sheria za Kazi, Usalama Kazini, Uhamiaji na Mazingira zitatumika ndani ya *SEZ.* Kuhusu usuluhishi wa migogoro, migogoro itakayojitokeza kati ya mwekezaji kutoka nje na Mamlaka ya *SEZ* au Mamlaka ya Leseni kuhusina na uwekezaji kwenye *SEZ* itatatuliwa kwa

majadiliano baina ya pande husika. Endapo utatuzi wa migogoro hiyo utashindikana kwa njia ya majadiliano, taratibu zifuatazo zitafuatwa: -

(i) Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(ii) Taratibu za *International Centre for Settlement of Investment Disputes - ICSID* au taratibu zilizowekwa chini ya makubaliano kati ya nchi au Shirika la Kimataifa husika na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu kuendeleza na kulinda vitega uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mamlaka ya Kutunga Kanuni *(Power to Make Regulations),* Waziri anayeshughulikia uwekezaji raslimali anaweza kutunga taratibu za kusimamia ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya *SEZ* na uendeshaji wa *SEZ.*

Aidha, Waziri wa Fedha kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya sheria hii anaweza kutunga taratibu za kuimarisha udhibiti wa masuala ya kodi ndani ya *SEZ.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makosa ya kuendesha shughuli za biashara bila leseni, mtu yeyote atakayebainika kuendesha shughuli za kibiashara kwenye *SEZ* bila ya leseni kutoka mamlaka husika atatozwa faini isiyozidi Shilingi milioni 15 au kifungo kisichopungua miezi 6 ama vyote viwili kwa pamoja akipatikana na hatia. Endapo ni kampuni, itatozwa faini isiyopungua Shilingi milioi 50. Aidha, adhabu kali zitatolewa kwa watakaotoa taarifa za uongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema mambo yafuatayo:-

(i) Viwango vikubwa vya kasi vya ukuaji wa pato la taifa ndivyo vitatuwezesha kupanua ajira na kuongeza wastani wa kipato cha Mtanzania na hatimaye kupunguza umaskini. *(Makofi)*

(ii) Katika mazingira ya sasa ya ushindani wa kimataifa nchi zote duniani zimeishatambua umuhimu wa kuwekeza raslimali katika maendeleo. Kwa sababu hii, kila nchi inavutia wawekezaji kwa kuboresha mazingira ya uwekezaji. Tanzania haina budi kuzidisha juhudi za kuboresha mazingira yake ya uwekezaji na kuwavutia aina ya vitega uchumi vyenye uwezo wa kunufaisha uchumi na wananchi wake. Hili ndilo lengo kubwa la Muswada huu wa Sheria ya *SEZ.*

(iii) Ni muhimu Mikoa, Wizara na Taasisi zibainishe fursa na aina ya maeneo maalum yanayofaa kuendelezwa na kuyatenga ili kuwavutia wawekezaji.

(iv) Viongozi wa ngazi zote washiriki kwa nguvu zaidi katika kutangaza fursa za Tanzania.

(v) Tujenge tabia ya kutekeleza mipango na maamuzi yetu kwa ukamilifu na kwa wakati.

Kwa tabia ya uchumi wa ushindani hakuna nafasi kwa nchi na watu wanaochelewa kutoa maamuzi au kutekeleza mipango kwani wawekezaji wanao uhuru wa kuwekeza raslimali zao popote duniani maana wanaona na kulinganisha fursa zinazopatikana katika kila nchi. Watawekeza katika nchi ambazo zipo tayari kuwavutia na kuwapa mazingira muafaka ya uwekezaji. Kwa tabia hii ya wawekezaji kwenda mahali popote panapowavutia zaidi, mtaalam mmoja wa Kijapani amewaita *migrating birds*, ambao hutua mahali panapowafaa ambapo amepaita *pond* ili kutaga mayai ya dhahabu *(golden eggs)* na kuongeza idadi yao. Hivyo, ni jukumu letu kujenga *ponds* nzuri ili *migrating birds* waje nchini mwetu kwa wingi. Ni dhahiri kwamba unapokuwa na *ponds* nzuri na nyingi ndipo utapata *migrating birds* wengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ukiwa Sheria ya *SEZ* utatupatia uwezo wa kuzingatia yote haya na kuboresha mazingira yetu ya uwekezaji. Bila kuchelewa tutaanzisha maeneo maalum ya uwekezaji raslimali katika sehemu kadhaa nchini.

Maeneo haya yatatuwezesha kuwavutia wawekezaji na kutangaza kwa nguvu zaidi fursa za nchi yetu. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumeamua kujiweka sawa katika ulimwengu huu wa utandawazi ambapo ushindani haukwepeki na hivyo tutakuwa tunafanya kwa vitendo na tutakuwa na msingi mzuri wa kufanikisha nia yetu ya kuendeleza maisha ya Watanzania kuwa bora kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Waheshimiwa Wabunge, naomba muunge mkono hoja hii ili tuwe na sheria ya *SEZ* itakayotupatia uwezo wa kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji raslimali yatakayosaidia katika kuwavutia wawekezaji nchini mwetu na hivyo kukuza uchumi wetu kwa kasi zaidi na kuupiga vita umaskini kwa uhakika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA – MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi baada ya kuchambua na kujadili Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuweka utaratibu utakaosimamia uanzishaji, uendeshaji na usimamizi wa maeneo maalum ya uwekezaji (*Special Economic Zones)* kwa mwaka 2006. Maeneo ambayo yatakuwa na miundombinu inayohitajika kuwafanya wawekezaji wa nje na wa ndani wa bidhaa na huduma wazalishe kwa tija na ufanisi unaotosheleza ushindani wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuwasilisha maoni ya Kamati, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati

ya Kudumu ya Fedha na Uchumi kwa imani kubwa waliyoonyesha kwangu kwa kunichagua kuwa Mwenyekiti wao. Tutafanya kazi kwa bidii kusaidiana na Serikali na hatimaye kumsaidia Rais katika kutekeleza maagizo mbalimbali kama yalivyoainishwa katika ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wajumbe hao ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Abdallah Omari Kigoda - Mwenyekiti, Mheshimiwa Adam K. Malima - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Charles M. Kajege, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Elisa D. Mollel na Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Omar Sheha Mussa, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Dr. Omari M. Nibuka, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Suleiman A. Saddiq, Mheshimiwa Zitto Kabwe Zubeir, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Ndugu Anselm Mrema, ambaye ni Katibu wa Kamati na Ndugu Hellen Mbeba, ambaye pia ni Katibu wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani za kipekee ziwaendee wananchi wote wa Tanzania kwa kukipatia Chama cha Mapinduzi kura nyingi za Waheshimiwa Wabunge na za Mheshimiwa Rais. Hii ni ishara ya kutosha kuonyesha imani yao kwa uongozi wa Chama chetu na uongozi wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetu wa Awamu ya Nne. Wananchi walipotathmini na kutafakari utendaji wa vitendo vya CCM, hawakusita kutoa imani yao kwa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Aidha, niwashukuru vile vile wananchi wa Jimbo la Handeni kwa imani kubwa waliyonipa kwa kunipa ushindi wa zaidi ya asilimia 80. Nitawalipa kwa kufanya nao kazi kwa nguvu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo furaha kumpongeza Mheshimiwa Samuel Sitta kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Spika wa Bunge letu Tukufu. Napenda vile vile kukupongeza wewe mwenyewe kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Hii ni ishara kubwa kuwa dada zetu na mama zetu wakipewa fursa wanaweza. Chini ya uongozi wenu nina hakika Bunge hili litakuwa na mchango mkubwa kwa wananchi na Serikali katika kufanikisha Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa (Mbunge), kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu na hii inathibitisha imani kubwa waliyokuwa nayo Wabunge kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 70 (2) toleo la mwaka 2004, naomba sasa niwasilishe maoni ya Kamati yangu kuhusu Muswada uliotajwa hapo juu ambao madhumuni na sababu zake ni kuweka utaratibu wa kisheria utakaosimamia uanzishaji, uendeshaji na usimamizi wa maeneo maalum ya uwekezaji raslimali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza na kuiunga mkono Serikali kwa kuleta Muswada huu hivi sasa wenye malengo ya kuharakisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada uliopo mbele yetu umeonekana na Kamati kwamba unatuelekeza kwenye malengo kadhaa ya kuimarisha kasi ya uwekezaji na uzalishaji katika uchumi wetu *(investment drive*), kigezo muhimu katika kukuza uchumi wa nchi yoyote duniani. Muswada huu utatuwezesha kujenga mazingira ya uwekezaji yenye wigo mpana zaidi utakaovutia wawekezaji na vitega uchumi katika sekta zote, zile za huduma na za uzalishaji mali wa moja kwa moja, lengo likiwa ni uwekezaji na uzalishaji wa bidhaa za kuuza katika soko letu la ndani na la nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo maalum ya uwekezaji raslimali, Kamati imeona yatasaidia uboreshaji wa miundombinu kama ujenzi wa barabara, kuunganisha huduma za umeme, simu, maji, usalama na kadhalika. Maeneo haya yatakayoanzishwa yatasaidia kupunguza gharama za uzalishaji kwa kufaidika na misingi ya *economies of scale*. Maeneo haya yatachochea uanzishaji wa viwanda hususan vile vya usindikaji na hivyo kuongeza thamani ya bidhaa zetu.

Aidha, maeneo haya yatachochea uboreshaji na ujasiriamali baina ya wananchi, lakini la msingi zaidi ni kuchochea upatikanaji wa ajira na hivyo kuboresha mapato ya mwananchi mmoja mmoja. Kwa mfano, eneo maalum la Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, linaloanzishwa pale Mabibo Dar es Salaam, linatarajiwa kuajiri zaidi ya wananchi 20,000 litakapokamilika. Hali hii italeta mafanikio na manufaa makubwa si kwa wananchi tu, bali hata katika kukuza soko letu la ndani, uchumi wetu pamoja na kuwawezesha wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete, changamoto iliyopo mbele ya Serikali na Taifa kwa jumla ni kuhakikisha kuwa mafanikio ya kukua kwa uchumi mkubwa *(macro economy)* ni lazima sasa yatiririke kwa wananchi mmoja mmoja hasa vijijini ili kupunguza umaskini wa kipato katika jamii ya Watanzania. Muswada uliopo mbele yetu, Kamati imeona unalenga kuanzisha maeneo hayo maalum na ni moja ya mkakati madhubuti wa kufikia lengo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakapoongeza kasi ya uwekezaji na uzalishaji katika kukuza soko la ndani na lile la nje, pamoja na uboreshaji wa miundombinu kama zilivyofanya nchi za Asia ya mbali, itaisaidia Serikali kufikia malengo iliyojiwekea katika MKUKUTA na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu imetambua kuwa utaratibu huu wa kuanzishwa kwa maeneo maalum nchini petu si jambo geni kwani nchi nyingi zinazoendelea duniani wanafanya utaratibu huu ndio maeneo haya yanaandamana na sheria na taratibu maalum hasa kuhusiana na masuala ya kodi, ajira na biashara. Kwa hiyo, Kamati imebaini kwamba hatuwezi kutumia uwezo lakini lazima uwezo huo tuutumie kwa kuufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kikao cha pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kilichofanyika tarehe 2 Februari, 2006 Kamati yetu ya Fedha na Uchumi, ilipitia vifungu vyote vya Muswada ambapo baada ya majadiliano kamati iliupitisha Muswada pamoja na mapendekezo mbalimbali yaliyolenga kuboresha Muswada ambayo kimsingi Mheshimiwa Waziri aliyakubali. Maeneo yaliyoangaliwa ni pamoja na mfumo wa usimamizi na uendeshaji wa maeneo hayo, utaratibu wa kubaini na kutangaza eneo kuwa maalum, utaratibu wa kutoa leseni kwenye maeneo hayo, vivutio kwa waanzishaji wa maeneo na wawekezaji rasilimali, uhusiano wa sheria hii na nyinginezo, usuluhisho wa migogoro, makosa ya kuendesha shughuli za biashara bila leseni na Mamlaka ya kutunga taratibu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata pamoja na kuafiki Muswada huu wa Serikali, Kamati ilikuwa na maoni yafuatayo:-

Kwanza, kuanzishwa kwa maeneo maalum ya wawekezaji rasilimali, kunaweza kusababisha kuwepo kwa tofauti za maendeleo na kimaisha hasa ikizingatiwa kuwa eneo moja litakuwa limeendelezwa zaidi dhidi ya maeneo mengine ya kiuchumi. Hivyo ni wajibu wa Serikali kuchukua hatua za makusudi kuhakikisha kuwa tofauti hizi hazijitokezi sana. (*Makofi*)

Pili, kwa kuwa moja ya faida kubwa ya kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji rasilimali ni kupanua ajira na kuongeza wastani wa kipato cha Mtanzania, ni vema Serikali ikatoa kipaumbele na kuwezesha ajira nyingi zishikwe na Watanzania. Hivyo sheria zetu za kazi zifanyiwe marekebisho ili ziendane na wakati huu wa utandawazi hususan tunapoingia katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. La sivyo tutajikuta kazi zote nzuri zinachukuliwa na wenzetu.

Tatu, Muswada huu uliwasilishwa kwenye kamati kwa muda mfupi, hivyo kuinyima Kamati muda wa kutosha. Miswada igawiwe mapema kwa Waheshimiwa Wabunge, ili waweze kutoa michango mizuri wakati wa mijadala. Hii ni pamoja na uendeshaji wa semina kwa wakati muafaka.

Nne, katika kifungu cha 430 cha Muswada Kamati inapendekeza kuwa kuwe na wajumbe wanne badala ya wawili ambao watateuliwa na Mheshimiwa Rais kutoka Jumuiya ya wafanyabiashara ili kuongeza ushiriki wao.

Tano, Kamati inaiagiza Serikali kufanya marekebisho ya haraka kwa kupunguza urasimu katika eneo la upatikanaji wa leseni ili kuepuka kuwasumbua wawekezaji na

wafanyabiashara. Eneo hili bado linaiondolea sifa Tanzania katika uwekezaji kutokana na matatizo na ucheleweshaji wa kupatikana kwa leseni husika.

Sita, Serikali moja ya kipaumbele ambacho inabidi ikishughulikie ni kuboresha eneo la utoaji maamuzi kwa kuepuka maingiliano na kupunguza urasimu ili kuwapunguzia wawekezaji hawa gharama za urasimu, utawala na utendaji kazi wao wa jumla. Tukifanya hivi maeneo haya maalum yatakuwa ni kivutio kikubwa kwa wawekezaji. (*Makofi*)

Saba, Serikali izingatie na kutoa kipaumbele katika uboreshaji wa miundombinu. Kivutio kikubwa cha wawezekaji na wazalishaji.

Nane, Kamati inashauri Serikali kuwa makini katika kuwachuja na kuwapata wawekezaji wote wa ndani na wa nje ili kuepukana na wawekezaji wadanganyifu na matapeli kwa kuwa na miongozo itakayoainisha *style* zote za kuwapata wawekezaji ambao ni *strategic*. (*Makofi*)

Kamati inaishauri Serikali iandae kwa haraka tathmini ya mpango wa *SEZ* zingine ili tufahamu ni sehemu gani katika Mikoa inalengwa kuanzishwa *SEZ* zingine hasa ikizingatiwa kwamba uanzishwaji na mafanikio ya *SEZ* yanasambaza manufaa haya katika nyanja nyingine za maeneo hayo, manufaa ya kiuchumi na kijamii.

Kamati inapendekeza tathmini ya awamu zinazofuata za utekelezaji wa *SEZ* kama ni Tanga, Kigoma, Mtwara, Mbeya, Mwanza, Arusha n.k. ufanywe mapema kwa kuwa utekelezaji wa *SEZ* hutanguliwa na maandalizi makubwa ya miundombinu. Serikali ianze mapema matayarisho kwani wakati hausubiri maamuzi yetu sisi. Yale ya awali yanayoweza kuanza kutekelezwa yaanze kufanyiwa kazi. (*Makofi*)

Kamati inaishauri Serikali pamoja na manufaa makubwa na mapana ya kiuchumi na jamii yanayopatikana na mafanikio ya utekelezaji wa *SEZ* wengine waliojaribu hawajapata mafanikio yaliyotarajiwa kwa kuwa walishindwa kufanya tathimini ya mazingira maalum ya uchumi wa nchi hizo. Kwa hiyo, kamati inaitaka Serikali izingatie mazingira maalum ya Tanzania na ufahamu huo wa mazingira mahususi *element of lo*cal *knowledge*, pia izingatiwe katika utekelezaji wa mpango wa *SEZ* katika awamu zote. *(Makofi*)

Napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa michango yao makini ambayo kwa kiwango kikubwa imesaidia sana kuboresha Muswada uliopo mbele yetu. *(Makofi*)

Mwisho napenda kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Naibu wake Mheshimiwa Salome Mbatia, Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Johnson Mwanyika na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mipango na Uwekezaji, Dr. Enosi Bukuku, pamoja na maafisa wao kwa kuisaidia Kamati kufanikisha kujadili na kuupitisha Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MIPANGO, UCHUMI NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu 43 (5) ( c) Na. 8 (1) za toleo 2004. Kama unavyoelewa kuwa lengo hasa la kuwa na maeneo maalum ya uwezekaji rasilimi ni kujitahidi kuongeza tija kwa taifa wakati huo huo kuongeza ajira kwa nchi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwekezaji yoyote anayetaka kuwekeza katika eneo lolote lile huwa anaangalia vitu vifuatavyo:-

Kwanza, amani na utulivu katika eneo husika.

Pili, soko la bidhaa zake katika eneo nje na ndani. Aidha na uwezo wa wananchi katika kufanya manunuzi *(purchasing power*) ambayo kwa kiasi kikubwa hutegemea na idadi ya watu katika eneo husika na uwezo wao kifedha. *(Makofi)*

Tatu, miundombinu pamoja na gharama za uzalishaji,

Nne, utawala katika Mamlaka zinazotoa vibali mbalimbali kama vile leseni, vibali vya wageni kufanya kazi na kadhalika.

Tano ni vivutio vya kodi ambavyo wengi wanadhani ndiyo muhimu sana kuliko nilivyotangulia kusema yaani utulivu, soko, miundombinu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na idadi kubwa ya watu waliopo Tanzania ni kigezo kizuri kwa wawekezaji kuja kuwekeza kwani atakuwa na uhakika wa soko la ndani kwanza. Ila tatizo ni uwezo wa Watanzania kufanya manunuzi kitu ambacho kinaweza kubadilika kulingana na upatikanaji wa ajira iliyo rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi za India, China, Indonesia n.k. zilifanikiwa katika mpango wa *SEZ* kutokana na kujipanga vizuri kwa kuwapa elimu ya kutosha wananchi wao. Wao walianza kuwajenga kimawazo wananchi wao ili waweze kujiajiriwa kwa wingi zaidi kuliko wageni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuonyesha kuwa Tanzania bado tuko nyuma kwa kulinganisha na majirani zetu wa Kenya na Uganda katika elimu angalia idadi ya wahitimu wa Vyuo Vikuu katika nchi hizo kwa mwaka, ambao ni wanafunzi 50,000 kwa Kenya, wanafunzi 40,000 kwa Uganda na Tanzania ni wanafunzi 15,000 kwa takwimu za mwaka 2004. Hata idadi hiyo nayo ukilinganisha na uwezo wao na majirani zetu ipo tofauti kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kenya ina idadi ya watu wasiopungua 34 milioni, Uganda ina idadi ya watu wasiopungua 27 milioni na Tanzania idadi ya watu wasiopungua 37 milioni kwa takwimu za mwaka 2005.

Kambi ya Upinzani inaona kutokana na Takwimu wanaohitimu Vyuo Vikuu kwa nchi za Afrika Mashariki na kulinganisha na uwiano wa idadi ya watu ni dhahiri kuwa pindi teknolojia mpya itakapoingizwa na wawekezaji katika mpango wa *SEZ* basi Tanzania litakuwa soko zuri la ajira kwa wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hatusemi kuwa iwe ndiyo sababu ya kutoanzisha *SEZ* ila tujue upungufu wetu ili tujiandae vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi ya upinzani siyo kama inakataa au kupingana ila nadhani *SEZ* inaweza iko Tanzania lakini isiwaongezee ajira Watanzania. Kwa maana watakaonufaika na hiyo *SEZ* ni wageni zaidi kuliko wenyeji hivyo, ile dhana ya wawekezaji isifanikiwe vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi ya upinzani inatoa rai kuwa kuna haja kuwa makini kwani lengo la mwekezaji yoyote ni kupata tija wakati yeye suala la ajira hupewa umuhimu mdogo sana. Hili limejitokeza kwa baadhi ya viwanda vilivyomo kwenye *EPZ* kutokujali maslahi Wafanyakazi wao. Hivyo tunashauri kuwa Serikali itoe mwongozo utakaokuwa wazi kwa wawekezaji na waajiri, waajiriwa ili kuepuka unyanyasaji wa waajiriwa pamoja na kuepuka migomo ambayo nayo ikikithiri wawekezaji huondoka na wengine huogopa kuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 9 (1), (2) za Muswada huu kuhusu madhumuni ya uanzishwaji wa maeneo maalum ya uingizaji rasilimali una upungufu kwani kutokana na hali halisi ya kiwango cha elimu cha Watanzania bado ajira itakayopatikana ni ajira muda mfupi tu (ya vibarua) kitu ambacho siyo lengo la mpango huu. Kwa kuwa sehemu kubwa ya ajira katika nyanja za uwekezaji zitahitaji watu waliofikia angalau kidato cha nne.

Kambi ya Upinzani kwa hili inashauri ni bora mpango huu uende sambamba na kuongezeka Bajeti kuhakikisha watoto wetu wanafikia elimu ya sekondari ili mpango huu wa *SEZ* uwe na maana kwa Watanzania isije ikawa ajira ya kudumu zinachukuliwa na wenzetu toka Mataifa jirani na sisi tunaambulia ajira za muda mfupi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 28 ya Muswada huu imezungumzia aina za mashine zitakazotumika katika uzalishaji kuwa hazijawahi kutumika mahali popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kupunguza kazi toka nje ya nchi kwa kisingizio cha kukosa utaalam wa kuendesha mashine hizo za uzalishaji litakuwa ni jambo la hatari sana kwetu. Ni dhahiri kuwa nguvu kazi itakayohitajika italazimika iwe na kiwango kikubwa cha taaluma ili iweze kuendana na teknolojia inayoletwa nchini. Serikali isipowaandaa Watanzania kipengele hiki kitakuwa ni mwanya na sababu nzito za wawekezaji kukitumia ili kuwapatia ajira watu wao na hivyo kurudisha nyuma juhudi za Serikali za kuwapatia ajira Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa kifungu hiki kambi ya upinzani inashauri yafuatayo:-

Serikali ijitahidi katika kuandaa Watanzania ili waweze kuajiriwa katika kazi za kudumu, hivyo ishauriane na asasi za Elimu za juu na Wizara ya Kazi, mapema juu ya mahitaji ya wataalam katika mradi husika.

Pili, Serikali iweke msukumo katika uwekezaji katika sekta ya elimu ya sekondari na ufundi.

Tatu, Serikali iwe na mpango maalum wa kuhakikisha kuwa vijana wetu waliofaulu kuingia kidato cha kwanza wanapata nafasi za kusoma ikibidi hata kuwalipia katika shule za watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, Miundombinu ni moja ya changamoto kubwa katika kuvutia wawekezaji rasilimali kwa maeneo husika. Kwa hivi sasa tatizo kubwa ni gharama kubwa ya umeme na maji, viwanda vyetu vingi vilifungwa kutokana na gharama za vitu hivyo kuwa kubwa mno. Matatizo haya ndiyo yatakayokuwa kisingizio cha Mikoa mingine kama vile Kigoma, Pemba n.k. kukosa wawekezaji.

Kambi ya Upinzani inashauri Serikali kuweka utaratibu ambao unaweza kutamka kama ni *SEZ* bila ya kuwa na eneo maalum la uwekezaji. Kwa mfano, kama mwekezaji ameweka kiwanda cha samaki Kigoma basi ile sehemu ya kiwanda peke yake iweze kutangazwa kuwa ni sehemu ya *SEZ* siyo kungoja eneo ambalo litatamkwa rasmi na Serikali kama lile eneo kubwa au kiwanda kwa mfano cha ku-*process* nyuzi za pamba Mwanza basi apewe fursa vile vile za *SEZ* kama mwekezaji mwingine.

Kwa mfano kama mwekezaji akiweka kiwanda cha samaki Kigoma au Pemba, Makunduchi basi apewe fursa naye kama zile za *SEZ* kwa sababu *EPZ* na *SEZ*, *SEZ* ina fursa nyingi zaidi kuliko *EPZ*. Aidha Serikali imshauri mwekezaji kutumia mali ghafi katika uzalishaji ili kuongeza soko la uzalishaji, maana mwekezaji anaweza kutoa mali ghafi nje wakati mali ghafi ipo hapa nchini kama hamkumwekea utaratibu wa kutumia mali ghafi. Tumejifunza hiyo, katika kiwanda cha bia wakati kiagizia shayiri kutoka *South Africa* wakati shayiri inazalishwa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itasaidia sana kupunguza manung'uniko miongoni mwa Wabunge juu ya maendeleo katika Mikoa yao na Majimbo yao na pia kuongeza ari ya uzalishaji kwa wakulima wetu wanaozalisha bidhaa za viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu mengine yaliyomo kwenye Muswada huu wa sheria ya *SEZ* inaonyesha kuwa Serikali imeshindwa kuona kuwa hapakuwa na umuhimu wa kuendelea wa kuwa na Mamlaka inayoshughulikia uanzishwaji wa viwanda viwanda vinavyozalishwa kwa ajili ya mauzo ya nje *EPZ* kwani majukumu yako yamo ndani ya *SEZ*. Aidha Mamlaka nyingine si ambazo shughuli zake zimo ndani ya *SEZ* ni *TIC*. Hivyo basi msukumo mkubwa unatakiwa uwe kwenye *SEZ* na Mamlaka zilizotajwa ziwe ni Idara ya *SEZ,* yaani *EPZ* na *TIC* sasa ziwe ni Idara tu ya *SEZ* badala ya kuwa na vyombo hivi vitatu mbalimbali. Vinginevyo ni kuongeza gharama bure. Kambi ya

Upinzani inaona tofauti na ushauri huo itakuwa ni Serikali kutumia vibaya fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Waziri atupatie tathmini ya utekelezaji wa *EPZ* iliyokuwa chini ya *NDC* pia atuelezee hivi *EPZ* itakuwa chini ya Waziri na *SEZ* itakuwa chini ya Rais. Je, hatuoni kwamba hii nyingine itakuwa tu ipo kinadharia?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wale wachangiaji mahususi tayari wamemaliza sasa tunafungua mjadala kwa wachangiaji wengine. Maombi yanaruhusiwa kuendelea kuletwa kwa hiyo orodha haijafungwa. Kwa hiyo, mnaweza kuleta. Kwa hiyo, ninaomba nimwite Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah, halafu Mheshimiwa Mporogomyi ajiandae na Mheshimiwa Ngeleja ajiandae.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kupata nafasi ya kwanza kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Kwanza, mimi niunge mkono hoja hii iliyo mbele yetu kwamba ni hoja nzuri kwa manufaa ya nchi yetu na Watanzania kwa ujumla. (*Makofi*)

Hoja zilizoletwa mbele yetu na Mheshimiwa Waziri, ni hoja ambazo zinatekelezeka, hazina matatizo, ila wasiwasi wangu moja ni kwamba hoja kama hizi nzuri na nyingine nyingi ambazo tumezipitisha katika Bunge letu Tukufu, baada ya kuzipitisha tunaziona kwamba zinachukuliwa na kuwekwa katika *shelves* na Idara mbalimbali bila kufanyiwa kazi katika masuala mazima ya utekelezaji wa maamuzi ambayo tunapitisha hapa.

Sasa fursa hii inafanana na hoja mbalimbali ambazo zimeletwa katika Bunge letu Tukufu kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu na kutoa ajira nyingi kwa Watanzania, nyingi bado hazijaleta ufanisi. Sasa naomba na hili lisije likawa linafanana na yale mengine ambayo tayari tumeshayapitisha.

Nitoe mfano wa suala zima la kuingia katika *AGOA* na Tanzania kupata nafasi nzuri ya kuuza bidhaa zetu kwa utaratibu mzuri zaidi na unafuu zaidi ili tuweze kushindana na soko la dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii *SEZ* ina manufaa makubwa zaidi na ni moja ya sheria ambazo kwamba zitatoa fursa kubwa sana kwa wananchi wa ngazi ya chini ya Watanzania kuweza kufaidika kwa njia moja au nyingine ikiwa ni ajira au katika biashara ya moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie eneo la uwekezaji. Katika kutayarisha eneo la uwekezaji kwa maana ya miundombinu, simu barabara maji sana na maji taka naamini kwamba maeneo haya yatatayarishwa na sekta binafsi na siyo Serikali ili kuondoa urasimu na ukiritimba ambao unaweza ukatokea katika kuchelewa azma nzima

ya kuweka haya maeneo ya uwekezaji. Sasa Serikali itoe nafasi kwa sekta binafsi kuandaa maeneo kama haya ili yawe mazuri kwa sababu watu binafsi wana upeo mzuri labda kwa kuona maneno mengine wameyafanyia kazi maeneo kama haya na kuweka utaratibu mzuri ni jinsi gani tunaweza tukafanya kama mfano uliokuwepo sasa hivi Dar es Salaam katika eneo lile la Mheshimiwa Benjamin William Mkapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jingine ni teknolojia mpya ambayo itaingia nchini ambayo Watanzania watapata faida kutumia teknolojia mpya ambazo ziko nje na hazipo katika nchi yetu. Lakini kama walivyotangulia kusema wenzetu wa mwanzo ni kwamba tuna wasiwasi wa Watanzania waliokwenda shule hapa kama tunao wa kutosha wa kuweza kutumia teknolojia hizi mpya kwa hiyo kuna umuhimu, sasa hivi Serikali kutoa maelekezo kwa Wizara ya Elimu ya Juu pamoja na Wizara ya Elimu, ili kuwa na matayarisho maalum kwa ajili ya kuweza kukabili matatizo haya ya *skills* ambazo kwamba tuko wachache na hatimaye kutoa nafasi za wenzetu wa nchi jirani kutumia nafasi hizi zetu.

Kutokana na fikra nzuri ambazo sisi tunazo na Tumeanza kuanzisha na hatimaye wenzetu wakaja juu ya migongo yetu na kutumia fursa hizi na sheria hizi nzuri tulizoziweka na sisi wenyewe tusipate faida ndani yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kutahadharisha jambo lingine masuala ya kodi, *TRA* ndiyo Mamlaka ambayo inasimamia kodi ya nchi hii. Naiomba sana *TRA* izingatie mipaka ya kazi yake isijiingize katika maeneo ambayo hayawahusu, waingilie kati katika mipaka ambayo inawahusu kusimamia na kudhibiti kodi za nchi lakini wasitoe nafasi wakaanza kuwabugudhi wawekezaji katika maeneo ambayo wao hawahusiki na hatimaye kuwakatisha tamaa wawekezaji ambao watakuja kushiriki katika suala zima la *SEZ* hapa Tanzania.

Hili suala zima la ununuzi wa bidhaa ghafi ambazo kama tunazo hapa Tanzania ni vema wawekezaji hawa wakawekewa sheria mahususi kwamba bidhaa ghafi ambazo japokuwa anao uhuru wa yeye kuleta bidhaa popote anapotaka nchini, lakini watoe kipaumbele kwa bidhaa ambazo zipo hapa Tanzania zinunuliwe hapa Tanzania, ziingie katika viwanda vyao na hatimaye itatoa nafasi nzuri kwa wakulima wetu kupata soko nzuri la bidhaa zao ambazo zitaingia katika soko hili *SEZ* na kufanyiwa kazi na hatimaye Serikali kwa njia moja au nyingine itaweza kupata kodi au itapata faida kubwa ya kupata ajira vijana wetu na hatimaye kufaidika katika hili.

Kubwa ninaloliona hapa kwa hivi sasa ni kwamba Tanzania itakuwa na nafasi kubwa zaidi siyo katika kodi lakini ajira ndiyo itachukua nafasi kubwa kwa ndugu zetu vijana wetu wa Tanzania waweze kufaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema hakuna sababu ya Watanzania kwenda Japan au kwenda Dubai kwenda kununua gari, kwenda kununua makatapira kwenda kununua *excavator* wakati hii fursa ya *SEZ* tunaweza na sisi tukawaita watu wenye uwezo na wenye mitaji mikubwa wakafungua masoko kama haya hapa hapa Tanzania na tukiwa ni wa kwanza kuanzisha soko kama hili hapa Tanzania ninaamini ndugu zetu wa

Kenya, Uganda, *Congo DRC,* Zambia, Malawi watakuwa hawana sababu ya kusafiri kwenda mpaka Dubai au nchi nyingine za Mashariki ya mbali na kununua vifaa hivi.

La msingi ni kwamba yule anayekuja kuleta vifaa hivyo viwe hapishani kwa bei kati ya kununua Dubai au na Japan tofauti iwe ni nzuri na ya hatimaye nina uhakika tayari itakuwa imepata faida nyingi katika soko hili, kwa mfano sasa hivi ukinunua gari nje kule hapa nchini kule unatoka kuna kodi ndogo ndogo ambazo hazipungua kwa mfano *inspection* ya magari, kodi mbalimbali za bandari, kodi ndogo ndogo ambazo kwamba wao wenyewe wanaokuja kununua bidhaa hizi wanaziona ni za kawaida lakini sisi tunazipeleka nchi nyingine. Ingekuwa ni vema kodi hizo zikabaki hapa ndani na ni nyingi zinaweza zikasaidia kukua uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia inamrahisishia vile vile yule anayekwenda kununua awe anakuja Tanzania inamchukua muda mfupi.

Sasa la msingi ni jinsi gani Serikali itadhibiti zile bidhaa ambazo hata Mtanzania anaweza kununua pale itabidi alipe kodi za kodi za ndani ya nchi, lakini yule ambaye siyo Mtanzania na anatoa bidhaa zile kupeleka nchi jirani anakokwenda tuwe na utaratibu mzuri wa jinsi gani ya kuona kwamba bidhaa hizo zinatoka nje na hazibaki hapa ndani ili kuikosesha Serikali mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina amini kwamba kama tutakuwa (*aggressive)* tutakuwa tunajituma kwa uhakika na Serikali kusimamia kwa haraka zaidi hili wazo tunaweza tukalitekeleza na maeneo ya kufanyia kazi au maeneo ambayo yanaweza yakawekwa kwa ajili ya sheria hii yako mengi, tuna maeneo ya bandari kama Tanga, Dar es Salaam na Mtwara, haya ni maeneo ya kuvutia uwekezaji wa namna hii na maeneo mengine ya nchi jirani kama kule Kigoma na Mwanza na maeneo ambayo mengine yanaweza yakaainishwa kwamba ni maeneo *potential* kwa ajili ya uwekezaji wa namna hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa niseme naiunga mkono hoja hii na nakubaliana kabisa na wazo kwa hiyo ninachoomba Serikali iharakishe utekelezaji wake ili tusije tukachelewa na hatimaye nchi jirani wakachukua nafasi yetu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimewaomba wanaotaka kuchangia walete maombi yao, tafadhari mtumie zile tunazoombea kwa sababu inakurahisishia unataka kuchangia nini. Sasa kuna miswada miwili katika *order paper* kwa hiyo, tunachokizungumza sasa ni *Special Economic Zone Bill (SEZ)* naomba tuombe hii kwanza msiombe Miswada hii yote miwili tutachanganya hapa. Muswada mwingine mtapata nafasi ya kuchangia.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa na mimi ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika jengo hili naomba nichukue nafasi hii kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Naibu Spika na kwa

kipindi kifupi ambacho tumekuwa hapa kwa kuonyesha uwezo mkubwa wa kuliongoza Bunge hili. (*Makofi*)

Lakini la pili, naomba unifikishie salama zangu kwa Mheshimiwa Spika, kwa kuchaguliwa na Wabunge karibu wote na kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini nampongeza zaidi kwa sababu katika kipindi kifupi alichokaa hapa Bungeni ameonyesha kwamba kweli yeye ni mtu wa *standards and speeds* nampongeza sana. (*Makofi*)

Lakini nachukua nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kwa kura za kimbunga kuwa Rais wa Taifa hili chini ya uongozi mahiri wa Chama cha Mapinduzi ambazo kimeliongoza Taifa hili toka uhuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward N. Lowassa, kwa kuchaguliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu wa nchi hii na kuthibitishwa na Wabunge wote kwa kura nyingi sana. Pia Nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote na manaibu Mawaziri kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete nawapa pongezi nyingi sana. (*Makofi*)

Lakini pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwekezaji kwa kazi nzuri waliyoonyesha katika Muswada huu wa *Special Economic Zone.* Maneno ambayo Mheshimiwa Waziri amekuwa akiyazungumza katika Muswada huu ni maneno mazito sana. *Policy implications* zilizoko katika Muswada huu ni kubwa sana.

Najua mwanzoni tulikuwa tunazungumza humu ndani ya Bunge tunaogelea, tunazungumza maneno mengi ikiwa ni pamoja na kufungua Taifa hili ili liweze kupata maendeleo ya haraka zaidi. Muswada huu unatoa majibu kwa yale yote ambayo tumekuwa tunayazungumza. *(Makofi)*

Nampongeza pia Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa hotuba yake nzuri ambayo inalenga kuonyesha yale ambayo Kamati wanachama wa Kamati ya Fedha na Uchumi waliyaonyesha katika majadiliano. *(Makofi)*

Msimamo wa Kamati ulikuwa wazi na Mheshimiwa Mwenyekiti, aliuzungumza na kuonyesha wazi. Lakini napenda niseme hivi, mwanzoni tulisema tutumie uchumi wa jiografia ya nchi yetu ili tuweze kufungua Taifa hili na tuweze kupata maendeleo ya haraka. Na mimi nafikiri mpaka hivi sasa wote tunakubaliana kwamba kwa kweli maendeleo ya nchi yangekwenda haraka kama tunge-*focus* katika mambo makubwa ambayo ndiyo yangepewa kipaumbele katika kupanga mipango yetu ya Taifa hili. Mwanzoni tulisema Tanga ni bandari nzuri, sasa tujenge reli kutoka Tanga kupitia Moshi kwenda Arusha kupitia Manyara iende mpaka Musoma na hiyo ingesaidia kufanya biashara na nchi za jirani Kenya na Uganda. Na hilo ni jambo jema. Limezungumzwa kwa muda mrefu halisikiki sasa limepoa. *(Makofi)*

Lakini kwenye mpango huu wa *Special Economical Zones* nafikiri ni wakati muafaka sasa wa kwenda nao. Kwa upande wa Kusini, bahari nzuri *infrastructure* imeanza kutengenezwa. Lakini haitoshi kwa sababu bado iko mito mikubwa kama vile Kilombero na sehemu zingine ambako unahitaji siyo kivuko unahitaji daraja la kudumu linaloweza kusukumwa likapita Mahenge likaenda mpaka Songea likaungana na *Mtwara Corridor. (Makofi)*

Haya yote yangeweza kufungua nchi yetu na sisi tungejikuta kwa kweli tunapata maendeleo ya haraka. Kule Mchuchuma tunazungumzia habari ya *resources* zilizoko pale Mchuchuma ya kusaidia kuleta umeme katika Taifa hili. Tulikuwa tunazungumza kwamba wawekezaji wameanza kufikiria hivi tutapita wapi. Hivi tutapelekaje, hivi vitu tutasafirishaje. Makona mengi yametokea kwa sababu *priorities* zetu hazijakaa sawa tumekuwa tunashindwa tuanze wapi na tuende wapi. Lakini Mchuchuma ndiyo njia pekee itakayotuokoa nchi hii. Maana inabidi tufike mahali tuondokane na matumizi haya ya *hydropower* na tunaona jinsi tunavyoteseka na hii *hydropower.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulizungumza juu ya Mkoa wa Kigoma. Mkoa wa Kigoma ndiyo *growth path* ya nchi hii. Kama mkoa ule ungeweza kuendelezwa na mipango kwa kweli ikafanywa kama inavyotakiwa ifanywe. Lakini Mkoa wa Kigoma huipitiki na barabara hakuna. Sasa tunaishukuru Serikali kwa sababu inaonyesha nia kubwa ya kujenga barabara za Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Barabara ya kutoka Tabora kwenda Kigoma tumeambiwa itajengwa na katika mpango huu ili mpango huu au mipango hii ifanikiwe, barabara ya Tabora kwenda Kigoma ijengwe, barabara ya kutoka Tunduma kwenda Sumbawanga, Mpanda, Uvinza, Kigoma ijengwe na barabara ya kutoka Nyakanazi inayoungana na barabara ya Kagoma-Rusahunga kuja mpaka Kibondo-Kasulu-Kigoma zikijengwa hizo zitaunganisha Mikoa yote mitatu hiyo niliyoitaja na kutakuwepo na biashara kubwa na wakulima wa Mkoa ule wa Kigoma watalima kwa kasi mpya, nguvu mpya na ari mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mazao mengi katika Mkoa wa Kigoma ambayo hayauzwi sehemu nyingine yoyote kwa sababu ya ukosefu wa usafiri. Ndizi ziko nyingi, maharage yako mengi, mahindi yako mengi, mihogo iko mingi na Mkoa wa Kigoma unaweza kuzalisha *palm oil* za kulisha nchi hii na tusihitaji *import* ya aina yoyote katika Taifa hili. *(Makofi)*

Leo Taifa hili linapoteza fedha nyingi eti tunaleta malighafi katika Taifa hili ya mafuta ya mawese. Nimekwishazungumza katika Bunge lako, naomba nirudie hakuna malighafi ya mafuta ya mawese yanayotoka Malaysia, wala Singapore, wala Hongkong. Malaysia ndiyo nchi peke yake inayozalisha mafuta kwa wingi. Lakini Malaysia kwa Sheria zilizopo Malaysia haipeleki nchi ambayo hawana *Joint Venture* hawapeleki. Wanapeleka Hongkong kwa sababu wana *branch* yao kule na wale wanafanya kitu kama *Concoction* ya mafuta yale na yale mafuta ndiyo yanachukuliwa yanaletwa hapa kama malighafi lakini yale mafuta ni *98% refined* ndiyo yanaletwa hapa yanasemekana ni malighafi. Hakuna malighafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha azma mzima ya *Special Economic Zones* yako mambo tunayoyahitaji. Elimu ni msingi sana kwa Taifa hili. Kitu cha msingi sana, je leo tunazungumzia habari ya kwenda kwa *Standards* zinazotupeleka kwenye sayansi na teknolojia lakini kusema kweli hakuna mpango mahsusi ambao unaonyesha jinsi ambavyo tuna-t*ransform* hii hali tuliyonayo tunayoilalamikia kila ya elimu ili kuiweka katika hali ambayo Watanzania wengi watakuwa wameingizwa katika mfumo wa sayansi na teknolojia. *(Makofi)*

Mpango huu wa elimu mahsusi ndiyo uliowafanikisha wenzetu ambao Mheshimiwa Waziri ameuzungumza hapa kwenye Muswada kwamba walipiga hatua kubwa kwa sababu walitumia *labour force, educated labour force* kama kiungo muhimu cha ku-*transform* uchumi wa nchi zao, na mimi nafikiri Tanzania inawezekana kama tukikaa si kwa mpango wa pengine hii haiwezekani, pengine hii inawezekana. Lakini mimi nina imani kwa jinsi Mheshimiwa Waziri alivyosoma Muswada huu, Muswada huu unawezekana kama wote tukikubali kwamba *we can do* siyo *we can't do. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma pale kunahitajika *Port* ambayo Benki ya Dunia ilipofanya utafiti kwenye *Port* ya Kigoma ilisema kama ile *Port* peke yake ingefanyiwa *rehabilitation* ikatengenezwa vizuri tungeuza na tungesafirisha watu kwenda Burundi, kwenda Rwanda, kwenda *Congo* na kwenda Zambia na bidhaazetu zingekwenda huko, dagaa zingekwenda huko, migebuka ikwenda huko na hata maharage haya tunayosema yangekwenda huko na viwanda vingekuwepo vya samaki, vya dagaa na vya maharage. Benki ya Dunia walisema Kigoma *produces the best beans in the whole of Africa*. Lakini: "*we need to produce a minimum of 50,000 tons of beans".*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tungeweza hivyo na nina imani kwenye mpango huu tunaweza. Tukazalisha kiwango kikubwa na wakulima wetu wanao uwezo, maana ni wachapa kazi wakubwa sana. Tukifika hapo nchi itakwenda. *Airport* ya Kigoma ikifanywa *International Airport* ndege kubwa zitakuja kutoka *Congo Brazaville,* kutoka *Congo,* kutoka Burundi, kutoka Zambia zitakuja kuchukua bidhaa Kigoma na kwa kutumia kilimo cha Kigoma peke yake bado chakula kingine kinaweza kuletwa ndani ya nchi na kikaweza kusaidia mikoa mingine ambayo ina upungufu wa chakula. *(Makofi)*

Kwa taarifa Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma ndiyo Mkoa peke yake katika nchi hii ambao haujawahi kuomba msaada wa chakula. *(Makofi)*

Na hao wakulima wa Mkoa ule wanastahili wapewe tuzo na Serikali maana kazi wanayoifanya kwa Mkoa ule ni kubwa pamoja na kwamba wanakaribisha Wakimbizi wengi katika Taifa hili. *(Makofi)*

Maana lazima tuwakaribishe, tumewakaribisha kwa njia maalum ya peke yake, wakija sisi tumesema hatuwafukuzi tumewakaribisha tumewaweka pale. Lakini wakija wanapofika hamuelewi adha tunayopata. Tunawalisha katika vijiji vyetu, kisha ndipo wanakwenda kwenye Makambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni nzuri sana na mimi naunga hoja mkono mia kwa mia utekelezwe haraka na mbinu za kufanya Muswada huu utekelezwe nchi nzima zifanywe kwa kweli kwa nguvu zetu zote na Serikali iweke uwezo wake wote katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na nawapongeza sana walioleta Muswada huu ndani ya Bunge hili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngeleja, nimekuweka kwa ajili ya Muswada ule mwingine. Uliandika *EPZ.*

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Hapana.

**NAIBU SPIKA:** *Okay* nimekuelewa. Nimwite Mheshimiwa Cheyo basi wewe baadaye.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nataka kutumia nafasi hii tena kusisitiza kwamba kwa kuwa tuna njaa zaidi sehemu ile ya kwetu ya Kanda ya Ziwa na zaidi Bariadi basi Serikali iongeze tena msaada wake wa chakula na pia chakula hiki kamwe kisitumike kwa njia nyingine yoyote wala kisigawiwe kwa kufuata upendeleo wa kisiasa au kwa njia nyingine yoyote kwa sababu wanaogharamia ni Watanzania wote na wale ambao wamejaribu kuweka mkono wao kuiba pale kama ulivyofanya Nhobola juzi basi nawaomba wananchi wao wenyewe wajichukulie ndiyo waangalizi wakubwa wa chakula hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kujielekeza kwenye Muswada uliyo mbele yetu. Kwanza mimi napata tatizo juu ya taswira nzima ya Muswada huu. Inaonekana kwamba sasa hivi tumeiga tu kutoka nchi zingine kama vile zilivyotajwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Pametokea na msisitizo zaidi kuangalia sehemu kama vile sehemu itachaguliwa kama vile ilivyochaguliwa Mabibo na kuweka kila kinachohitajika pale kama miundombinu pamoja na kuhamasisha wafanyabiashara waingie katika sehemu hiyo. Wazungu wanasema *processing* au kuweza kuweka viwanda ambavyo vitaweza kutoa zaidi mali ambayo inakwenda nje.

Mimi naona hii taswira ni finyu mno, zaidi taswira yenyewe ingepashwa tuangalie sekta fulani na sekta hii ambayo mimi naona tungejielekeza zaidi ni sekta ya wale walio wengi kama nia yetu ni kupunguza umaskini kufuatana na mpango wa MKUKUTA basi asilimia 80 ya nchi yetu ni wakulima. Asilimia 80 ya watu walio maskini ni wale ambao wanategemea kilimo. Kwa hiyo, tutakuwa na mtazamo wa kisekta tukaiangalia sekta ya kilimo ni mazao yapi tuyatamke wazi kwamba mazao haya ni *Special Economical Zone,* kama tukifanya hivyo basi nguvu zetu zote zielekezwe katika kuhakikisha kwamba sehemu au mazao hayo yanasaidiwa kwa kila njia kuhakikisha kwamba kama kuna vivutio vya aina yoyote vinaelekezwa upande huo.

Nataka kutoa mifano, kwa mfano, tunaweza tukajielekeza kwa pamba, tunaweza kujielekeza kwa korosho, tunawezesha kujielekeza kwa kahawa.  Tunaweza kujielekeza kwa tumbaku.  Pia tusisahau mahindi pamoja na mchele kwa sababu inavyoonekana kama tukilima mchele mwingi watu walio karibu na sisi kama Kahama kule wanaupenda sana mchele wa Tanzania.  Sasa kama tukichukua mfano kama wa pamba, sasa hivi, jana nilikuwa namsikiliza Waziri wa Kilimo, nilisikitika kuona kwamba inaonekana kama vile Serikali imekata tamaa kabisa juu ya kutafuta mbinu mbalimbali za kuweza kuwawezesha wakulima wa pamba, wakulima wa kahawa, wapate tija na pia wapate bei ambayo inastahili.  Katika majumuisho ya jana kwa mfano kulikuwa na maneno mawili tu ya Waziri wa Kilimo na Chakula juu ya pamba na juu ya mazao ambayo yametupa fedha kwa muda mrefu.  Kwa hiyo, mimi nasema kwamba tukijielekeza kwa sehemu hiyo, tunapozungumzia hao watu watakuja kusindika, watasindika nini kama hakuna mazao ya kutosha kutoka kwa wakulima.  Tunaposema kwamba tuwape vivutio vya kodi ndiyo kusema tunainyima Serikali mapato ya kodi.

Lakini kama haiwasaidii watu walio wengi ina faida gani ni wageni tu ndiyo watakaochukua faida hii na kuchukua hizo fedha na kwenda nyumbani.  Sisi tunaachiwa umaskini wa kudumu.  Kwa hiyo, mapendekezo ambayo nayatoa ni kama yafuatavyo:-

Kwanza, kama tukikubaliana kwamba tuangalie hili jambo kwa kisekta kwamba tusaidie sekta ya kilimo, tusaidie watu ambao wanatengeneza kwa mfano wanaolima *oil seeds* ndiyo kusema basi tumnyanyue mkulima wa pamba kwa mfano aonwe kama mwekezaji katika sekta hii ambayo inatusaidia kupata fedha za kigeni na iangaliwe yumo katika *Special Economical Zone* basi kama akionwa namna hiyo basi Serikali ielekeze nguvu zake kule.  Kwa mfano, kutoa ruzuku ya bei. Mkulima akihakikishiwa kwamba akilima pamba atapata bei hii mtashangaa kwamba nchi hii na Mungu tubariki kwamba tuweze kupata mvua, wakulima watawapatia zaidi ya marobota milioni 2 katika mwaka mmoja bila kuwa na matatizo.  Tatizo la sasa mkulima hana uhakika analima pamba yake hajui atapewa bei kiasi gani na hiyo bei atakayopewa itakuwa na makato kiasi gani. Kwa hiyo, ni bahati nasibu tu.  Unaingia kwenye biashara ambayo hujui mvua itakuja, hujui bei itakuwa sawa sawa.  Kwa hiyo, sasa hivi kama kuna sekta ambayo mimi naona inahamasisha umaskini ni sekta ya kilimo, kwamba tunakuwa na wakulima ambao ndiyo wao wanafidia sekta nzima.

Kwa mfano, mkulima kwa sasa hivi wa pamba gharama yake ya kulima pamba ni kama shilingi 200 kwa kilo moja ya pamba.  Na katika sehemu zingine ni zaidi ya 250 kwa hiyo anapopewa bei ya sh.150 ndiyo kusema kwamba mkulima huyo anatoa ruzuku kwa *industry* nzima au kwa sekta nzima ya sh.50 kwa kilo moja na sehemu zingine inafika mpaka shilingi 100 kwa kilo moja.

Kwa hiyo, kama Serikali ikiamua leo kuiangalia sekta hii ya kilimo na zaidi kama pamba kama *Special Economica Zone* na ikasema tunaweka tutahakikisha mkulima utapata bei hii, lima na tatizo la soko la pamba, sio matatizo kama tukilima pamba watu wanahitaji hiyo pamba wako wengi tu.  Kwa hiyo, mimi naona tutanue fikra zaidi namna tunavyofikiria hii *Special Economic Zone* na tumwingize zaidi mkulima na pia katika sehemu ile wanayolima pamba, korosho na sehemu zingine tukitamka kwamba hizi ni *Special Economic Zone* ndiyo kusema barabara za vijijini pia kama vile itakuwa ni

miundombinu inayohitajika kuhakikisha kwamba gharama ya kusafirisha haya mazao inapungua na kama gharama ya kusafirisha haya mazao yamepungua ndiyo kusema mkulima atapata bei iliyo mzuri zaidi.

Mimi nina mfano halisi kutoa pamba kutoka Ngwamale kuipeleka kwenye jineri Luguru Wazungu wanasema *is a night mare* maana yake hakuna barabara, ni mashimo tupu. Kwa hiyo, tukifanya hivyo tutakuwa basi tunainua kipato cha mkulima ambaye tunamzungumzia katika MKUKUTA ambao unatangazwa kila wakati na Serikali. Halafu tukiachia kuangalia hiyo habari ya wakulima kama sekta pia ningependa kujielekeza kwa upande wa utalii, sehemu hiyo ya Kanda ya Magharibi.

Sehemu ya Magharibi yaani *Western Serengeti* imesahauliwa sana. Kila tunapozungumzia juu utalii, watu wanazungumzia juu *Kilimanjaro Airport,* watu wanazungumzia *Dar es Salaam Airport* na vitu kama hivyo. Mimi nina hakika kama tukiweka nguvu ya kutosha kwa kuweza kuhamasisha watu wengi waweze wakawekeza katika utalii sehemu ya *Western Serengeti* itaweza kuleta ajira kwa watu wengi na pia tutapata angalau sehemu hiyo faida ya kupakana na wanyama waliopo Serengeti.

Kwa leo kwa mfano ukifika Mwanza ukiangalia *Airport* yenyewe tu inakatisha tamaa. Tuna dhahabu, tuna pamba, tuna samaki na tuna watu kibao, lakini *airport* ya Mwanza haifanani hata kidogo na utajiri ambao uko karibu na *Airport* hiyo mimi nashangaa ukiingia mahali kama Kigali kuna *airport* safi ni nini ambacho watu wa Kigali wanatuzidi, watu ambao tunatoka Kanda hiyo ya *Western Serengeti.*

Kwa hiyo, ningeweza kuhimiza Serikali katika maeneo ambayo naomba waangalie ni pmoja na kuhakikisha kwamba wanajenga vizuri *Airport* ya Mwanza siyo hivyo tu tunahitaji pia kuhamasisha watu waweze kujenga mahoteli makubwa sehemu ya Mwanza na njia mojawapo ni tui-*declare* hiyo *area Special Economical Zone* ili mtu anayeweka pale hoteli yake asiwe anabughudhiwa na shughuli yoyote ile ya kodi. Leo hii ukipata watu 250 watalii Mwanza sijui utawaweka wapi. Ni sehemu ambayo imesahauliwa kabisa lakini ina uwezekano kabisa wa watu wengi kwenda Mwanza. Kuna Ziwa Victoria laweza kuonwa, kuna Serengeti ya kuweza kuangaliwa. Kuna Utamaduni wa aina mbalimbali pamoja na ngoma za Wasukuma ambazo haziwezi zikapatikana mahali popote ulimwenguni za kuweza kuangaliwa. Kwa hiyo, ni sehemu ambayo ikitajwa kwamba ni *special economic area rather than a special economic zone* mimi nina hakika kwamba itaweza kusaidia sana katika kumaliza umaskini katika sehemu hiyo ya Kanda ya Ziwa.

Kwa kumalizia nataka kuzungumzia pia sekta ya samaki. Watu wote wale ambao wako katika *processing* ya samaki sasa hivi kuna kodi kibao. Hili pia lingepashwa kuangalia ili watu wote ambao wamo katika *issue* za ku-*process* samaki waweze wakapata unafuu ambao baadaye unaweza ukasaidia katika kutoa bei mzuri zaidi kwa wavuvi mbalimbali ambao wanategemea maisha kwa uvuvi wanaweza kupata fedha zaidi kwa wakati huu ambao ni wa njaa.

Baada ya kusema hayo, nataka kumpongeza Waziri kwamba mtazamo wa *Special Economic Zone* ni mzuri lakini taswira yenyewe ipanuliwe zaidi kuliko kufikiria maeneo tu. Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutakuwa tunajifunza neno moja kila wakati. Tumeingia kwenye Miswada, sasa tutazungumzia habari ya Miswada. Habari zingine za huko huko siyo sehemu ya Muswada. Kwa hiyo, msimlazimishe Spika kukuambia rudi kwenye Muswada. Kwa hiyo, naomba mlizingatie hilo. Mnaweza kupongeza, mnaweza kushukuru lakini isiwe habari zingine. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Nakushukuru Naibu Spika, kunipatia nafasi hii kuweza kutoa mchango wangu kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na wenzangu kumpongeza sana Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa taarifa yake ambayo ni nzuri sana na kimsingi inatupa mwelekeo mzuri kwa maslahi ya nchi yetu. Lakini pia nampongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, kwa taarifa ambayo ameitoa.

Nami naanza kwa kusema kwamba naunga hoja mkono na kwa kweli taarifa ya mtoa hoja Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa, Waziri pamoja Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi imejibu kwa kiasi kikubwa duku duku ambazo nilikuwa nazo. Lakini pia pamoja na hayo kuna machache ambayo naomba nichangie katika hili.

La kwanza, ni kuhusu misamaha au unafuu ambao wawekezaji watapewa katika Sheria ambayo itatokana na Muswada huu. Kwa jinsi ambavyo naona Watanzania naomba tutoe changamoto kwa Serikali kuwa makini zaidi ya jinsi ilivyo kwa sababu sisi Watanzania pamoja na uzoefu ambao tumeelezwa na Waziri mtoa hoja pamoja na Mwenyekiti lakini Tanzania tuna historia tofauti kidogo. Nakumbuka suala la misahama kwa mfano kodi kwa wawekezaji ilikuwepo miaka ya 1990 lakini kama sikosei mwaka 1997 iliondolewa. Na kipindi kile kwa mfano, misahama ya kodi iliyokuwepo ilikuwa ya miaka mitano. Sasa tunakuja na misamaki ya miaka 10 pengine inaweza kuwa zaidi baadaye na kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili nilikuwa naomba niishauri Serikali tujifunze kutokana na makosa ambayo yalifanyika yakatupelekea ile misamaha ambayo ilikuwa inatolewa miaka ya 90 ikaondolewa, mwaka 1997. Nadhani hili ni la msingi sana katika mazingira yetu ya Tanzania. Kwa sababu pamoja na uzoefu ambao tumeupata kutoka kwenye nchi mbalimbali ambazo taarifa zimeonyesha kwa mfano nchi za Kusini Mashariki mwa Asia, Kenya na nchi zingine. Lakini bado sisi Tanzania tuna historia ambayo inatuonyesha kwamba tulishajaribu utaratibu huu lakini kwa kweli ulitupa matatizo kwa kiwango fulani ambacho kilipelekea tukafuta utaratibu huu. Sasa hii ni changamoto kwa Serikali. Na mimi nilikuwa naiomba Serikali tuwe makini zaidi kuhusu misamaha hii isije ikatufikisha mahala ambapo tukashindwa kui-manage kama ilivyotokea miaka ya nyuma na baadaye tukabadilisha utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilikuwa naomba niongelee suala la kuuzwa kwa mradi ambao utakuwa katika maeneo haya ya *Special Economic Zone.* Nilikuwa napitia Muswada huu hauko wazi sana endapo itatokea mmiliki wa mradi fulani ambao upo kwenye maeneo haya ataamua kuuza mradi huo ndani ya kipindi ambacho yeye anapata unafuu wa mambo mengine ikiwemo kodi. Sasa nashindwa kuelewa kwa sababu katika hali ya kawaida kama jambo hili halitakuwa wazi, linaweza kutuletea matatizo mbele ya safari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwekezaji anaweza kuja hapa akawekeza vizuri kabisa, akapata unafuu ambao sisi tunaona kama ni vivutio. Lakini aka-*breack even* hapo katikati ndani ya kipindi ambacho yeye anafaidika na unafuu huu, akaanza kupata faida. Lakini wakati unaelekea kwisha wakati wake wa unafuu ambao anaupata kutokana na vivutio hivi, basi anaamua kuuza huu mradi. Anauza kwa mtu mwingine au mwekezaji mwingine. Sasa hapa Sheria haiko wazi sana endapo atakuwa ameuza mradi huo.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliangalie hili ili kuwe na uwazi kwa sababu kama itachukuliwa kama ilivyokuwa zamani kwamba anapouza mradi wake unafuu ule hauendelei maana yake ni kwamba yule anayekuja basi naye ataanza upya. Na ataomba apatiwe unafuu kwa kiwango kile kile ambacho Sheria inaonyesha. Kwa hiyo, hili mbele ya safari linaweza likatuletea matatizo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi nilikuwa naomba Serikali ilione na ilifafanue kwa uzuri ili tujihami na yale ambayo yalisha wahi kutupata miaka ya 1990.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kuchangia katika hili ni suala la kilimo. Ni kweli kwamba nchi yetu sisi zaidi ya asilimia 80 ni watu wanaokaa nje ya mjini, vijijini na hawa pia ni wakulima ambao uhai wao wote unategemea shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba pamoja na kwamba Muswada unaonyesha kuna baadhi ya mazao ambayo Serikali inayaona na inayapa niseme labda kipaumbele zaidi, au inaita mazao maalum. Nilikuwa naomba pia baadhi ya mazao yawemo katika hili ikiwemo pamba. Kwa maana ya kwamba zao la pamba likitambuliwa kama zao maalum na likapewa mkakati wa nguvu kwa hii *approach* ambayo tunachukua kwa sasa, litatusaidia sana kuendeleza viwanda vyetu vya hapa nchini. Lakini pia itatusaidia sana kufaidika na mauzo ambayo tutaanzia hapa ndani lakini tutakwenda nchi za Afrika ya Mashariki na baadaye tutakwenda nje.

Sasa hii faida yake ni kubwa kwa sababu tuna viwanda lakini vingi vimekuwa vikiagiza malighafi kutoka nje ya nchi. Lakini endapo tumeweka msukumo wa pamoja uwekezaji ukatambulika kama zao maalum katika hili zao la pamba na mazao mengine yanayofanana na hili, faida yake ni kubwa kuliko ilivyo sasa.

Kwa hivi, Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba hili litazamwe hivyo na ninaamini kwamba litatusaidia sana katika kukuza pato la uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Narudia kusema tena kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia zote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nitoe mchango wangu katika hoja iliyoko mbele yetu na kabla sijafanya hivyo naomba nichukue nafasi hii kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili kwa cheo hicho ulichonacho cha Unaibu Spika kazi ambayo tunaona umeimudu kwa nguvu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Spika, Mheshimiwa Samuel Sitta, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi na Waheshimiwa Wabunge katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana na Waheshimiwa wapiga kura wetu, wanachama wa CCM na wasio wanachama wa CCM, amepita kwa kishindo, tunampongeza sana. Pia tunazidi kumpongeza kwa sababu ameanza kazi yake vizuri kwa kushughulikia janga la ukame na njaa iliyoko Tanzania, tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu na kupitishwa na Waheshimiwa Wabunge kwa kura karibu asilimia mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa zao na tunawatakia kila la kheri. Niwapongeze pia Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao tumepita kwenye tanuru la uchaguzi wa kushinda na kuwa katika Bunge hili na mwisho niwashukuru wananchi wangu wa Arumeru walionipitisha kwa mara ya tatu kuwa Mbunge wao na ninaahidi kwamba nitajitahidi kuwatumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudi kwenye hoja iliyopo mbele yetu, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Naibu wake Mheshimiwa Salome Mbatia, Makatibu Wakuu na Watendaji Wakuu kwa kutayarisha, kuandaa na kuleta Muswada huu wa kutenga kisheria maeneo maalum ya uwekezaji katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nionavyo mimi maeneo haya yatatuharakishia ukuuaji wa uchumi wetu, uzalishaji wa bidhaa bora ambazo zitamudu ushindani katika soko la Kimataifa na kwa hiyo na sisi sasa tutakuwa wadau wa soko la Kimataifa kwa bidhaa zetu na uzalishaji huu utatuongezea fedha za kigeni kwa mauzo ya nchi za nje na uzalishaji huu utakuwa na ubora ambao utatuwezesha kutoagiza bidhaa nyingine ambazo hazina ushindani bora katika nchi yetu, hivyo ku-*save* katika uagizaji wa bidhaa zisizo za lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba licha ya mafanikio makubwa ya kiuchumi na kijamii ambayo yamepatikana katika Awamu ya Tatu, bado tuna changamoto kubwa kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri ya kufikia na kufanikisha malengo ya dira ya maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025 kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri. Baadhi ya malengo hayo ni pamoja na kuendeleza ukuaji wa uchumi kwa viwango vinavyoridhisha kila mwaka, kuongeza mauzo nchi za nje, kuongeza uzalishaji na kuboresha na uzalishaji wa bidhaa zetu hapa nchini na kuibua ajira mpya pamoja na kuimarisha biashara ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu haya ni makubwa na mazito na ni muhimu kwa nchi yetu. Hivyo tunaishauri Serikali kama ilivyofanya sasa kuchukua kila hatua ya kuteka kila fursa ya uwekezaji ambayo itaonekana au itakuja hapa nchini na kuitumia kwa haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishauri Serikali iandae mbinu mbalimbali, mikakati mbalimbali ya kufanya na kuleta mipango kama hii iliyoleta sasa katika nchi yetu ili tuweze kufanikisha malengo ya dira ya maendeleo ya Taifa kama tulivyopanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alipokuwa anatoa mada yake alitupa uzoefu wa nchi mbalimbali za Asia Kusini ambazo zimetumia mpango huu wa kutenga maeneo maalum ya uwekezaji wa fedha au uwekezaji wa mitaji katika nchi hizo na zimekuwa na mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mafanikio ambayo tuliambiwa ni kwamba nchi hizi zimeweza kukuza uchumi wao kwa asilimia au kwa viwango vya kuridhisha mwaka hadi mwaka. Lakini hii imeletwa au imetokana na vivutio walivyotoa kwa wawekezaji wa ndani na nje ambao wamekuja kuwekeza katika nchi hizo pamoja na usimamizi bora, pamoja na *political commitment* ya uongozi wa nchi zilizotajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba kwa kweli tusipotoa vivutio hivi ambavyo vimeainishwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, tusipokuwa na usimamizi makini katika maeneo haya ya uwekezaji, usimamizi unaoaminika, usimamizi usio na utata na utawala bora, hakika hatutapata wawekezaji ambao watakuja kuwekeza katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba tusiogope kutoa misamaha ya kodi, kwanza tumeshaanza kutoa misamaha ya namna hiyo katika uanzishaji wa maeneo maalum kama hili la Benjamin William Mkapa, tumetoa katika sehemu mbalimbali za uwekezaji katika sheria mbalimbali. Tusiogope hili kwa sababu umaskini wetu sasa unakithiri mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba tusiogope kupoteza kile ambacho hatuna mkononi maana yake hakijapotea, tukisema tuna fursa ya maendeleo tuna hiki, tuna kile, tuna kile lakini tunazidi kuwa maskini siku hadi siku, hatutafika.

Mimi naomba niwaambie wenzangu kwamba tukubaliane na vivutio hivyo ambavyo vimependekezwa katika Muswada huu bila kuogopa kwamba tunapoteza chochote. Sasa hivi kama tunataka kuendelea lazima tuwe na mitaji, mitaji hatuna lazima tutafute mitaji kutoka kwenye sekta binafsi na sekta binafsi ndio hiyo inataka vivutio. La pili tunahitaji teknolojia ya kisasa, hatuwezi kuwa na teknolojia yetu binafsi ni mpaka hawa wanaokuja kuwekeza waje na teknolojia hiyo ili na sisi tuweze kufaidi teknolojia hiyo ya kisasa kwa wakati huu ambao tunauhitaji na tuendelee kuwaendeleza wananchi wetu kwa kuwafundisha na kuwapa elimu bora na kuwafundisha katika misingi ya teknolojia ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirejee eneo maalum la Benjamin William Mkapa ambayo Mheshimiwa Waziri ametaja kwamba eneo hili likimalizika tutapata ajira rasmi ya 20,000 na si ajabu tukafika kwenye ajira isiyo rasmi ya 50,000 ajira hiyo yenyewe Waheshimiwa Wabunge wenzangu itatuwezesha kupata mapato kutokana na kodi za mapato ambazo zitatozwa kwa wananchi wetu. Hii ni hatua kubwa sana kama katika eneo moja tu tunaweza kupata ajira 50,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa sana kwamba katika Muswada huu Mheshimiwa Waziri amebainisha sehemu ambazo zinaweza kuguswa na kuanzishwa kwa *Special Economic Zones* na imegusa karibu sekta zote mbalimbali muhimu na katika mikoa mbalimbali. Ningeomba kwamba wakati wa utekelezaji basi tujaribu kuzingatia usambazaji huu, uwiano huu wa mikoa ili kila mkoa uweze kufaidi matunda ambayo yatatokana na *Special Economic Zones* hasa lile la ajira, hasa kuimarisha uzalishaji wa soko la ndani ili kuimarisha biashara ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, niipongeze Serikali kwa kuwa katika kuandaa Muswada huu wamewashirikisha magwiji wa Japan, *Japan International Development Institute* kwenye kuandaa Muswada huu, hawa ni magwiji wa biashara kama tunavyojua wote na kwa kweli imeipa *paper* hii *credibility* kubwa sana kwamba tumewashirikisha hawa ambao licha ya kuwa magwiji wa biashara, pia kwenye nchi yao wali-*adopt* mpango huu wa *Special Economic Zones*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashauri kwamba kama mpango huu utasimamiwa vizuri ajira hizo ambazo tunatarajia kupata za 50,000 kwenye kila eneo la uwekezaji ni hatua kubwa sana katika kuondoa kero kubwa ya vijana wetu wasio na kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misingi hiyo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi ili niungane na wenzangu katika kuchangia Muswada ulioko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba leo nichukue nafasi rasmi, kwani viongozi wengine wote nilishawapongeza katika kuchangia hotuba ya Rais, lakini wewe binafsi Naibu Spika wetu nilikupongeza kwa mkono tu leo naomba nizungumze.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 19 Julai, 2005 wakati nawasilisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha tukihitimisha kumaliza miaka mitano ya Ubunge, niliwaomba sana wananchi wa Njombe Kusini wakuchague kwa kura nyingi, tulikuwa bado tunakuhitaji. Wananchi wa Jimbo la Njombe Kusini walinisikia na kweli wameweza kutimiza ahadi ya ombi langu na leo ninasema ahsanteni sana ndugu zangu wa Njombe Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wanawake tuliomo ndani ya Bunge hili tunakuenzi na tunaendelea kukuenzi mama yetu hatimaye matokeo ya kura nyingi za Njombe Kusini ulivyopata umepata Unaibu Spika na hatimaye tena sisi Wabunge wanawake ndani ya Bunge hili tumekuchagua uwe Mwenyekiti wetu tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa zote hizi ambazo sisi Wabunge wenzio wanawake ndani ya Bunge hili wakiungana na Wabunge wanaume kwa kukuchagua kuwa Naibu Spika tunakuombea maisha mema na Mwenyezi Mungu atakusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niingie kwenye Muswada wetu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji katika kuuleta Muswada huu, huu ndio wakati wake na ndio kweli tunakubaliana kwamba ni ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya maana Serikali hii ya awamu ya nne imeonyesha maendeleo ambayo sasa katika kuubariki huu MKUKUTA wanaonyesha jinsi gani Watanzania tutashirikishwa namna gani katika kukuza uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unaelekeza kukuza uchumi kwa kuwahusisha Watanzania wote, wengine katika kuchangia wanasema haijaleta ajira. Lakini katika Kamati yetu ya Fedha na Uchumi nikiwa mjumbe mmojawapo tumeonyeshwa majengo tayari yameshaanza kujengwa. Kwa hiyo, pale ajira ya wale vibarua wanaotumikia katika kujenga pale ajira tayari imeshaanza, kwa hiyo, nina uhakika ajira itazidi kuongezeka na tayari imeshaonyesha njia halisi kwamba katika kuendeleza hii ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya majengo tayari yameshaanza kujengwa na kasi yenyewe imeonyesha kwamba sasa Wizara hii inatupa matumaini makubwa sana kwamba tutafanikiwa kule tunakoelekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii naipongeza sana katika kuonyesha kwamba ili kumuenzi, kwa sababu tulishampongeza Rais wetu alishasema hapa ndani ya Bunge letu kwamba ataendeleza yale yote yaliyoandaliwa katika Awamu ya Tatu. Ninafarijika sana nikielezwa katika taarifa niliyopewa na Waziri katika Kamati yetu hata maeneo ya Mabibo yametajwa jina la Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, ili awe na kumbukumbu kubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuenzi mambo makuu kama haya basi tutaomba tena na viongozi wenzetu wanaokuja waige maendeleo ya kumuenzi anayetoka na anayeingia ili aendeleze yote ambayo yameandaliwa.

Nomba nichangie Muswada huu, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 10 ametueleza kabisa kwamba waatalamu na wote ambao waliohusika katika kuandaa mkakati huu wa kuleta Muswada huu walitembelea maeneo. Kwa sababu Muswada wenyewe ni mzuri ninaomba tusiuharibu sana, wameanzia Dar es Salaam, *EPZ* imekuwa Dar es Salaam na hii sasa iko Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe katika kuendeleza kuhakikisha kwamba Watanzania wote tunashirikishwa katika uwezeshwaji katika kukuza uchumi wetu waelekee basi watakapomaliza majengo ya hapo Ubungo, Dar es Salaam waelekeze katika maeneo mengine kama Mwanza, wakitoka pale tuelekee Dodoma Makao Makuu ili iendane sambamba na maamuzi tuliyotoa jana katika Muswada wa mazishi ya viongozi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuwa na wasiwasi katika ukurasa wa 18 katika hotuba ya Waziri wetu katika vivutio. Nilikuwa naomba tu ili tutoe vivutio vya wawekezaji wa kutoka nje na wa ndani ya nchi yetu, hivi tunapopunguza maeneo ya mapato yetu tuangalie ni maeneo gani ambayo hayataathiri mapato yetu kwa sababu mpaka sasa hivi tunavyozungumza *TRA* imefikia katika kiwango kizuri sana cha kukusanya mapato na tunawekeza maeneo haya kuhakikisha kwamba mapato yetu yanazidi kukua. Sasa nitaomba tuweke vivutio vya kuwavutia wawekezaji waje lakini tusiathiri mapato yetu ambayo tunayategemea katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiendelea katika ukurasa wa 18 huu ambao la mapato nilishalimaliza, basi ninaangalia katika kipengele cha d, msamaha wa ukaguzi wa mizigo kabla ya kuingizwa nchini wasamehewe wasiwe wanakaguliwa. Ninatoa tahadhari tu tukiacha namna hiyo wazi kabisa nafikiri kuna wengine wanaweza kupenyeza mambo yao ya kuleta labda silaha au nini kama tusipokuwa makini katika kuweka misamaha ya kukagua mizigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni msamaha wa kodi ya thamani kwa gharama za huduma na yenyewe nilikuwa naomba tu Wizara ikae na wataalamu wa kuhusu hii misamaha ya kodi ili watoe sababu za kuonyesha kwamba hapa haitaathiri mapato yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho nilikuwa naomba tu kwa sababu bado kuna muda unaweza ukampa nafasi ili aweze kuchangia vizuri, niombe mapendekezo ya Kamati katika ukurasa wa nane wa maelezo ya Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Fedha na Uchumi kuomba idadi ya wale wajumbe wanaoteuliwa kuwa wanne basi ningeomba ipendekezwe tu iangaliwe jinsia zote mbili kama wanne basi iwe mbili wanawake na mbili wanaume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga hoja Muswada huu upite bila wasiwasi na ninawapongeza sana Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, tuendelee, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema kwa mchana huu yeye atakuwa msemaji wetu wa mwisho, halafu pia tukumbushane ipo Kanuni ya wale ambao hawakupata *floor* kuwa watulivu wakati wengine wanaongea.

Kwa hiyo, sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.48 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. RICHARD S. NYAULAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi ambayo umenipa ili niweze kuchangia Muswada huu.

Awali ya yote ningependa kutoa pongezi kubwa sana kwa maelezo mazuri ya Muswada ambayo yamefanywa na Waziri husika. Vile vile ningependa kutoa pongezi kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa kuweza kuunga mkono na kwa kuweka hoja nzito katika kuukubali Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni mzuri sana. Kwa hakika unaweza kuleta manufaa makubwa sana katika nchi yetu kwa sababu umelenga kuongeza kasi ya maendeleo, kuongeza ajira. Vile vile nina imani kabisa kwamba umelenga katika kuongeza uchangiaji wa kodi katika Mfuko wa Serikali. Lakini pamoja na kwamba Muswada ni mzuri nilikuwa nafikiri kwamba nichangie hoja kama mbili au tatu ambazo zingeweza kuboresha Muswada huu.

Sehemu ya kwanza ni kwamba *SEZ* ni njia mojawapo ya uwekezaji. Kwa kawaida vitu vyote ambavyo ni vya uwekezaji ni vitu vya kibiashara na kwa hiyo, uanzishwaji wake huwa unafanyika zaidi katika maeneo ambayo yanaweza kuleta faida kwa mwekezaji muda mfupi zaidi. Kwa misingi hiyo, ina maana kwamba inastahili kuanzishwa sehemu ambapo kuna miundombinu na ndiyo maana hata hii *SEZ* ya sasa imeanzia Dar es Salaam ambayo kuna miundombinu mizuri zaidi kwa kuwezesha hiyo *SEZ* kufanya kazi vizuri zaidi.

Kwa mantiki hiyo basi, sehemu zile ambazo hazina miundombinu mizuri kama sehemu za Magharibi ya nchi pamoja na sehemu za Kusini hazitapata nafasi ya kuwa na *SEZ* kwa muda mfupi ujao. Kama zitaanzishwa basi itakuwa katika miaka ya mbali kutokea hivi sasa. Lakini kwa wakati huo huo tunajua kuwa sehemu za Kusini na sehemu za Magharibi za nchi ndiko huko kunakohitaji maendeleo zaidi na nilikuwa nafikiria zaidi kwamba *SEZ* ingeweza kutumika kama kichocheo cha kuweza kuleta maendeleo katika maeneo haya. Katika misingi hiyo nilikuwa nafikiria kwamba kungekuwa na upendeleo maalum kwa upande wa Serikali katika kuanzisha *SEZ* katika mikoa ya Kusini pamoja na mikoa ya Magharibi ili kuweza kuleta kichocheo cha maendeleo katika sehemu hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kutoa mfano wa maeneo kama ya Mkoa wa Mbeya, ambako kuna uwanja mkubwa wa ndege ambao unajengwa wa Songwe. Huu ni uwanja wa Kimataifa ambao ni wa pili kwa ukubwa katika Tanzania, lakini kwa hakika uwanja huu ulipokuwa unajengwa ulikuwa unatazamia kwamba kuhudumia sehemu nyingi za nchi za *SADC*. Tunategemea kuwa ukianza kufanya kazi vizuri nchi za *SADC* pamoja na mikoa mingine ya Kusini zinaweza kutumia uwanja huo vizuri zaidi.

Katika misingi hiyo kuanzisha *SEZ* katika maeneo ya Mbeya namna hiyo maana yake ni kwamba tutaweza kusaidia kuinua shughuli za maendeleo na ambazo zitaweza kusaidia hata kuweza kupeleka bidhaa zetu katika nchi za jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya kusini yana mvua nzuri na ukiangalia katika miradi ambayo Mheshimiwa Waziri alikuwa ameitaja asubuhi maua, mboga mboga na hata maharage ya soya yote haya yanaweza kupatikana sehemu za Kusini kwa sababu hali ya hewa ni nzuri, ardhi ni nzuri na ni kubwa na kuna watu ambao ni wachapakazi wenye uwezo wa kuzalisha hasa kwa mtindo wa *contract farming*.

Naomba kwa misingi niliyoieleza ya namna hiyo kwamba Serikali itakapokuwa inaanzisha *SEZ* ijaribu kuangalia kuanzia na sehemu za Kusini pamoja na Magharibi. Kwa baadaye inaweza kwenda sehemu za Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaanzisha miradi hiyo katika sehemu za Kusini iruhusu *SEZ* kama chombo cha biashara kuanzishwa na wafanyabiashara. Katika maeneo yale ambayo miundombinu imekuwa ni mizuri zaidi. Miundombinu inaweza ikawavutia wafanyabiasha wakubwa ili kuweza kuanzisha *SEZ* katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napendekeza kwamba mikoa kama ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza ambapo tayari miundombinu imeshakuwa ni mizuri zaidi inaweza kuwavutia wawekezaji wafanyabiashara kuliko sehemu za Kusini. Kwa hiyo, sehemu za Kusini Serikali ijaribu kusukuma maendeleo kwa kuweza kujenga *SEZ* na sehemu nyingine ambazo miundombinu imekuwa imara basi wafanyabiasha wanaweza kupewa nafasi ya kuweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo nataka kuchangia ni suala linalohusu uchambuzi yakinifu ambao unastahili kufanywa na Mamlaka husika. Kama uchambuzi huo ukifanyika, maana yake wafanyabiashara watatumia mchanganuo huo kuamua na kisha kuruhusiwa kufanya biashara katika maeneo hayo ya *SEZ*.

Sasa hapo mimi napata kigugumizi kidogo kwa sababu kama uchambuzi yakinifu umefanyika na mamlaka na baada ya uchambuzi yakinifu wafanyabiasha wanatumia hiyo *report* kwenda kuwekeza katika eneo la *SEZ* na endapo kutatokea wafanyabiashara kutofanya kazi zao vizuri hawatapata faida. Aidha, kwa sababu wana mitaji midogo au kwa sababu ya uongozi mbaya hao wafanyabiashara watatoa kisingizio kwa mamlaka iliyofanya uchambuzi yakinifu.

Kwa hiyo, watatoa kisingizio kuwa wanapata hasara kwa sababu uchambuzi yakinifu haukuwa umetoa taarifa sahihi. Kwa hiyo, hapo naona kwamba kunaweza kuwa na utata kidogo na inaweza kuwa ni eneo ambalo kunaweza kutokea migogoro baadaye kwamba wafanyabiashara kuanza kuishtaki mamlaka kwa kuwa hawajapata faida.

Kwa hiyo, nashauri kwamba endapo uchambuzi yakinifu ukifanyika na mamlaka basi sehemu hiyo iwe ni Serikali ambayo inahusika kwa ajili ya kuweza kujenga *SEZ* inayohusika.

Lakini mahali ambapo tunafikiri kwamba wafanyabiashara wanaweza kuwekeza katika eneo la *SEZ* basi wafanyabiashara hao wapewe nafasi kufanya uchambuzi yakinifu kwa sababu watakuwa wanajiridhisha kwamba eneo hilo ndilo ambalo linaweza kuwaletea faida kwa siku zijazo. Kwa kufanya hivyo, natumaini eneo la utata halitakuwepo. Kila mmoja ambaye anataka kuwekeza ikiwa ni Serikali ifanye uchambuzi yakinifu na kisha iwekeze kwa utaratibu, natumaini haya matatizo ya utata na kuingiliana madaraka utapungua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kuchangia katika hoja hii linahusiana na vivutio. Naishukuru Serikali kwa kuweza kufikiria vivutio mbalimbali ambavyo wanastahili kupata wawekezaji ili kuweza kuwavutia na kuweza kujenga maeneo haya ambayo tuna uhakika wa kuweza kutuletea maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina matatizo makubwa na vivutio vingi ambavyo vimependekezwa, lakini nafikiria kwamba suala la kuondoa kodi ya makampuni moja kwa moja linanipa matatizo kabisa. Wafanyabiashara wanakwenda *SEZ* kwa ajili ya kufanya biashara baada ya kufanya uchambuzi yakinifu kwa hiyo, wanakuwa wanajua kwamba biashara ya *SEZ* italeta faida na biashara.

Kwa kuwa tumetoa misamaha mingi mimi nafikiria itakuwa ni vizuri kama watalipa kodi ya makampuni. Lakini kama tunafikia kwamba tunastahili kutoa kodi hiyo basi ingekuwa ni vizuri kungeweza na upendeleo maalumu wa kupunguza kiwango cha kodi, kutoka asilimia ya kodi ya 35 kwa 15% mpaka 20% ili angalau na wenyewe waweze kuchangia katika kipato cha kodi kwenda Serikalini.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya kuwa na maeneo ya maendeleo kama *SEZ* ni kujaribu kupanua uwanja wa kuongeza kodi kwa upande wa Serikali. Katika hotuba ya *workshop* tuliyoifanya majuzi Waziri wa Fedha alikuwa ameeleza kwamba tatizo kubwa ambalo tunalo katika Tanzania ni kwamba wigo wa mapato ni mdogo zaidi kwa hiyo kama tukiruhusu hizi *SEZ* zianzishwe na wasilipe kodi ina maana kwamba wigo wa mapato uzidi kuwa mwembamba zaidi.

Kwa hiyo, nafikiri kuwa mtu ambaye anawekeza katika *SEZ* ni sawa na mfanyabiashara mwingine yeyote ameshapewa *concession* za aina mbalimbali lakini kwa upande wa kodi basi anastahili kulipa kodi ambayo inastahili. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeongeza wigo kwa kukusanya kodi zaidi kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono moja kwa moja Muswada huu na kuomba maoni yangu yaangaliwe zaidi ili kuweza kuboresha Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia kwenyeMuswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyotoa mada yake asubuhi ya leo wakati akitoa hoja na ukisoma huu Muswada kweli unaona nia thabiti ya Serikali ya kuendeleza nchi hii ili tutoke hapa tulipo tuweze kwenda katika manufaa zaidi, kwa kweli nilikuwa napitia hii hotuba aliyoitoa asubuhi Mheshimiwa Waziri unaona kabisa kwamba sasa huko tunakokwenda mwanga unaonekana.

Lakini kuna mambo ambayo mimi nimesema naona ni vizuri tuyaangalie, tumegawa hizi *zones* katika *Special Economic Zones,* kama kuna *zone* ambayo nadhani ilitakiwa ipewe *priority* ya kwanza basi ilikuwa ni Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kigoma tumepakana na nchi nyingi sana na ni moja ya wanasema *it is a sleeping giant,* bado hatujatumia ule mpaka vizuri. Kama nilivyosema tuyaangalie kwa makini, ukisema unaanzisha *SEZ* Kigoma hakuna mwekezaji yeyote atakayekwenda Kigoma kwa sababu hakuna miundombinu ya kufanya mwekezaji avutiwe kwenda pale ingawa una hakika ukiweka pale ile *hub* anayosema Mheshimiwa Waziri tutapata *market* kwa sababu tumepakana na nchi nyingi. Lakini leo Kigoma hakuna barabara, umeme, maji. Sasa huyo mwekezaji anayekuja Kigoma anaanzia wapi? Hata kama kuna mipango hiyo ya kuleta maji, umeme na barabara Kigoma ninaamini Serikali ina mpango lakini itatekelezeka lini?

Nilidhani ni muhimu sasa tuwe *realistic,* tuondoke kwenye nadharia nyingi sana, tuwe *realistic* kwamba jambo hili tunafanya tuwe tuna maandalizi ya kutosha. Mheshimiwa Waziri mwenyewe amesema mkichelewa wawekezaji wanatembea ni kama ndege kwa hiyo, watakwenda ku-*invest* kwingine, kwa hiyo, ninyi mna *potential* lakini hamjajiandaa kwa hiyo, mwekezaji hawezi kusubiri ninyi mjiandae.Kwa hiyo, ningeomba sasa tujiandae kwa kasi kweli kweli ili tuweze na sisi kuwavutia wawekezaji na wengi waweze kuja kwetu na hatimaye nchi yetu ifaidike.

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi wakati Mheshimiwa Waziri anasema ameainisha vizuri kabisa kwamba tujenge tabia ya kutekeleza mipango na maamuzi yetu kwa ukamilifu na kwa wakati. Sasa mimi nilidhani hii sentensi yake ni ya muhimu sana wakati anahitimisha kwamba sasa tuweke muda maalum kama tuna hakika mpaka baada ya miaka hii tutakuwa tumetekeleza haya kwa mkoa wa Kigoma ili kama sehemu ambayo nayo ni *potential* katika *SEZ.* Mimi naamini katika nchi hii Magharibi bado

haijafunguka lakini Magharibi ina *potential* kuliko maeneo mengine yoyote katika nchi yetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba wakati tunaamua haya basi juhudi za kufanya Mkoa huu ufunguke ama Magharibi ifunguke basi juhudi hizi ziwe kubwa maana ukiangalia ukifuata kama tunataka kujenga barabara ukiiangalia hii *Project Circle* ya kuanzisha barabara mpaka una-*identify you want to build this road* mpaka siku ya mwisho mtu anajenga ni miaka minne mpaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, una hakika kwamba huyu mwekezaji atakuwa anawasubiri ninyi mjenge barabara kwa miaka minne au mitano ijayo muweke *airport* ndiyo aje? Matokeo yake zitabaki ni nadharia kama alivyosema asubuhi Mheshimiwa Waziri na mimi nisingependa sasa tuondoke kwenye kuwa watu wa nadharia kila wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la kiwanja cha ndege cha Kigoma. Kiwanja cha ndege cha Kigoma kinaweza kikasaidia tuna hakika ndege itatoka Dar es Salaam itafika Kigoma watu watakwenda Kongo Brazzaville, watakwenda Burundi kutokea pale na leo tunavyosema kuna *Air Burundi* inakuja kwenye kile kiwanja lakini kile siyo kiwanja.

Lakini leo ninayo hakika tunayo *Kilimanjaro Airport,* upo mpango wa kujenga *Arusha Airport* lakini hivi kweli kwa maana ya ku-*priotise* kiwanja cha Arusha inawezekana ni cha muhimu lakini kwa sasa ni cha muhimu kuliko cha Kigoma wakati tunayo *KIA?* Nadhani imefika wakati tufanye *distribution* za *resources* vizuri. Inawezekana nia thabiti ya Serikali ya kujenga kiwanja cha *Airport* cha Arusha ni nzuri na kuna sababu lakini kuna maeneo mengine ambayo hayajafanywa ni vizuri *resources* hii iende kufanya kule ambako tuna hakika napo patainua uchumi wa nchi yetu tukishamaliza kule sasa *then* ndiyo tuje tutakwenda kufanya Arusha lakini kwa sasa Arusha bado inaweza *served* na *KIA.* Hili nalo nilitaka Mheshimiwa Waziri nalo aliangalie kwa makini ili kweli hizi *SEZ* ziwe na maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni suala la *education.* Ukiangalia wenzetu kule Asia wameendelea kwani kazi ya kwanza ilikuwa ni elimu, lakini nimesikiliza hata asubuhi Mheshimiwa Waziri anajibu maswali naona tunakwenda kwenye kufikiria wanafunzi wengi waende shuleni, wapate elimu ya msingi na wengi wapate elimu ya sekondari, naona hatujadili suala la *quality* ya *education* kwa sababu leo kuna shule za sekondari za vijijini zina walimu wawili, shule ina walimu wawili shule hii haiwezi kutoa elimu ya kutosha na huo ndiyo ukweli.

Kwa hiyo, niombe sasa na suala la elimu tulipe kipaumbele, kuna *issue* ya walimu, kuna vitabu, maabara lakini pia tuziangalie *curriculum* zetu ziweze kukidhi *international standards* ili na sisi tuweze ku-*compete otherwise* tutaanzisha vitu hivi vyote lakini sisi tutakuwa waangaliaji katika maendeleo yetu. Leo tunakwenda kwenye *East African Community* watakuja watu kutoka Kenya wako *well qualified* sisi tutakuwa vibarua wao zile kazi zote za maana watachukua watu ambao si Watanzania.

Kwa hiyo, nilidhani suala la elimu nalo ni la muhimu sana katika kwenda kwenye haya mapambano makubwa ya kidunia kwa sababu leo tunakwenda kwenye dunia ya utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, dunia ya utandawazi haina huruma hata kidogo, tunayo hakika tusipojiandaa tutaanza kujilaumu wenyewe kwa hiyo, nadhani sasa tuondoke kwenye kusema *education* yetu ni kuhakikisha watoto wengi watakwenda shuleni, mimi nasema hapa, nadhani nafuu tupate wachache lakini iwe *quality,* leo *University of Dar es Salaam* watu wanamaliza mtu hawezi kuongea hata kiingereza, huo ndio ukweli. Ukienda kwenye *interview* ukiwaita vijana waliomaliza *University* wengine hata na *Masters* utashangaa, kwa hiyo, ningeomba *quality education* yetu iwe ya muhimu sana.

Lakini pia kuna *issue* ya *Science and Technology.* Katika dunia ya leo tunataka lazima *Science and Technology* ni ya muhimu sana kwa sababu tunaelekea kwenye kuwa *industrialized* ili tuweze kwenda kwenye viwanda ni lazima elimu ya Sayansi na Teknolojia iwe nayo tui-*incorporate* kwenye *curriculum* zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na mimi naunga mkono hoja lakini ningependa mambo hayo niliyoyasema tuangalie kwa kina na tuyafanyie mkakati wa kweli kweli ili *SEZ* hizi ziwe na maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naomba nichukue nafasi hii kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada ambao uko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naendelea kuipongeza Serikali. Serikali yetu mara zote inaendelea kuangalia ni namna gani inaweza kuandaa sera na mipango mbalimbali ya kuweza kuwezesha jamii ya wananchi wa Tanzania kukimbizana na wakati katika suala zima la maendeleo ya kiuchumi, kijamii na hali nyingine tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada uliopo mbele yetu kwa kweli hata mimi nasema kwamba ni Muswada wa kimsingi sana. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi imesisitiza sana suala zima la kufanya *modernization* katika maeneo tofauti ya kuleta maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizingatia suala zima la kimsingi la *modernization* ya uchumi na maendeleo ya Watanzania basi mimi nasema kwamba Mheshimiwa Waziri Mzee wetu Dr. Juma Ngasongwa na Naibu wake kwa jinsi walivyo watendaji wazuri, ninaamini kabisa kupitia Muswada huu watachangia kiasi cha kutosha katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi iliyouzwa na Chama cha Mapinduzi na hasa kwa kuzingatia Serikali hii ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa kuharakisha uwekezaji na uzalishaji ni wa kimsingi kabisa na Muswada huu utasaidia sana kuhusisha raslimali walizonazo wananchi na maeneo waliyonayo katika kuleta maendeleo endelevu ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi labda nikipitia katika vifungu mbalimbali vya Muswada wenyewe nilikuwa naangalia maeneo fulani fulani ambayo labda yangesaidia kuuboresha kama itaonekana kwa kufuata sheria na taratibu inaweza ikasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Kamati kwa kutoa lile pendekezo la kuongeza wale Wajumbe kutoka wawili mpaka wanne ukurasa ule wa 24 na wale ambao watakuwa *appointed* na Mheshimiwa Rais na mimi nasema kwamba ninakubaliana na Kamati ninaomba Mheshimiwa Waziri alizingatie hilo. Lakini nilikuwa nafikiria kwamba wale wengine wawili watakaoongezeka basi labda Kanuni ya kiutekelezaji izingatie wahusika wakuu ambao watakuwa katika mfumo mzima wa maeneo haya muhimu ya uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika ukurasa wa 24 wa Muswada wenyewe iko pale *Article number 4* katika ukurasa wa 24 ambayo ni *addition point* ya *sub section one* ambayo iko ukurasa uliotangulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hiyo *addition point* ambayo inazungumzia suala la kazi ambazo zitafanywa na mamlaka. Mimi nilikuwa nashauri kama inawezekana ni kwa nini pale tunaanza kuzungumzia *function* za mamlaka tusiongeze *concept* ama tusiongeze wazo la kuonyesha kwamba uwepo umuhimu wa kufanya majadiliano baina ya mamlaka, Wizara husika ama *Local Government* ama tuseme Halmashauri zetu ili kuweza kutekeleza *functions* ambazo zimeorodheshwa pale chini. Nina maana kwamba *with the consultation* ya *Ministers* ambayo labda *Minister* wa Ardhi ama *Local Government* halafu ndiyo zile *function* ziweze kufanyika kadri ya zilivyoainishwa pale chini kwenye ukurasa wa 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza hilo kwani ninachoelewa ni kwamba kama tutaacha tu *functions* hizo zifanyike bila kufanya mawasiliano ama mashauriano na *Local Government* ama vyombo vingine ambavyo ndivyo vinavyoshika raslimali kule ambako watu wapo inaweza pia kidogo ikaleta matatizo ya namna moja ama nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 29 nimeona Muswada unaeleza ni namna gani mamlaka imejipangia siku za utekelezaji wa kazi mbalimbali. Mimi nalipongeza sana hilo na ninaona ni suala la msingi kwamba vitu vyote ambavyo vinatendeka kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu ni lazima viwe na muda maalum, lakini nilikuwa napenda Mheshimiwa Waziri ni kwa nini hakuona pia umuhimu wa kuwapa siku za utekelezaji wale *developers* wote ama wale wote ambao watakuja kuwekeza?

Mimi nadhani kumekuwa na *experience* mtu anaweza kuamua kusaidia kuwekeza katika suala fulani lakini badala ya kufanya shughuli zake za uwekezaji kwa mwaka

mmoja anaweza aka-*relax,* akafanya taratibu hata kwa miaka 10 sasa bila kuwa na kipengele cha sheria ambacho kitambana na yule *developer* naye katika muda fulani awe ameshamaliza kufanya utekelezaji wa uwekezaji ama wa hatua za kiutekelezaji ninafikiri kwamba kunaweza kukawa na tatizo moja kubwa la kimsingi la kiutekeleza wa kazi zenyewe katika azma hii ya kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile nilikuwa naendelea kufuatilia hotuba ya Mheshimiwa Waziri na hasa alipokuwa akiwasilisha Muswada huu kwenye Kamati iliyochambua Muswada.

Mimi nakubaliana kabisa kwamba kazi imefanyika ya kutosha ya kuanza kuteua mikoa itakayoshughulika katika mpango huu ambao ni wa muhimu sana kwenye suala la kukuza uchumi. Lakini kila mkoa ambao umeteuliwa kwenye karatasi ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha kwenye Kamati kumewekwa vigezo vilivyosababisha mkoa ule labda uteuliwe ama upewe kipaumbele katika suala zima la kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimestushwa tu kwa kitu kimoja kwa kuona kwamba mpango mzima wa utekelezaji umechukua maeneo ya Kusini na hasa unapogusa Mtwara na Lindi na Mheshimiwa Waziri amezungumzia sana pale kwamba azma ama dhana ya *Mtwara Corridor Development* imekuwa ni kigezo kikubwa cha kuchukua mkoa wa Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri na timu yake wakahama kwenye Mkoa wa Lindi na Mtwara wakahamia Iringa, Mbeya na Rukwa. Sasa mimi imenishangaza kidogo sijui ile Ruvuma imeachwa wapi, kwa sababu unapochukulia *concept* ya kuendeleza Bandari ya Mtwara kwenye suala zima hili la kuendeleza maeneo maalumu kiuchumi huwezi kuzungumzia Bandari ya Mtwara kwenye mpango wa *Mtwara Corridor* bila kuzungumzia Bandari ya *Mbamba Bay,* haiwezekani kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimeshangaa kidogo sijui hawa wataalamu wetu walikuwa wanawaza nini na kwenye *concept* iliyojengwa pale kwa ajili ya ku-*select* mkoa wa Mtwara na Lindi wao wamesema kwamba kigezo kikubwa ni Daraja la Umoja namba moja linalojenga kuunganisha Mtwara - Lindi na Msumbiji kwa maeneo ya Kusini, sasa hayo maeneo ya Kusini kwa maana hiyo Ruvuma haiko Kusini, sasa sijui Ruvuma iko Kaskazini ama iko wapi, hiyo inanipa shida kidogo. Kwa sababu unaposema unaendeleza maeneo ya Kusini aidha, Ruvuma uiunganishe na Mtwara na Lindi ama uiunganishe na Iringa na Mbeya.

Sasa kwenye Iringa hatupo, kwenye Mtwara na Lindi hatupo, *concept* ya *Mtwara corridor* ipo hapo, sasa kwa kweli hiyo imenishangaza na kunistua. Sasa mimi naomba kusema ama Mkoa huu wa Ruvuma uingizwe haraka sana kwenye mpango huu vinginevyo mpango huu utakuwa na malengo ya kutenga Mkoa wa Ruvuma usiwe na kwao, usiwe na Kusini wala usiwe na Kaskazini ubaki yatima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nasema kwamba nampongeza Mheshimiwa Waziri, nimeanza kwa kusema kwamba Mzee wetu Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa ni mtu makini sana. Nami naamini inawezekana wakati wanaandaa hii walisahau tu kuingiza Mkoa wa Ruvuma na ninaamini kabisa wakati anajibu hoja ataniambia tu kwamba kuna karatasi moja ilisahaulika na atakuwa ameiweka itakayoonyesha kwamba Mkoa wa Ruvuma upo ili kama kweli tume-*select* Mikoa ya Lindi na Mtwara kwa maana ya *Mtwara corridor* ina maana hatuwezi kuondoa bandari ya *Mbamba Bay* ambayo mpaka sasa hivi sisi tunahangaika kuona kwamba ni lazima ianze kushughulikiwa. Kule wenzetu Malawi katika mpango wa Mtwara *corridor* wameshapiga hatua kubwa sana kwa maana hiyo utakuwa umeshapitia maeneo haya yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizungumzia pia kigezo cha eneo ambalo linapata mvua kwa mwaka mzima, mimi namshukuru Mungu Mkoa wa Ruvuma sasa hivi mvua ambazo zinanyesha sio kawaida. Sasa sijui unaachaje. Ama ukizungumza habari ya Mtwara na Lindi ukaacha Tunduru, hadhi iliyoko Mtwara, Lindi, Masasi na Tunduru inafanana kabisa wala haitofautiani.

Sasa sisi ni mapacha, sijui tuseme watatu ama sijui wangapi na tunaendelea kusema, tunaomba Kusini mtuangalie na kwa kweli mpango huu utatusaidia sana Kusini na naomba sana hii Ruvuma kama nilivyosema Mheshimiwa Waziri karatasi aliyoisahau aiongeze hapa ili tuweze kuiona na Ruvuma nayo iingie na naamini kwa timu yake na Naibu Waziri wake mambo hapa yatanyooka na yatakwenda vizuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kumtakia Mheshimiwa Waziri kazi njema. Hii kitu itatusaidia sana na naamini baada ya muda basi tupanue mpango huu kwa nchi nzima ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kupata nafasi ili niweze kuchangia machache katika huu Muswada ambao uko mbele yetu wa *SEZ.*

Kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa ajili ya kuleta Muswada huu lakini pia niwapongeze hata wataalam wake ambao wameshiriki katika kuandaa Muswada wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi tumezoea kusema kwamba Muswada umekuja kwa wakati wake, lakini mimi ningesema pengine huu Muswada umekuja kwa kuchelewa kwa sababu tunapata manufaa yanayoonekana kwamba katika Muswada huu kama hii *SEZ* itaanzishwa basi utakuwa na manufaa makubwa sana kwa maana ya kwamba tunategemea kwanza utaongeza ajira kwa watu wetu lakini pia utasaidia sana katika kukuza uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nichangie machache kama ifuatavyo, kwanza Mheshimiwa Waziri alipokuwa anatoa hotuba yake akiwasilisha Muswada wake alisema kwamba wataalam wetu na wataalam kutoka *Japan Development Institute* walifanya ziara katika baadhi ya Mikoa kuangalia maeneo ambayo yangefaa kwa ajili ya uanzishwaji wa *SEZ.* Moja ya eneo ambalo lilitembelewa ni pamoja na Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, alipokuwa anachangia Mheshimiwa Richard Nyaulawa alizungumza sana kuhusu upande wa Mbeya. Baadhi ya maeneo ambayo yanafaa sana kuwekeza katika Mkoa wa Mbeya ni pamoja na sekta ya kilimo kama hotuba ya Waziri ilivyobainisha. Mimi nafikiri kwamba ili tuweze kuwekeza kwenye kilimo na ili tuweze kuwapata watu ambao wapo tayari kuwekeza kwenye kilimo lazima hawa watu wahakikishiwe kwanza kwamba *infrastructure* itakuwepo na mwenzangu Mheshimiwa Richard Nyaulawa alizungumzia kiwanja cha ndege kinachojengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nachangia hotuba ya Mheshimiwa Rais, mimi niliomba sana kwamba Serikali ni vizuri ikafikiria kujenga Kiwanda cha Mbolea Mkoa wa Mbeya ingawa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika alipokuwa anajibu hoja alisema kwamba si lazima kiwanda kijengwe Mbeya kwa sababu mwekezaji anaweza kuchagua mahali popote pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nilikuwa nafikiri bado ni muhimu ili kuvutia wawekezaji ambao wanaweza kuwekeza katika eneo hili ni lazima pia tuhakikishe kwamba nchi hii inazalisha mbolea na mimi sitaelewa kwamba tunaita au tunaanzisha maeneo ya uwekezaji, tunaanzisha *SEZ* kwamba watu wawekeze kwenye kilimo lakini hawana uhakika na upatikanaji wa mbolea. Mimi naona kwamba pengine watu wanaokuja kuwekeza katika eneo hili wanaweza wasione kwamba ni busara sana, tutakuwa tunaanzisha vitega uchumi vingi lakini bado watu wakalazimika kuagiza mbolea tena kutoka nje ya nchi. Naomba Serikali ifikirie mara mbili mbili, tutakapoanzisha *SEZ* basi watu ambao wataitwa au wataombwa kuwekeza wawe ni wale ambao wanaweza kuwa tayari kujenga Kiwanda cha Mbolea hasa katika Mkoa wa Mbeya ambao mimi nafikiri ni *link* nzuri katika Mikoa yote ambayo ipo Nyanda za Juu Kusini, lakini pia na Mikoa yote ya kilimo katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka pia nichangie kidogo kuhusu ni maeneo mangapi, sasa hivi tunatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2005 - 2010, lakini Mheshimiwa Waziri aliposema kwamba wataalam walipita akasema kwamba wamebaini ni maeneo karibu ishirini na tano mpaka thelathini ambayo *SEZ* hizi zinaweza kuanzishwa. Sasa hii inasemekana kuanzia sasa mpaka mwaka 2020 tunatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na inapofika mwaka 2010 maana yake ni lazima tuweze kuwaambia Watanzania kwamba Ilani ya Chama cha Mapinduzi tumeitekeleza kwa kiwango gani kwa maana ya kwamba maeneo ya *SEZ* katika eneo hilo ambalo tumewekeza katika kipindi hicho ni mangapi. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiri ni vizuri angesema pia tunawekeza maeneo ya *SEZ* mangapi na pengine tumeajiri au tunategemea kuajiri watu wangapi katika kipindi hicho kwa maana kwamba ndio mambo ambayo tutawaeleza wapiga kura wetu wakati tutakapokuwa tunaomba tena kura mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumze kidogo kuhusu wigo wa kodi. Mimi nilivyokuwa nasoma Muswada huu kidogo imenitisha kwa sababu sehemu nyingine karibu tunaondoa kodi zote. Lakini ukichukulia mifano ambayo Waziri alikuwa anaitaja ya nchi zingine ambazo pengine tumejifunza, tumeona wenzetu maeneo mengine kuna kodi za kiasi fulani wameweka au ule muda wa kulipa kodi umepunguzwa. Sasa sisi maeneo mengi tumeweka miaka kumi na pengine kodi zile hazipo kabisa.

Sasa mimi nilikuwa nafikiri hata kama tunataka tuanzishe hizi *SEZ* zitusaidie kukuza uchumi na kuleta ajira, lakini tusije tukuwa wanyonge sana kwa kuondoa kodi zote ambazo mimi sidhani kama zinaweza kuwa ndio hasa maana ya Muswada huu kwa sababu tunategemea pia na Serikali na yenyewe inufaike kutokana na kodi ambazo hawa wawekezaji wanalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasi wasi wangu ni kwamba mwekezaji anawekeza miaka kumi, inapofika mathalani miaka nane huyu mtu anaweza kuamua kuondoka pengine sijui kama Muswada umezungumzia kitu gani kwamba mtu amewekeza unasema baada ya miaka kumi ndio aanze kulipa lakini kabla ya hapo akaondoka au biashara yake ikaenda vibaya na yeye mwenyewe asiweze kuendelea na Serikali itakuwa haijapata kitu chochote hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichangie kuhusu suala la ajira. Suala la ajira huwa linakuwa na matatizo mahali pengi sana. Tumeona makampuni mengi ya kigeni ambayo yamekuja katika nchi hii, mengi yalikuja na wataalam wake na wakati mwingine hata sheria zilisema kabisa kwamba, watakuja na wataalam wa ajira watano au kumi, lakini baadaye imekuja kudhihirika wataalam waliokuja ni wengi zaidi kuliko wale ambao Sheria zilihitaji wawepo. Mahali pengine kwa mfano, *NBC* ilikuja kubainika kwamba watu walikuja na wakasema hao ni ndugu zao, wengine watoto wao au wamekuja kutembea tu, lakini baada ya muda fulani wakabainika hawa watu wanafanya kazi na sijui maafisa waliohusika kama walichukuliwa hatua zozote za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa natahadharisha kwamba pamoja na kwamba katika Muswada huu tunasema kwamba Serikali italazimika pengine kama Muswada unavyosema kwamba watakuja watu watano, sasa Serikali iwe makini sana katika eneo hii tusije tukasema watu wanakuja watano halafu baadaye ikaja kubainika kwamba watu ambao wameajiriwa ni wengi kuliko idadi hiyo iliyotajwa.

Kwa hiyo, mimi naomba Watanzania ndio tunataka wapatiwe kazi katika *SEZ* hizi ambazo tunategemea tuzianzishe, wasije Watanzania kuwa vibarua na wafanyakazi wakawa wa kutoka nje au watu ambao wanakuja kuwekeza katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie Sheria ya Usalama. Inaonekana kwamba hata katika maeneo ambayo yaliwekezwa huko nyuma kama vile sheria zetu za usalama kazini hazieleweki sana. Mifano ambayo tunayo kwa mashirika ya kigeni ambayo yapo nchini mengi tumeona kabisa hayakuheshimu sheria zetu za usalama kazini. Watu wamekuwa wanashtakiwa bila taratibu, watu wanafukuzwa kazi

bila taratibu na inaonekana sheria hiyo hiyo ikienda mahali pale haifanyi kazi na wakati mwingine hata vyama vya wafanyakazi vimepigwa marufuku katika baadhi ya maeneo yale ambayo watu hao wamewekeza.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba niitahadharishe Serikali kwamba watu wetu wasije wakawa watumwa katika nchi yao pamoja na kwamba tunafanya kwa nia nzuri kwamba tunataka tuanzishe hizi *SEZ,* nchi yetu inaweza kukuza uchumi wake na watu wake wakapata ajira lakini tusimamie sana sheria hii ya usalama kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilitaka nizungumzie hivyo hivyo kidogo kuna Sheria ya Uhamiaji, kama nilivyosema kwamba kuna watu ambao wataingia kazini ambao hawakuwa kwenye sheria au sheria haiwatambui. Watu hawa wanaoingia mimi sidhani wanapita sehemu gani ambazo hata watu wa uhamiaji wanashindwa kujua. Kwa hiyo, nafikiri inapobainika kwamba watu wapo nchini na hakuna hatua zozote ambazo zinachukuliwa na watu wa uhamiaji pengine kwa kutokujua basi hatua za kinidhamu pia zichukuliwe kwa hawa maafisa uhamiaji kwa sababu hawa watu watakuwa wanafanya kazi nchini, wameingia namna gani, wanafanya kazi namna gani nchini bila watu wetu wa usalama hasa watu wa uhamiaji kujua. Kwa hiyo, nafikiri ni eneo lingine ambalo Serikali iliangalie sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka pia nizungumzie suala la mazingira. Pamoja na kwamba hizi *SEZ* zitakuwa zinasimamiwa na Serikali lakini wale wenyewe watakaokuwa wamewekeza katika *SEZ* hizo inawezekana kabisa wasifuate kanuni au wasitunze mazingira. Leo Bunge hili linapiga kelele linasema kwamba kuna hali ya ukame kwa sababu mazingira yameharibiwa lakini hawa watakaokuwa wamewekeza humu tusipowaambia na wenyewe watunze mazingira au Serikali isipofuatilia tunaweza badala ya kutunza mazingira na wenyewe wakawa chanzo cha kuharibu mazingira kwa sababu najua kuna viwanda Dar es Salaam ambavyo vimeanzishwa na vinafanya kazi kinyume na sheria za kazi ambazo zipo na sheria za usalama kazini na kwa kweli wataalam walipofuatilia wameona kweli baadhi ya viwanda vinakiuka taratibu. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba sana Serikali ifuatilie sana watu ambao watawekeza kwenye *SEZ* hizi kwamba wanafuata sheria, taratibu na kanuni na hasa kadri ya Muswada wenyewe unavyoelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo naunga mkono hoja na ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii nami kukupongeza, nadhani nilipokuwa natoa hotuba yangu ya awali hukuwepo mezani lakini naomba nichukue fursa hii kukupongeza sana. Kwetu sisi hususan mimi, ambaye naamini kwamba wanawake tunaweza sana, tumefarijika na tunajivunia kuchaguliwa kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo sitasema yafuatayo, siku ya kwanza nilipoongea niliomba msaada wa waandishi wa habari, hivyo

naomba niwashukuru walinisikia Wilaya ya Kilindi na waliniona. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nichukue fursa hii nimpongeze sana Waziri wa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, kwa hotuba yake nzuri sana. Vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza pia Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi na Kamati yake yote kwa kazi nzuri waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona katika taarifa na hotuba ya Mheshimiwa Waziri tarehe 7 Julai, 2005 kulikuwa na semina ya mpango huu. Kwa kweli nimesikitika sana, nilikosa lakini kwa kusoma yaliyoandikwa naunga mkono yale yote ambayo Wabunge waliamua na kwa kweli nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema kwamba mpango huu kwa kweli umekuja kwa wakati ila tatizo ni moja ambalo naliona. Kama wengi walivyosema kwa sababu mengi ambayo nilipanga kuyasema yameshasemwa, sidhani kama kuna sababu ya kuyarudia. Lakini naomba niseme kwamba, nimeona hapa kwamba kulikuwa na ziara ambayo walizunguka katika Mikoa kadhaa na walifika Tanga kweli, lakini nina wasiwasi kama walifika Kilindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu kwa kweli Kilindi wengi hawaifahamu. Kilindi ina utajiri wa kila aina, tuna dhahabu ya kupindukia, tuna madini nadhani mengine mpaka leo hayajajulikana kama *gemstones,* tuna ardhi yenye rutuba ambayo ipo wazi, tumekaribisha wageni kutoka kila sehemu na wanaendelea kuingia kutoka Mikoa mbalimbali. Tuna misitu ya kila aina, tuna wanyamapori lakini utashangaa kuona kwamba miundombinu kule hakuna, hakuna anayejua habari zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahi kwamba jirani yangu Mbunge ambaye ndiye Mwenyekiti wa Fedha na Uchumi ametoa taarifa hii, nadhani ananielewa ninaposema kwamba kule tuna kila sababu ya watu kuja kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tu nilipokuwa nikipita kushukuru wananchi waliniambia, mama kazi ya kwanza tutafute watu wa kuja kuwekeza. Sasa nadhani Mheshimiwa Waziri umesikia. Tatizo letu kutokana na taarifa yako ni miundombinu. Kwa kweli barabara hatuna nzuri lakini tupo tayari hata kuzibaziba yale mashimo wawekezaji wakafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kilindi wana kiu ya maendeleo, wapo tayari kufanya lolote angalau na sisi tuingie kwenye huu mpango. Mara nyingi ukiongelea Tanga utaongelea bahari na fukwe zake na kadhalika lakini ninawahakikishieni utalii kule kwetu tuna milima ya kihistoria ambayo hata yule Chifu Kimweri kwa ambao mnafuatilia historia aliingia na mbwa mia moja ipo kule, imekaa imeachwa. Wajanja wachache Wajerumani wanaoijua wanakuja kiholela tu na kuondoka bila hata kulipa chochote. Kwa hiyo, nasema kwamba kwa kweli mimi nimefarijika, lakini tatizo langu je, tutaingizwa kwenye huo mpango kwa sababu nadhani kama kuna sehemu chache ambazo zimebaki zenye rasilimali nyingi mno ni Wilaya ya Kilindi. Kwa

hiyo, nilikuwa naomba sana mtakapokuwa mnapanga mtufikirie sisi kwa ukaribu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alizungumzia maeneo manne ambayo yatafanyiwa kazi kwa kipindi hiki cha miaka mitano. Narudia tu kwa sababu nisisitize, nayo ni kilimo, utalii, upandaji miti na *ICT,* naona hizo ndio *priorities* za miaka hii mitano. Naomba Mheshimiwa Waziri akumbuke Kilindi kuhusu kilimo, tunalima na hatumalizi maeneo na rutuba, ni nzuri mno na mazao ni mengi na ya kila aina alizeti inastawi, hiliki kule juu milimani inaozea mashambani. Naomba sana jamani na sisi tufikiriwe kwenye huu mpango kwa niaba ya wananchi wa Kilindi kwa kweli *otherwise* ule msemo wa *migrating birds will never fly down* Kilindi, nina hakika watakuwa wanaturuka tu wanapita hewani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala la kuingiza wataalam. Kwa kufanya kazi kwa zaidi ya miaka kumi na tano ndani ya Serikali nilibahatika kufanya katika kitengo cha ajira za wageni. Kwa kweli utaratibu huo unakuwa umewekwa lakini hawa wawekezaji saa nyingine wanakuja na mambo magumu, wanasema sisi tunataka kufanya kazi tunakwamisha tunakosa Watanzania wenye uwezo wa fani fulani, fulani. Pamoja na utaratibu ambao unakuwa umewekwa inafika mahali inabidi muweze kuwafikiria ku-*waive*. Kwa hiyo, ndugu zangu nasema kwamba hili ni suala ambalo linahitajika sana kuangaliwa kwa ukaribu na la pili basi tunaandaaje vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapanga watu waje wawekeze lakini vijana wetu tumewaandaa vipi na wazee pia sio vijana peke yao. Tumewaandaa vipi kuweza kufanya kazi katika maeneo hayo kama mnavyokumbuka Mheshimiwa Rais alisema hata kwenye hoteli unakuta Watanzania ni wale wako kwenye *low cadre* huku chini chini, lakini kwenye uongozi na *supervisory positions* zote wamechukua wenyewe wageni. Kwa hiyo, naomba na hili nalo tuliangalie kwa mkazo ili kwamba haya matatizo mengi tunayoyaongea endapo kutakuwa na watu wenye uwezo nina hakika tutaweza kuyasimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mimi sikuwa na mengi ila nilikuwa naomba tu ni-*solicit* kwamba Kilindi ifikiriwe kwa macho ya huruma. Wananchi wana kiu ya maendeleo, wapo tayari. Leo nilikuwa nazungumza nao kwa sababu *Celtel* imeanza kazi wiki hii Kilindi, kwa mara ya kwanza tumekuwa na mtandao. Nawashukuru sana kampuni ya *Celtel.* Kwa hiyo, tayari tuna mawasiliano, naamini kwamba kwa kuwezeshwa na Serikali na kwa kutumia nguvu zetu sisi wananchi wa Kilindi tutaweza kufika mahali.

Mheshimiwa Naibu Spika kwa kweli kama ninavyosema Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, namfahamu sana, ni mtu wa vitendo, nilikuwa naye Cancun, Mexico kwenye mkutano wa *WTO,* niliona ambavyo anaweza kufanya kazi hata katika mazingira magumu sana, naamini hata katika hili la Kilindi pamoja na mazingira yake magumu ataweza kutusaidia kutuingiza kwenye mpango na sisi hatimaye tuweze kunufaika na kuepukana na lindi hili la umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumepewa taarifa na wenzetu wa redio kwamba kama Mbunge anazungumza, wanaomzunguka wasizungumze, wakizungumza basi inaingiliana na mawasiliano yale yatakayotoa yatakuwa hayawi wazi. Kwa hiyo, nadhani tutazingatia hilo. Kwa hiyo, naomba nimwite Mheshimiwa Fatma Mikidadi atafuatiwa na Mheshimiwa Sameer Ismail Lotto na Mheshimiwa Aloyce Kimaro, akae amejiandaa.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi napenda kuwapongeza viongozi wote kwa sababu ndio mara yangu ya kwanza kusimama tangu nifike hapa Bungeni. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kumpongeza Rais, Mawaziri, Waziri Mkuu, Spika, Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, Wakuu wa Mikoa wote ambao wamepata nyadhifa hizo na vile vile kuwashukuru wananchi wa Lindi ambao wameniwezesha mimi kuja hapa kuwa Mbunge, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, kwa kuandaa mpango mzuri kama huu ambao kwa kweli utatuletea tija katika nchi yetu kama ulivyozungumzwa kwamba ajira zitapatikana, miundombinu itakuwepo na mambo mengine mazuri ambayo yataleta manufaa kwa nchi yetu. Kwa kweli nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 10 katika hotuba yake ameelezea maeneo ambayo yalifanyiwa utafiti wakitumiwa Wajapani pamoja na wataalam wa Tanzania. Maeneo hayo ni Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Iringa, Mbeya na Mtwara. Nataka nimwambie ndugu yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama, Lindi haikutajwa.

Mheshimiwa naibu Spika, sasa mimi nataka kuongezea hotuba ya mama Jenista Mhagama kwamba Ruvuma na Lindi haikutajwa. Nataka kusema tu kwamba kuna maeneo ambayo hayapitiki lakini kama yakichunguzwa vizuri maeneo hayo na yakawekwa miundombinu yanaweza kuwa na manufaa makubwa kuliko hata haya ambayo yametajwa sasa hivi yanaweza kuwa nyuma kwa mipango yake. Kwa mfano, maeneo ya Lindi na Ruvuma ambayo yametajwa hapa ambayo ni jirani na Mtwara kuna mambo mengi mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue mfano mmoja katika eneo la Mkoa wa Lindi, eneo la Mkoa wa Lindi pamoja na kwamba halipitiki na kwamba limeachwa katika mpango huu lakini kuna mambo yafuatayo ambayo yangeweza kuwa mazuri katika nchi hii, kwanza Kilwa kuna kisiwa kimoja kina boko mia tano, boko hao wanazungumza na binadamu ukiwaambia inuka wanainuka, ukiwaambia kaa, wanakaa, ukiwaambia kimbia, wanakimbia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii alipokuwa Mheshimiwa mama Zakia Meghji alikuja kuwaangalia, yeye ni shahidi aliwaona hao boko, hilo la kwanza. Lakini la pili, kuna ule urithi wa dunia, magofu ya Waarabu Kilwa

*(Kilwa Ruins)* yapo Mkoa wa Lindi, Kilwa. Hiyo sehemu ya utalii. Halafu kuna *beach* nyeupe, *white sand, beach* hiyo hutembelewa na hao *divers of the world*, wanatembelea, katika kutembea kwao kuzunguka dunia lazima wafike *beach* ya Lindi, inaitwa *Mitema Beach* ni *white sand*. Hizo ni shughuli za utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hayo tu kuna *Makonde Plateau*, pia kuna mapango makubwa kati ya mapango yale 21 ya Tanzania, pango la kwanza kubwa lipo katika Mkoa wa Lindi, Kilwa pango kubwa kabisa. Hilo wamezungumza kwamba litawekwa katika mpango ule wa *wonders of the world,* kwa hiyo lipo Kilwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *skeleton* ya mjusi mmoja anaitwa *dinosaur,* mjusi mkubwa sana. Mjusi huyo yupo Kilwa, Lindi Vijijini, *skeleton* zake zimechukuliwa zimepelekwa kwenye *zoo* ya Ujerumani mpaka sasa yupo kule, pale imebaki mikia, miguu, lakini mjusi huyu wamempeleka Ujerumani na Wajerumani wanafanya shughuli za utalii kupitia kwa mjusi wetu kutoka Mkoa wa Lindi anaitwa *dinosaur.* Kwa hiyo, mjusi huyo anaweza kurudishwa Tanzania akajengewa *zoo* katika Tanzania kwa nini akae Ujerumani, akae kwetu Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si hayo tu niliyotaja hapo juu kuna kiwanja cha ndege katika Mkoa wa Lindi, kina *runway* sita kilichokuwa kinatumika wakati wa Vita ya Pili ya Dunia. Ni uwanja wa ndege safi ambao umeshindiliwa, aina yoyote ya ndege inaweza kutua pale, hiyo ni Lindi. Si hilo tu, kuna eneo la Kilwa ambalo lilikuwa linatumika zamani wakati wa Vita ya Majimaji, kuna huyu Kinjekitile, ipo Kipatimu, watu wanaweza kuangalia pale wakaona, wakafaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si hilo tu kuna *Selous Game Reserve* ipo Liwale Mkoa wa Lindi, haya ni masuala ya utalii tu. Sasa tukiachia masuala hayo, tukija katika sehemu ya kilimo ambayo ameizungumzia katika ukurasa wa 13, kuna korosho, korosho zinatumika Amerika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Amerika wanaokula korosho au kutafuna korosho ni wale matajiri. Hivi hivi mtu wa kawaida huwezi kutafuna korosho, kwa hiyo, korosho nyingi na ufuta vinapatikana katika Mkoa wa Lindi. Sasa hivi tumewapanga wananchi, vijana kabisa, vijana kumi, kumi, kila kijana ni ekari kumi anapanda korosho mpya ili kuendeleza zao la korosho, tumeanza na mpango wetu wenyewe. Kwa hiyo, katika kilimo utakuta korosho na ufuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye uvuvi bahari ya Hindi maji makubwa hupita Mkoa wa Lindi, ukitokea Msumbiji kwenda huku Kenya ipo katikati. Kwa hiyo, utakuta samaki wale wakubwa wakubwa wapo katika Mkoa wa Lindi kwa sababu ni katikati ya bahari, huwezi kwenda Dar es Salaam bila kupitia Lindi pembeni kwenye bahari kuu.

Mheshimiwa Naibu spika, kwa hiyo, hii bahari kuu ina samaki wa kutosha kabisa ambao wanaweza kuvuliwa. Baada ya *operation* ile ya uvuvi haramu ambayo ilifanyika mwaka 2000 baada ya kuwakamata wale wavuvi haramu wa kutumia mabomu, sasa hivi

samaki wanapatikana wengi na wakubwa, kwa hiyo, ukiingizwa mpango huu tunaweza kupata manufaa makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo napenda kuunga hoja hii mkono na ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. SAMEER ISMAIL LOTTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nashukuru kupewa nafasi kuchangia hotuba hii inayohusu *SEZ.* Lakini nianze kwa pongezi. Wengi nimeshawapongeza labda niwapongeze wale ambao Chama cha Mapinduzi kimewateua kuwakilisha katika Bunge la Afrika Mashariki. Naomba watuwakilishe vyema wakifika huko, najua watapita hakuna Upinzani. *(Makofi)*

Pia nipongeze kundi la watu fulani ambalo ndio linatufikisha hapa sisi Wabunge wa CCM kuwepo hapa. Nao ni wana Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa. Nawapongeza sana. Mkifika kule Chimwaga msitusahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *SEZ* kipengele kinasema kwamba wawekezaji wataruhusiwa kuja na wataalamu angalau watano na wanaweza kuongeza ikibidi kama watafuata kanuni za Uhamiaji. Hatujazungumzia, nafikiri kuna kipengele kinasema kwamba tutaajiri au watapata ajira wananchi wetu angalau 50,000. Lakini hatujatangaziwa au kuelezwa kwamba hao 50,000 watapatikana vipi? Hakuna kipengele kinachosema kwamba Watanzania wangapi wataajiriwa. Kwa kweli zitapishana wengine wadogo, lakini kuwe na asilimia ijulikanayo kwamba asilimia 75 au 85 ya Watanzania wataajiriwa pale. Hilo nafikiri pia litasaidia sana katika kuhakikisha ajira za Watanzania.

Pili, ni *SEZ* Vijijini. Vijijini pia tunahitaji hii *Special Economic Zones* zisiwe tu katika maeneo ya miji ambapo miundombinu kweli imekamilika lakini vijijini kama walivyoongea wenzangu hapa pia tunahitaji mambo hayo. Kwa mfano, nitazungumzia kwangu Tarafa ya Mkuyuni tunataka mwekezaji wa kusindika matunda awe kama anaweza kukidhi mahitaji yale basi apewe ile *priority* na yeye ahusishwe katika hilo. Kama Tarafa ya Ngerengere tuna *poultry farms, cattle farms* waje wawekeze watafute ng’ombe wa *hybrid* wawekeze pale tuweze kushirikiana nao na waweze kuvuna, nyama ya ng’ombe, ngozi na kadhalika. Tuwe na *Ostrich farms* zile haziwezi kuwekwa mijini kwa sababu mbuni anahitaji mazingira ya pori pori. Lakini zaidi pia tunataka *crocodile farms,* sasa hivi mamba wana soko zuri sana lakini wanataka mito na mabwawa. Kwa hiyo, tuangalie vitu kama hivi kama tunaweza kuvi-*incorporate* na vikawa huko vijijini kwetu.

La tatu, nataka kuongelea kwamba pamoja na kusema kwamba tuwe na waajiriwa Watanzania angalau asilimia 70, 80 lakini vile vile katika Wakurugenzi wa Kampuni hizi angalau mmoja au wawili wawe Watanzania ili aweze kutetea si mambo ya uchumi tu lakini kuwe na uzalendo fulani kwamba kuna wakati wanaweza kufanya maamuzi yakawa si sahihi kwa ajili ya Tanzania basi yule akawa anatetea. Lakini mbali na hapo awe ndio mtu ambaye sisi tunaweza kumdhibiti wakiboronga hawa watu. Kwa hiyo,

tunahitaji angalau kuwa na Mtanzania mmoja ama wawili katika nafasi ya Ukurugenzi katika hizo Kampuni zao kwenye *economic zones* hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni mikataba. Ningeomba mikataba yao iliridhiwe na Bunge. Nashukuru na naunga mkono hoja ambayo naamini itarekebishwa kama nilivyopendekeza kwa maslahi ya nchi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia hoja hii. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali kwa kuleta hoja hii nzuri ambayo ndiyo tunajadili sasa. Nawapa hongera sana. *(Makofi)*

Nianze kwa kuchangia muundo wa hii *Export Processing Zone* pamoja na *Specials Economic Zones.* Tukianza na mamlaka unaweza kuona kwamba Mwenyekiti wake atakuwa ni Mheshimiwa Rais, wajumbe wake watakuwa ni 18, wawili tu ndio watakuwa ni wafanyabiashara, wengine wote ni Mawaziri pamoja na Mkurugenzi ambaye atateuliwa. Sasa kwenye *authority* kama vile wewe mtu mmoja *Executive Director* uende ukaongee na *authority* ambaye anaongoza Mheshimiwa Rais na wengine wote 16 ni Mawaziri hakuna kitu ambacho unaweza kusema, wewe utakuwa unasikiliza yale wanayosema wao, wewe utakuwa unasema ndio mzee, ndio mzee, ndio mzee. Mimi naomba muundo huo ubadilishwe ili waingize *Private Sector* kule ndani maana hii ndiyo biashara. Sasa Serikali haifanyi biashara na tumekubali kwamba Serikali haifanyi biashara tubadilishe huu muundo tuweke wafanyabiashara kwenye hii authority wawe wengi zaidi. Nashauri Serikali ifanye hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine hata ukiangalia kwenye Kamati ile ya *Special Economic Zone.* Kamati ile Mwenyekiti wake atakuwa ni *Chief Secretary* wengine wote 16 ni Makatibu Wakuu ukiongeza na Kamishna wa Ardhi, Kamishna wa *Labour, Director* wa *Immigration* na Kamishna wa *Customs,* wote hao ni watu wa Serikali. Sisi tulishakubaliana kwamba Serikali iondokane na biashara, ibaki kwenye ushauri. Mimi nashauri vile vile Serikali katika Kamati hii iongeze wafanyabiashara zaidi. *(Makofi)*

Nikiingia sasa kwenye *real terms* ya ku-*implement* huu muundo wa *Special Economic Zones.* Nia na madhumuni ya kuanzisha hii *Special Economic Zones* ni kuongeza uzalishaji ndani ya nchi na kuhamasisha uuzaji wa bidhaa nje ya nchi pamoja na kuongeza ajira kwa Watanzania na kukuza Pato la Taifa. Sasa yote haya ukiyaunganisha lazima kuwe na muundo mzuri na wafanyakazi wazuri na maeneo yaliyotengwa yawe ya vivutio na watu ambao wamekwishawekeza tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nibobee kwenye eneo la utalii. *Special Economic Zones* wamesema wataanzisha *Special Tourist Parks. Special Tourist Parks* zinahitaji wawekezaji. Mimi nashauri Serikali iwaangalie kwanza wale wawekezaji wa ndani, iangalie Watanzania na wakati wa kuwekeza hata wanapokuja watu wa nje, je, ni asilimia ngapi wanapaswa kuwekeza. Ni asilimia mia moja ama tuwe na Watanzania ambao watakuwa *partners,* tuwe na *Tanzania Associates* ili uchumi wa nchi wetu tuweze kumiliki sisi Watanzania kwanza. Sera ya Ardhi inasema mgeni hawezi akamiliki ardhi.

Sasa kama mgeni hawezi kumiliki ardhi hizo hoteli wazojenga nani atazimiliki. Tunaweza kuwabana kwa njia hiyo. Amekuja mwekezaji tunamwambia lakini sisi sera yetu ya ardhi inasema huwezi kumiliki ardhi, kwa hiyo, huyu mwenye ardhi lazima uwe mshirika naye. Kwa hiyo, tayari ataingia Mtanzania pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye eneo la utalii Kilimanjaro. Kilimanjaro inaweza ikawa ndio *Special Economic Zone* kwa utalii kwa sababu zifuatazo, Kilimanjaro tayari kuna miundombinu kwa ajili ya utalii. Mlima wa Kilimanjaro umetangazwa dunia nzima. Mlima wa Kilimanjaro kule vijijini kuna hoteli sasa hivi zisizopungua 10 mojawapo ya hoteli ambayo iko kule ni ya kwangu mimi Kimaro hapa. Sisi tunatangaza utalii wa nje na wa ndani nawakaribisha Wabunge mfike kwenye hoteli Marangu Nakara kule kama watalii wa ndani ili muwe mfano, mpeleke na kule kwenu. Nawakaribisha sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watalii waliotembelea Mlima wa Kilimanjaro kipindi cha mwaka 2004/2005 ni watalii 31,665 hao wametoka nje watalii wa ndani walikuwa 1,472. *Expatriates* walikuwa 118 na jumla ni 33,255. Pato waliloingiza Serikalini kutokana na kutembea ndani ya Mlima Kilimanjajro ni dola milioni 14. Kwa fedha ya Kitanzania ukichukua dola shilingi 1,000 ni bilioni 14 kutoka kwenye utalii wa Mlima wa Kilimanjaro. Hiyo fedha imeingia Serikalini. Tukifaanya Kilimanjaro ikawa kama *Special Economic Zone* ya *Tourism* pato linalopatikana litaanzisha *another Special Economic Zone* ya *Tourism* kwenye maeneo mengine ya Tanzania. Yale maeneo ambayo yamekwisha kubobea kwanza tuhakikishe kwamba lile pato linalopatikana pale linakuwa ni halisi na linachukuliwa linakwenda kuanzisha sehemu nyingine. Utalii ni sawa sawa na uzalishaji kwa ajili ya kuuza nje. Kwa sababu watalii wanachukua dola wanaleta Tanzania. Tunapozalisha bidhaa tunasema tunazalisha kwa *export* una-*export* ili uweze kupata fedha irudi Tanzania. Utalii unauza kile kivutio kwa maneno mazuri, kwa kutangaza wao wanakuja wanaleta fedha kazi yetu ni kuhakikisha kwamba ile fedha wanayoleta ndiyo ile fedha halali kwa ajili ya vile vivutio wanavyokuja kuona.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi hii *package tourism* ambayo inatufanya sisi tunategemea *tour operators* walioko Ulaya, wale *tour operators* walioko Ulaya wanacholeta Tanzania ni robo tu ya kile wanachopata. Mfano halisi wewe ukiangalia Zanzibar kuna msululu wa hoteli kwenye zile fukwe, ndege zinakwenda kila siku, lakini wenye hoteli hizo wako Ulaya, wako Italy. Fedha zinabaki Ulaya au Italy watalii wanapokuja hapa wanakula tu chakula lakini robo tatu ya yale mapato yanabaki Ulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa inapoanzishwa *Special Economic Zone* kazi yake ni ku-*monitor* yale mapato. Kuwe na mfumo wa ku-*monitor* yale kwamba mtalii alipe kwa kutumia kompyuta, kwa kutumia *internet,* fedha yote ije Tanzania kama ni kurudi kuna mpangilio wa kurudi aidha, kwa kutumia *shares* na kadhalika warudishe ile *share* yao, lakini tuhakikishe kwamba fedha yote inaingia Tanzania kwanza halafu ndiyo irudi Ulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali sasa kwa sababu tayari kule Kilimanjaro tumeshaanza huo mfumo na hoteli tunazo, kule vijijini nimesema kuna hoteli

zaidi ya kumi. Wataalam sasa hawa *Special Economic Zones* waanzie pale ili kudhibiti yale mapato.

Kwanza wenye hoteli fedha zile zifike kwenye hoteli wakati watalii wanakuja. Pili wale wafanyakazi ambao wanawapeleka wale watalii Mlimani kwa *average* ya wale watalii 33,255 kwa kila mtalii *minimum* anachukua waongoza watalii watatu. Kwa hiyo, wamekuwa *employed* vijana zaidi ya laki moja. Sasa ajira ya vijana laki moja na wakilipwa vizuri fedha ile imeingia Tanzania itahama itakwenda hata mikoa mingine. Kwa sababu ni Mtanzania anayepata, hatujali sisi atakayechukua ile fedha ni Omar, Juma, Kimaro au ni nani lakini fedha hiyo iwe imeingia Tanzania itasambaa Tanzania nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ningependa nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuzungumza kwa mara ya kwanza katika Bunge hili Tukufu.

Pili, kwa maana hiyo basi, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi na Watanzania na kwa maana hiyo kumpa nguvu ya kuweza kutekeleza ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Pia ningependa kumpongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, ambaye alikuwa mgombea mwenza. Napenda kuchukua nafasi hii pia kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuteuliwa na baadaye kuthibitishwa na Bunge hili na kuwa Waziri wetu Mkuu. Ni mchapakazi, ninamfahamu siku nyingi sana. Napenda kuchukua nafasi hii pia kuwapongeza Mawaziri, Naibu Mawaziri wameanza vizuri sana ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Pia ningependa kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimwa Spika kwa kuchaguliwa kwanza na wapiga kura wake na pili, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Spika wetu katika Bunge hili Tukufu. Nikupongeze wewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika na kwa umakini wako wa kuongoza vikao hivi vya Bunge. Nakupongeza sana. *(Makofi)*

Napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa kuchaguliwa tena kwa kura nyingi kabisa katika Majimbo yenu na ninyi pia mmepata nguvu ya kutekeleza ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Ningependa kuchukua nafasi hii kwa moyo wa dhati kabisa kuwapongeza wapiga kura wangu wa jimbo la Lulindi kwa kunipa kura nyingi na kuwa Mbunge wao kwa kipindi cha miaka 5 ijayo. Nasema ahsanteni sana na ninaahidi kuwatumikia kwa nguvu zangu zote. Kama nilivyosema nilipokuwa nakutana nao kwamba sintowaangusha hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanza kuchangia Muswada huu naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kaka yangu Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa. Kwanza kwa maana ya Muswada wenyewe na pili kwa kuuweka Mkoa wa Mtwara katika orodha ya mwanzo kabisa wa maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa ya Kusini imebeba mzigo mkubwa kwa Tanzania wote tunafahamu historia yetu ni Mikoa ambayo iliathirika kwa mapambano ya kudai Uhuru katika nchi ya Msumbiji. Kulikuwa hakuna mawasiliano baadhi yetu tulikuwa hatutaki kwenda Kusini, Kusini kukawa *isolated,* wengine waliweza hata kuacha kazi kwa sababu tu wamepata uhamisho wa kwenda Kusini. Leo ni moja kati ya maeneo ya *Special Economic Zone.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kusini kuna mali nyingi sana. Kuna dhahabu, kuna vito vingine, kuna misitu mikubwa, kuna mazao ya kudumu kama korosho na mazao mengine chungu nzima. Kwa hiyo, uamuzi huu umekuja wakati wake hasa kwa watu wa Mikoa ya Kusini. Katika jimbo langu la Lulindi ni moja kati ya maeneo tunayozalisha korosho kwa wingi na hii dhahabu niliyoitaja inatoka katika moja ya kijiji changu katika jimbo la Lulindi kinaitwa Mchauru.

Naomba basi pamoja na uamuzi huu Mheshimiwa Waziri weka utaratibu mzuri tu wa *geological survey* katika Mikoa ya Kusini ambayo itatuwezesha kufahamu na kugundua madini mbalimbali. Kwa hiyo basi, ninachoomba katika maandalizi ya hii *Special Economic Zone* suala la miundombinu ni la msingi sana. Mimi nimekaa China miaka mitano. Nilikwenda kule mwaka 1993 mpaka 1998 kipindi kile ndiyo China iko katika heka heka kubwa ya kuendesha *Special Economic Zone.* Walichofanya wao hawakubababaisha hata kidogo katika maandalizi ya miundombinu, barabara, umeme, simu na mengine yote ambayo yalisaidia kuwavutia wawekezaji. Naomba basi kwa kuwa katika Muswada huu China imetajwa maana yake ni kwamba wanafahamu wenzetu hawa walifanya nini. Naomba katika eneo hilo kwa kweli tusilifanyie ajizi hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kulifanya jambo hili liwe na ufanisi wa kiwango cha hali ya juu, mwekezaji yeyote atakayekuja katika nchi yetu tumweleze kinagaubaga kwamba atumie malighafi ya kwetu Tanzania pale inapoonekana kuna ulazima wa kufanya hivyo. Wasije wakatuletea utaratibu wa kuchukua malighafi kutoka kwao wakati sisi hapa tunayo. Yale ambayo hatuna basi wanaweza kuchukua kutoka huko kwao wanakotoka.Hii itasaidia sana katika kupunguza umaskini kwa watu wetu watakaokuwa wanalima malighafi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine mimi nimekaa Ikulu pale nikiwa Msaidizi wa Rais, Siasa. Moja kati ya mambo ambayo nimekuwa nikiyafanya ni kusikiliza matatizo ya wananchi. Nilikuwa na kliniki kila Jumatano kuanzia saa mbili asubuhi mpaka saa nne usiku. Wengi waliokuja kunung'unika katika siku ile ni wafanyakazi wanaoajiriwa kienyeji katika baadhi ya viwanda vyetu na vingine ni hivi hivi vya wawekezaji. Hawana utaratibu mzuri wa kuajiri, wanaachishwa kazi bila ya utaratibu, ninachoomba basi katika utaratibu huu wa *Special Economic Zone* haya

yasiwepo. Kuwe na usimamizi mzuri kwa vijana wetu watakaoajiriwa wajue kweli tumeajiriwa ili azma yetu ya kutengeneza ajira milioni moja ionekane, ikamilike. Si vizuri hata kidogo Mtanzania katika nchi yake kwa utaratibu wake, kwa sheria yake asiajiriwe katika utaratibu ambao utampa matumaini ya kuishi vizuri. Naomba kwa hili Mheshimiwa Waziri akishirikiana na Wizara ya Kazi ijitahidi kuhakikisha kwamba vijana wetu watakaoajiriwa, waajiriwe kwa utaratibu kwa sheria zetu za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko tabia ambazo lazima sasa hivi tuanze kuziacha. Baadhi ya watu wetu si waaminifu. Wanapoajiriwa katika maeneo haya wanapenda kudokoa dokoa tutawakatisha tamaa wawekezaji. Lazima tuwe na utaratibu wa kuwaelimisha kwamba wanakwenda pale kwanza kupata ajira wao wenyewe, wanakwenda pale kulinda heshima yetu Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba kutoa ushauri. Pametajwa hapa nchi ambazo wameanza kufanya hii *Special Economic Zones* naomba basi Mheshimiwa Waziri kaka yangu, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa utazame uwezekano wa kuwapeleka baadhi ya Waheshimiwa Wabunge katika nchi hizi wakaone kwa macho yao hasa Jamhuri ya Watu wa China ambapo Dengsh Oping aliianzisha hii. Singapore kwa Lee Kwayuu wakaone pale na waje Malasyia kwa Maathiri Mohamed waone pale, wakija huku wawashawishi Watanzania kwamba kweli mpango huu wa *Special Economic Zone* utatuletea manufaa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa ningependa kumshukuru Waziri ambaye ameandaa haya mambo naona kwamba kwa kweli imetumika akili na muda katika kufanya maandalizi haya. Ningependa kumpongeza Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa kwa sababu inaonekana kila mara anapenda kuwa katika Baraza la Mawaziri katika kila awamu, kwa hiyo, inaonekana ni mtu mwenye uwezo mkubwa. *(Makofi)*

Mimi hii Miswada naiona ni mizuri isipokuwa ningependa kutoa mapendekezo kidogo na ushauri kwamba kwa Waziri kukiri ya kwamba tumeachwa nyuma miaka 40 nampongeza sana kwa sababu amezungumzia jambo ambalo ni la kweli kabisa. Kwa hiyo, ina maana kwamba inabidi tuanze kukimbia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hizo juhudi za kujaribu kukimbia ili tukabiliane na hali hii ya utandawazi ambayo kimsingi ni kwamba tunakabiliana na mfumo wa Ubepari na kuna mchangiaji mmoja amesema kwamba Ubepari kwa *nature* yake hauna huruma, kwa hiyo, tunakabiliwa na hatari kubwa sana. Nadhani mahali tulipokosea wakati tukiwa na siasa ya ujamaa na kujitegemea. Ni pale ambapo hatukufanya uchambuzi sahihi wa kisayansi kuhusiana na jinsi mfumo huu unavyoendelea. Ndiyo maana wenzetu wa China, Korea na Vietnam wameweza kutumia falsafa hiyo hiyo kuweza kujiwekea misingi na sasa hivi wako katika ushindani mzuri na nchi za kibepari duniani.

Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake amezungumzia kuhusu *middle income status* ambayo inatakiwa kujengwa kufikia mwaka 2025. Hapa anaongelea tabaka ambalo litakuwa linauwezo wa kiuchumi wa kibepari ambao unaweza kufanya tu na wazawa au wananchi wazalendo ambao wanaendesha uchumi wa kibepari kwa njia inayofaa. Kwa hiyo, ina maana kwamba ili tuweze kuwa hivyo ni lazima kwa makusidi mazima tuweze kuelekeza uchumi wetu katika kuwasaidia wananchi ambao ni wazalendo ili waweze kuunda hilo tabaka ambalo hilo tabaka litakuwa na manufaa makubwa kwa sababu itakuwa haitoroshi mali kutoka nchini kupeleka nje, watakuwa wanajenga hapa hapa.

Kwa hiyo, hili ni suala la msingi kabisa kuweza kuwa na hilo tabaka na likasaidiwa. Ndiyo maana naona mkazo mkubwa ungewekwa katika kuwasaidia wananchi wazalendo ambao wana nia ya kufanya biashara ambao kwa sasa hivi hawana mitaji na hawana nyezo. Kwa hiyo, kwa makusudi ielekeze katika kuwasaidia Watanzania wazalendo ili waweze kushiriki katika uchumi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika kingine ambacho ningependa kuongelea ni kwamba katika hizi S*pecial Economic Zones*. Mfumo wa ubepari kwa kawaida huwa una vitu vinaitwa *imbalances* yaani unakuwa hauna uwiano katika maendeleo yake na nimeona hiyo dosari katika hizi *Special Economic Zones* tunazojaribu kutengeneza hapa kwamba kumekuwa na mkazo zaidi katika kuendeleza maeneo ya Dar es Salaam na Zanzibar na sehemu nyingine ambazo tayari zimeshakuwa na misingi mizuri ya miundombinu. Lakini pia ningependa kutahadharisha kwamba hizi *imbalances* hazitakuwa na afya nzuri kisiasa kwa baadae. Kwa sababu dalili zenyewe mnaziona. Leo hii Bunge letu unaona kila Mbunge akisimama anaongelea ukanda wa kwao na ana haki ya kufanya hivyo kwa sababu sasa hivi kila watu wanaanza kujiuliza kwamba tuna nini, mchango wetu ni nini na mgao wetu utakuwa ni upi?

Kwa misingi hiyo hiyo ningependa kuzungumzia ukanda wetu wa Kanda ya Ziwa hususan Mkoa wa Mara, kwamba Mkoa wa Mara tumetengwa sana katika maendeleo ya kuichumi ya nchi hii hasa maendeleo ya viwanda. Jimbo ninalotoka mimi ni Jimbo ambalo lina mchango mkubwa sana wa kiuchumi katika nchi hii. Lakini hatuna hata kiwanda kimoja. Kwa hiyo, hii inaonekana ya kwamba kidogo Waheshimiwa Mawaziri mnatusahau kwa sababu ukiangilia mchango wetu wa mapato nchini, kwa mfano ukichukulia lile *gate* la Sirari ambalo mimi naita bandari kubwa pengine zaidi kuliko maeneo mengine kwa sababu ya mali inayopita pale inahudumia nchi sita za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Kongo na Tanzania yenyewe, inaingiza *revenue* kubwa sana Serikalini. Lakini hakuna *percentage* yoyote inayobali ku-*develop* lile eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwamba kuna barabara iliyojengwa kwa msaada wa *European Union* ambayo inatoka Mombasa hadi Mwanza, ndiyo ambayo imetusaidia sana pale kwa upande wa miundombinu. Vinginevyo barabra zingine za vijijini na za Mikoani hazipo ni mbovu kabisa. Kwa mfano, barabara imeweza kujengwa kutoka Arusha hadi *Ngorongoro Gate* lami ikaishia pale. Lakini ile barabara ingeweza kuunganisha moja kwa moja mpaka Kanda ya Ziwa ingeboresha sana uchumi wa eneo lile kwa sababu ni eneo ambao ni la utalii na biashara. Hili ningependa mlifikirie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho ningezungumzia katika hizi S*pecial Tourist Parks* ambazo zimezungumziwa, mtakapo kuwa manafikiria kuhusu kuweka *Tourist Centers* mtufikirie na sisi kule Mara hasa Tarime na Serengeti kwa sababu mkisikia hata hilo jina Serengeti ipo katika Wilaya ya Serengeti na imepakana vizuri sana na Tarime, Mkoani Mara. Lakini shughuli zote za kitalii zinafanyika Arusha na Kilimanjoro. Ina maana ya kwamba sisi hatuhusiki kabisa na uchumi wa utalii ambao unaendelea katika mambo haya na ukiangalia kwamba sasa hivi barabara kubwa ambayo ingeweza kuingiza watalii wengi, barabara ya kuingilia Sirari ambayo nafikiri kwa kiwango kikubwa sasa hata kule Namanga haitufikii lakini hakuna watalii wanaopita pale. Kwa hiyo, hii ni *imbalance* moja ambayo ningeomba muisaidie kuirekebisha ili wananchi wa eneo lile nao waweze kushiriki katika uchumi wa nchi kwa mipango hii ambayo Serikali ya sasa inayo.

Kingine ambacho pia ningependa kuwakumbusha ni kwamba Wilaya kama ya Tarime imekuwa na mchango mkubwa sana katika nchi hii hasa kwa upande wa ulinza na usalama. Nadhani tunapozungumzia kuhusu amani na utulivu tukumbuke vile vile ya kwamba tumechangia nguvu kazi kubwa sana ndani ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania ambalo watani wetu wanasema ni Jeshi la Wakurya Tangu Zamani (JWTZ) na inaonyesha ya kwamba sisi ni watu ambao tuna utii na tuna uaminifu na ndiyo maana hata Serikali inapenda kutupa hayo majukumu. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, mkumbuke ya kwamba lile eneo vile vile linahitaji kukumbukwa katika maendeleo ya nchi ili na sisi vile vile tuone ya kwamba ni Watanzania kama wengine. Kwa hiyo, najumuika na ndugu zangu wengine wa Kusini, ambao pia wanakilio chao hapa kila mara wanaposimama. Mimi nakubali kwamba kweli hata wao wanafaa waangaliwe na wale wa Magharibi ili nchi yetu iweze kwenda kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ndiyo huo naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ambayo inazungumzwa tangu mchana wa leo. Lakini kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako hili Tukufu, napenda kwanza nitoe pongezi kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi ambazo alipata katika Uchaguzi Mkuu. Napenda pia nimpongeze Waziri Mkuu kwa kuchaguliwa na wananchi wake wa Jimbo la Monduli na pia kwa kuteuliwa na Rais kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nimpongeze Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa na wananchi wa Jimbo lake la Urambo Mashariki na pia kwa kuchaguliwa na Wabunge wote kuwa Spika wa Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Napenda nikupongeze Naibu Spika, kwa wananchi wa Njombe kuihakikishia dunia kwamba wanawake wanaweza na kwa kufanya hivyo nasi Wabange tumeithibitishia dunia kwamba unaweza kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwapongeze Mawaziri na Manaibu Mawaziri kwa kuteuliwa kwao, niwapongeze pia Wabunge wenzangu kwa kupita kwenye kinyang'anyiro lakini sijawasahau wanawake wa Mkoa wa Dodoma kwa kunichagua na kuniwezesha kuwa mwakilishi wao katika Bunge hili, nawaahidi kwamba nitawapa ushirikiano mkubwa katika kuleta maendeleo ya Mkoa wa Dodoma napia kwa taifa letu.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Dr. Juma Ngasongwa, kwa mada yake nzuri ambayo inaendelea kujadiliwa kwa kuonyesha mwelekeo wa Serikali kwa upande wa uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia mada hii ya Serikali pia kwa kuona umuhimu wa kuanzisha maeneo maalum kwa uwekezaji rasilimali katika nchi yetu. Naamini kwa uwekezeji huu Watanzania wengi tutaondokana na umaskini. Lakini jambo ambalo napenda kuzungumzia ni kuhusu Mkoa wa Dodoma. Naamini Serikali ilipofanya uamuzi wa kuufanya Mkoa wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya Serikali waliangalia mambo mengi. Waliangalia hali ya hewa, miundombinu na mambo mengi ambayo yanaweze yakasaidia Mkoa wa Dodoma uwe Mkoa unaofaa kuwa Makao Makuu ya Serikali.

Lakini kitu ambacho nimekiona hapa katika mada ya Serikali ni kwamba Mkoa wa Dodoma haupo katika ile Mikoa ambayo ipo kwenye mpango wa *SEZ*. Naamini kama kweli Serikali ina mpango wa kuhamia Dodoma. Mkoa wa Dodoma ungekuwa Mkoa wa kwanza kufikiriwa na kama kweli tunataka kuhamia Dodoma basi Mkoa wa Dodoma ungewekewa vivutio vingi kwa wawekezaji ili wawekezaji waje kwa wingi na Mkoa uwe na shughuli nyingi za uwekezaji na Serikali iweze kuhamia kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba kama miundombinu ya barabara, barabara ya lami tunayo ya kutoka Dar es Salaam na Serikali inajenga barabara ya kwenda Singida na katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 barabara ya kutoka Arusha kupitia Dodoma kwenda Iringa itajengwa. Kwa hiyo, mimi naamini kabisa kwamba Mkoa wa Dodoma unafaa kuwa kwenye mpango wa Serikali wa *SEZ. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea kuhusu wale ambao maeneo yao yatachukuliwa kwa mpango wa *SEZ*. Serikali haikuonyesha kwamba wale ambao maeneo yatachukuliwa je, watafidiwa? Maana katika hotuba ya Waziri haikuonyesha kwamba wale ambao maeneo yao yatachukuliwa aidha, nyumba zao zinaweza zikabomolewa au mashamba yao yakachukuliwa au maeneo ya miradi yao yakachukuliwa kwa mpango huo wa uwekezaji. Je watafidiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu kukaguliwa kwa mizigo itakayoingia nchini kukaguliwa katika maeneo ya *SEZ* husika. Sasa wasiwasi wangu ni kwamba Serikali imeweka udhibiti gani katika maeneo yale ambayo mizigo itakaguliwa ushuru wa forodha katika maeneo husika. Naamini kwamba kama Serikali haitaweka udhibiti wa uhakika hawa wawekezaji watapata mwanya mkubwa wa kukwepa kodi. Kwa hiyo, naiomba Serikali iweke udhibiti mzuri au waweke utaratibu mzuri tu kwa maofisa wa forodha kuhakikisha kwamba ile mizigo haichelewi kutoka bandarini ikaguliwe mara moja na iende maeneo yanayohusika kuliko kukaguliwa katika maeneo ya *SEZ.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa mpango mzuri wa kuhakikisha kwamba wale wanaokuja kuwekeza, wataalam wanaoingia hawazidi watano. Lakini wenzetu wanaotoka nje ya nchi wengi wao ni wajanja kama Serikali ina nia kweli ya kudhibiti hali hii kwamba wageni wanaoingia wasizidi watano basi udhibiti huo uwepo. Kwa sasa tunaona katika hoteli zetu ambazo wageni wamewekeza hata wahudumu ni watu wa kutoka nje, *receptionist* ni watu wa kutoka nje na hata wapishi ni watu wa kutoka nje. Lakini kama Serikali ina nia ya kudhibiti hali hii basi udhibiti uwepo kama tunavyoambiwa hapa kwamba wataalam watakaoingia wasizidi watano na mimi naungana na Mbunge mwenzangu mmoja aliyesema kwamba katika uongozi angalau kati ya wale watano au kama uongozi una watu sita basi angalau nusu kwa nusu. Watatu wawe wageni na watatu wawe Watanzania ili kuwapa Watanzania nafasi ya kuitumikia nchi yao kupitia kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono hajo ya Serikali. *(Makofi)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi nichukue nafasi kumpongeza mtoa hoja yeye binafsi Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake ambao wameweza kufanya kazi ambayo inakidhi masuala ya kasi mpya, nguvu mpya na ari mpya kwa zindua vitu vipya. Hii maana yake *new things, new ideas, innovativeness.* Sasa Wizara hii na Waziri *in particular* ameweza kuwa *innovative* kufikiria vitu tofauti ambavyo vinaweza kutuletea maendeleo katika nchi hii. Kwa kweli napenda kuwashukuru sana, kuwapongeza na kuwasifu kwa kazi hii nzuri.

Nasema ni kazi nzuri kwa sababu inazingatia vivutio, rasilimali, kiingereza tunaita *opportunities* ambazo ziko kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu na ambayo inafanana kwenye kilimo tunazungumzia mambo ya *agro ecological zones.* Hii *zonation* inayozungumziwa hapa inafuata utaratibu na utaalam huo ambao ni mzuri sana ambacho amekififikiria vizuri sana na ni *idea* ambayo naiunga mkono vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kwa namna mbili, moja ningependa kwenda kwenye ukurasa wa 27 kwenye kifungu cha tisa ambacho kinazungumzia kuhusu *objectives* za *Special Economic Zone*. Pale inazungumzia kuhusu *objectives* ambazo zitafuatwa. *In other way* ni *criteria* zitakazo tumika kuchagua *SEZ.*

Kuna vitu kama *productivity, competitiveness, economic growth, export promotion and employment generation for poverty eradication*. Hapa nilikuwa nataka kuchangia, kuongeza, kupendekeza ili aidha, tunaongeza vitu vifuatavyo:-

Moja naamini kuwa ili programu iwe *sustainable on the short and long term,* lazima iwe *sustainable* na nitaeleza tutaipatapataje hiyo *sustainability* ambayo kwa vile katika *zone* moja kuna kuwa na *activitie*s nyingi, kwa mfano kutakuwa na kilimo, ufugaji viwanda na kadhalika katika eneo moja. Tuna sheria ya mazingira na watu wa Wizara ya mazingira bila shaka wako hapa ambayo inataka *projects* zozote mpya ni lazima ziwe *subjected to environment impact assessment*. Inayopendekezwa ni programu sio *project*. Ni programu ambayo itakuwa na *activities* nyingi, kwa hiyo, ili ku-*compare zone* moja na *zone* nyingine kama zina mazingira yanayofanana basi unafanya kitu wanakiita *strategic environmental assessment* ambapo itawezesha pamoja na mambo na *sustainability issues* uangalie *environmental* na *social costs*.

Kwa hiyo, hizo zinaweza kuwa ni *additional criteria* za kulinganisha *zone* moja na nyingine ambazo tunafikiria labda zina *opportunities* sawa. Kwa hiyo, kwa kufanya *strategic environmental assessment* utaweza kuangalia mambo ya *productivity, sustainability, competitiveness etc,* lakini pamoja na *environmental and social costs*. Tutategemea *zone* itakayochaguliwa iwe na *least environmental cost*. Nilidhani nichangie kwenye hilo kwa sababu Muswada hauzungumzi kitu hicho cha *environment* na *program* kubwa kama hii ambayo itahusisha vitu vingi sana kwenye ardhi fulani ili kujihakikishia kwamba inakuwa *sustainable* lazima tuangalie vile vile *environmental and social issues*.

Baada ya kusema hayo, waswahili husema kwamba kama watu hawakutambui basi unaweza ukawasha mshumaa ukauweka juu ya meza na ukuwatangazia watu, jamani nipo hapa. Sasa na mimi nilitaka kujivutia kwangu, nizungumzie kuhusu eneo moja ambalo nafikiria linafaa na hili linaweza lika-*focus* au likachukua *center* ikawa Ludewa. Pale tuna *deposits* kubwa za chuma. Karibu hapo hapo kuna makaa ya mawe, ardhi hii inayozunguka pale na Mkoa mzima wa Iringa hasa eneo tunaloita NJOLUMA. NJOLUMA ni Njombe, Ludewa na Makete na sehemu za Mufindi kuna hali ya hewa nzuri sana. *It is very cool,* mvua kila mwaka tunapata, udongo una rutuba ya kutosha na kuna uwezekano wa kuzalisha zao lolote utakalofikiria. Ukianzia kwenye *cash crops* chai, kahawa na *pyrethrum* vyote utavikuta kule.

Lakini vile vile kuna uwezekano wa kuzalisha *petrol* kutokana na mahindi kwa sababu Mikoa ile minne *(the big four)* ni *giants* na ukichukua ukanda wote ule wa Nyanda za Juu kwamba wanaweza kutoa mahindi ya kuweza kuzalisha *petrol* ya kutosha. Sasa nilikuwa nafikiria vile vile kwamba kwa Wilaya zile za Njombe, Makete na Ludewa tulishafikilia kuhusu *industrialization* ya eneo hili kwa sababu ya *strategic location* lakini vile vile sababu ya uwezo wa maeneo haya na tulikuwa tunaangalia nitatumia neno la kiingereza *strategic location* ya Makambako kwamba Makambako pale ni kama *needle centre* sijui kiswahili chake ni nini. Kuna barabara inayokwenda Mbeya kuja Dar es Salaam, kwenda Songea vile vile kuna reli inayopita pale kutoka Dar es Salaam kwenda Mbeya hadi Zambia na karibu sasa tutakuwa na kiwanja cha ndege kinachojengwa Songwe, Mbeya.

Kwa hiyo, utakuta kwamba eneo hili ukiangalia *opportunities* zilizopo ziwe za kilimo, ziwe za madini au viwanda, *agro industry,* kutengeneza mafuta ya alizeti au kama nilivyosema kuzalisha mahindi kuweza kutoa petroli vyote hivyo kwa kweli vinawezekana. Ukichukua eneo dogo pale unaweza kufanya vitu vyote hivi, hata ukipanua zaidi ukaweka Mikoa ya Iringa, Rukwa, Mbeya na Ruvuma bado hilo unaweza ukalitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naona kwamba katika maeneo ambayo kwa kweli tunaweza tusiwe na wasiwasi kama tutayachagua, baada ya kuyalinganisha haya na kuona ipi ina nafasi kubwa kuliko sehemu nyingine mimi nahisi hili eneo ambalo linakuwa na *center* yake kweye Wilaya ya Ludewa kwenye chuma na Makaa ya Mawe na maeneo yanayozunguka ambako unaweza ukafanya kilimo, ufugaji kila kitu unachoweza kufikiria unaweza ukapata hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili linapakana na Ziwa Nyasa kwa hiyo, ukianza kuzungumzia mambo ya uvuvi, uvuvi unaweza ukauunganisha hapo pengine tunaweza tuka-*link* na suala la mwenzetu Mbunge wa Peramiho kwamba unaweza kuunganisha na *Mbamba bay* halafu ukaunganisha na *corridor* ya Mtwara kwenda kutokea Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mchango wangu ulikuwa ni huo na nitashukuru sana kama Wizara wataangalia masuala haya kwa utaratibu huo, naomba niunge mkono hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kukupongeze kwa kuchaguliwa kwako kuwa Naibu Spika wa kwanza mawanamke nakupongeza sana. Hii inaonyesha kwamba wanawake sasa tunapiga hatua, hata nchi nyingi zitakaposikia hakika watasema Watanzania sasa wamechangamka. *(Makofi)*

Pili nimpongeza Mheshimiwa Waziri kwa Muswada huu na niwapongeze wote wale ambao walikuwa kwenye hiyo Kamati ambayo iliandaa Muswaada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nikianza na suala la *Tanzanite,* Mererani. Naishukuru sana Serikali kwa kuliona hilo na kupitisha sheria hii ya kufanya eneo lile la *Tanzanite* kuwa *controlled area*. Lakini kuna tatizo moja, naomba pia Serikali iangalie tena upya kuhusu ile ada iliyowekwa ikiwa ni kiingilio cha shilingi 20,000 kuingia kwenye lile eneo. Itakuwa ni shida sana kwa mwananchi wa kawaida kuweza kulipa shilingi 20,000. Hii inaonyesha kwamba hata wale wachimbaji, wale ma-*brokers,* kuna wengine mtaji wao ni shilingi 20,000 na anatamani aende pale naye akanunue sasa sijui atalipa kiingilio au atakwenda kununua madini. Kwa hiyo, namwomba Waziri na Serikali kwa ujumla iangalie upya kiingilio hiki cha shilingi 20,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, nindelee tena kuangalia upande mwingine wa pili, kwa upande wa wachimbaji wadogo wadogo, hawa wachimbaji wadogo wadogo wanatakiwa pia nao waangaliwe. Aidha, kwa kukopeshwa zana za kuchimbia kwa sababu pia nao wanachimba sawa sawa na hawa wachimbaji wakubwa, lakini tu kinachopungua pale ni

zana za kuchimbia. Naomba pia Serikali iangalie kama wataweza kukopeshwa zana ili waweze pia kuchimba na kwa sababu pia uzalishaji wao utaleta faida kwa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuendelee tena kuangalia upande wa ukataji na kusanifu madini. Madini haya ya *Tanzanite* ukiangalia hayapatikani mahali pengine popote duniani na Muswada huu umelenga kujenga kiwanda kwa ajili ya kukata na kusanifu madini. Nashauri Serikali kama kiwanda kile kitajengwa, basi kijengwe katika eneo la machimbo kama kule Mererani mkoa wa Manyara kwa sababu pia na mkoa wetu ni mpya ili nao upate jina. Kikijengwa kiwanda pale, hata wageni wanaokuja wanajua kwamba wanafika Mererani, wilaya ya Simanjiro, mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mengi sana ya kuchangia ila ninaomba na ninarudia tena kuomba wachimbaji wadogo wadogo waangaliwe sana kwa sababu nao ni nguzo nao ni wachimbaji na wanapopata madini yale yanabakia hapa hapa nchini na faida inayopatikana aidha ni kuwekeza, wanawekeza hapa hapa nchini kwetu na ile faida haiendi nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali iangalie jinsi ya kuwasaidia na zaidi pia iangalie namna ya kudhibiti yale madini wakati yanapotoka ili Serikali nayo isipate hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naunga mkono Muswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ADAM K. A. MALIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu, awali ya yote naomba nichangie hoja hii kwa kutoa shukrani kama ifuatavyo:-

Kwanza, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sisi sote tuliopo humu ndani kuvuka katika vinyang'anyiro vyetu huko. Pamoja na shukrani zangu, niwapongeze Wabunge wenzangu wote kwa kuvuka katika sehemu zao na majimbo yao mbalimbali ya uchaguzi. *(Makofi)*

Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwamba tumemaliza Uchaguzi Mkuu kwa amani na salama na hata katika hilo sisi ni mfano wa kuigwa Afrika nzima. Naomba nikishukuru Chama cha Mapinduzi kwa kuniteua kuwa mgombea wake wa Jimbo la Mkuranga na katika mantiki hiyo niwashukuru wapigakura wote wa Mkuranga kwa kukipa Chama cha Mapinduzi ushindi wa kishindo katika mafiga yote matatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa namna ya pekee naomba nimpongeze Mheshimiwa sana Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi mno kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Babu yangu mzee Malima angekuwa hai alikuwa na kauli yake moja anasema: "haijapata kutokea." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kura mlizopata wewe mwenyewe katika nafasi yako, Spika, Mheshimiwa Samuel Sitta katika kuchaguliwa kwake na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa katika kuthibitisha uteuzi wa Rais pia zilikuwa ni kura nyingi mno, zilitisha kuliko kimbunga. Mwenye macho haambiwi tazama. Nyote nakutakieni afya njema na mafanikio makubwa katika utekelezaji wa majukumu yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niwapongeze Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa uteuzi wa Rais na ninawahakikishia kwamba imani hiyo ya Rais wameanza kuidhihirisha wao wenyewe ndani ya jumba hili kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao huko Serikalini na humu Bungeni. Nyote pia nawatakia afya njema na mafanikio makubwa katika utekelezaji wa majukumu yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niingie katika hoja. *SEZ* si jambo geni, ni geni kwetu sisi, lakini katika dunia nzima huko kuna *SEZ* zaidi ya 3,000. Ni mkakati unaotumiwa na nchi nyingi kukuza uchumi, kuongeza uwekezaji, kuongeza ajira, kuboresha ushindani wa kiuchumi wa ndani na kadhalika. Lakini nchi nyingi zimepata maendeleo makubwa kwa utekelezaji wa *SEZ* pamoja na sera nyingine zikiambatanishwa na sera nyingine za kiuchumi. Katika fani ya Uchumi wa Maendeleo *(Development economics),* wanafalsafa wakubwa wa *development economics* wanatoka India na wao India wenyewe wana sera ya Taifa ya *SEZ* ambayo inakuwa *applied* kote. Wameanzisha *SEZ* mbalimbali na ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa leo asubuhi kwamba pamoja na India, Indonesia, Malaysia, Singapore na Korea, wamepata mafanikio makubwa ya kiuchumi yanayotokana na kutekelezwa kwa sera hizi za uchumi wa *SEZ.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini siyo *SEZ* zote ambazo zimeleta mafanikio yaliyokadiriwa. Katika nchi nyingine *SEZ* hizo zimechangia kuharibu mfumo wa ajira na badala ya kuongeza ajira, ajira zimehama kutoka sekta nyingine kwa sababu ya ukosefu wa *qualified labour.* Ajira zilipokadiriwa kuongezeka, hazikuongezeka ama kwa sababu wawekezaji hawa wanaingia katika nchi zetu tunawapa *preferential treatment* wanakuwa saa nyingine na hulka ya kuwanyanyasa wafanyakazi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi vivutio pia vinavyotolewa pale ambapo havifanyiwi tafiti za kutosha ili kubaini viwango stahili, muda wa kutoa vivutio hivi na namna ya kodi na nini, vivutio hivyo huishia kuleta hasara kubwa katika mapato ya Serikali kwa kupeperusha vyanzo vya kodi. *SEZ* hizi pia pale ambapo hazisimamiwi vizuri, zinaweza kuathiri uzalishaji wa ndani *(Domestic Industry),* kwa kupendelea mno wawekezaji wageni huku wakibomoa misingi ya uzalishaji ndani ya nchi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nisema yafuatayo, tunafahamu kwamba ni kweli nchi nyingi zimepata mafanikio makubwa kutokana na *SEZ* hizi. Mifano hiyo Mheshimiwa Waziri ameitaja asubuhi. Mimi naamini kwamba wajibu wa Serikali kwanza kabisa ni kufanya utafiti wa kina kabisa wa mazingira maalum ya uchumi wa Tanzania na kulingania na kuanzisha kwa *SEZ* hizi. Naamini pia kwamba

nimeshuhudia maelezo mbali mbali ndani ya Kamati ya Fedha ya Uchumi ya Waziri na wataalam wake na ninaamini kwamba kwa hakika wamefanya hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo tunaepukana na ile *whole sale importation* ya *programme* hizi bila kuweka *input* yetu ya *local knowledge.* Sasa kwa kuwa naamini kwamba Tanzania tunakwenda katika *direction* hiyo ya utekelezaji wa sera hizi kwa kuwa na *input* yetu sisi wenyewe, basi ninaamini kwamba tutatekeleza *SEZ* hizi na tutaepukana na kujikwaa ama kukwama pale ambapo wenzetu walishajikwaa ama kuanguka kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina sera ya umiliki wa mikakati ya uchumi *(Ownership of the Development Agenda).* Watanzania wenyewe lazima tuwe wadau na washiriki wakuu wa *SEZ* hizi kadri muda unavyokwenda. Hivyo Serikali lazima iwe na mikakati ya makusudi ili kujenga mazingira mazuri zaidi ya uwekezaji wa Watanzania wenyewe, wamiliki njia kuu za uchumi ama kwa kutumia mitaji ya ndani ama kwa kuingia ubia na *Foreign Capital.*

Mheshimiwa Naibu Spika, *SEZ* ikipata utekelezaji mzuri ina uwezo wa kuleta mafanikio makubwa sana. *SEZ* moja inaweza ikaleta mafanikio kwa Kanda nzima. Kiuchumi, ukiwa na *SEZ* Mtwara utaleta mafanikio Lindi, utaleta mafanikio Mtwara kwa sababu kuna *surrounding infrustructural requirement* ambayo inaleta manufaa kwa watu wote hawa.

Kwa hiyo, badala ya kila mtu kupendelea *SEZ* iingie nyumbani kwake, ningeshauri kwamba Serikali ifanye kwa wakati huu mikakati ya makusudi ili kujua tunakwenda kwenye awamu gani ya *SEZ* zinazofuatia baada ya hii ya Dar es salaam ama kama ni Mtwara ama kama ni Kigoma lakini Serikali iwe imeishafikia maamuzi hayo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu katika utekelezaji wa *SEZ,* lazima kuwe na mikakati ya makusudi ambayo inaanza muda mrefu kutekelezwa, kwa mfano, ukitaka kupeleka *SEZ* Kigoma, lazima uboreshe *Tanzania Railways Corporation* ili kufikisha mizigo hiyo kwa urahisi zaidi, lakini pia lazima ufungue njia ya Itigi - Tabora - Kigoma. Sasa, huwezi kupeleka *SEZ* mwakani wakati barabara yenyewe hii haijajengwa. Kwa hiyo, naomba kwamba Serikali ianze kuweka mikakati ya makusudi ili utekelezaji wa mipango ya maendeleo iendane na mikakati hii ya kuanzisha *SEZ* katika maeneo hayo muhimu ya maendeleo ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania huwa tunajivunia *potential* kubwa tuliyokuwa nayo. Lakini, *you cannot eat potential,* Tanzania huwezi kukaa ukasema tuna *potential* tu ikakutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Tanzania, kwa sisi wachumi tunajua, sio siri kwamba Tanzania ina uwezo wa kuwa *Economic Power House* ya *East and Central Africa,* tuna uwezo huo. Mungu ametupendelea, tuna vyanzo, tuna rasilimali za kila namna. Lakini maendeleo yana gharama na katika gharama hizo ni kuanza kuwekeza

mapema ili kupata mafanikio baadae ya muda mrefu. Wazungu wanasema, unaanza kujiandaa kuruka kihunzi kabla hujakutana na kihunzi chenyewe *(You begin to prepare to jump the huddle before you bump into the huddle).* Ili tufanye maamuzi makubwa ya kiuchumi kama haya lazima tuwe *bold.* Lazima tuwe tayari kukiri kwamba, lazima itabidi tu tujinyime, lazima itabidi hawa wakose, hawa wapate kwa manufaa ya pamoja ya *micro-economic level* ya Tanzania ya baadae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili naomba nitoe mfano wa bwana mmoja, Mmarekani mweusi mmoja anaitwa *Mr.* Williams, bado yuko hai alikuwa anaishi Los Angeles, kuna Suburb moja kule inaitwa Comton, Comton umaarufu wake ni *gun crime,* ujambazi, *prostitution, drugs.* Ukimtuma mtoto dukani akirudi unasema *Alhamdullillah!*

*Mr.* Williams alikuwa na mambinti zake wawili, anatafuta njia ya kuwatoa katika *culture* ile akasema: *"with all poverty,* nitafanya kila linalowezekana nawaona hawa watoto mabinti wawili kuwa wana-*athletes* wakubwa." Aka-*invest* kufanya kazi mbili, tatu, akawa anawasimia mwenyewe, akasema: "baada ya miaka kumi, Venus na Serena watakuwa *Champions of the World."* Na wameshinda katika mchezo ambao ulikuwa unatawaliwa na watu matajiri na wazungu. Sasa katika *spirit* hiyo, wenzake walikuwa wanamcheka, maanake wanasema watoto weusi hawachezi *Tenis,* wakaja kuwa mabingwa wa dunia. Leo Venus na Serena *jointly* wanatengeneza *$20 million per year.* Baba yao anakaa amepiga mkono tu, amesahahu dhiki yote iliyompata.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimetoa mfano wa bwana Williams ili nifananishe na hili la *SEZ,* hili la *SEZ* ni gumu. Tunataka Serikali itakayotutaka watu wote wa Tanzania tuingie na tushirikiane katika hilo. Utekelezaji wa *SEZ* unataka *leadership* na kwa bahati nzuri Tanzania ina *leadership* ya Serikali nzuri ya Chama cha Mapinduzi. Inataka *commitment* ya wadau wote na inataka busara katika maamuzi katika ngazi zake zote za wataalam, za wanasiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyosema *development is not cheap.* Kwa hiyo, naishauri Serikali kwamba mamlaka ya *SEZ* zilizofanikiwa ni *dynamic* zinafuatilia utekelezaji wa *SEZ* zake. Kwa hiyo na sisi tunaomba mara kwa mara muwe mnaandaa *progress report* na ziwe zinakuja hapa Bungeni ili pia na sisi kama wawakilishi wa wananchi tuwe tunaweza kufanya *assessment* ya maendeleo ya utekelezaji na mafanikio ya *SEZ* hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, nimepata fursa pamoja na wenzangu kupitia Muswada huu kwa kina zaidi huko kwenye Kamati. Licha ya muda mfupi uliokuja lakini tumewauliza wataalam na Waziri maswali magumu na mimi kwa binafsi nimeridhika kwamba Serikali imejianadaa vya kutosha kuanzisha *SEZ* hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninajengwa imani zaidi kuhusu mafanikio ya *SEZ* hizi kwa sababu msimamizi Mkuu wa *SEZ* ni Rais wetu na mamlaka ya *SEZ* ina Mawaziri husika wengi wa kila Idara na Mawaziri hao tumeishawaona umahiri wao kwa sababu ni hao waliko mbele yangu mkono wa kushoto. Pia, nafahamu kwamba wana

wasaidizi wataalam wenye uwezo mkubwa kabisa. Sasa kwa maana hiyo mimi nina imani kwamba *SEZ* zitafanikiwa na Tanzania yenye neema tele inawezekana kila mmoja akifanya wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango wangu katika Muswada huu wa Sheria ya Kuanzishwa kwa Maeneo Maalum ya Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nami nachukua nafasi hii kukubaliana na mpango wenyewe kwamba mpango ni mzuri kwa maana tunategemea utatusaidia kuondoa umaskini na kupunguza tatizo la ajira katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama jinsi ambavyo mpango wenyewe umesema kwamba lengo ni kuharakisha maendeleo ya Tanzania ifikapo mwaka 2020. Lakini basi mimi nadhani kuna baadhi ya maeneo ambayo ni ya muhimu sana yanahitaji tuyaangalie.

Eneo la kwanza kama ambavyo Waziri amesema katika ukurasa wa saba kwa maana ili tuweze kufanikiwa ni pamoja na kuandaa nguvu kazi yenye ujuzi. Kwa kweli hili kwetu sisi kama Tanzania limekuwa ni tatizo kubwa kwa maana kwamba kama hatukuliangalia mapema kwa sasa, basi tutajikuta hao wawekezaji wote wanaokuja wanakuja na watumishi karibu wote wa kutoka nje. Kwa maana hiyo, tunahitaji kuwa na vyuo vya kutosha katika fani mbalimbali ili basi watakapokuja na hawa watumishi wao wachache wakute na sisi tumejiandaa na watumishi wa kutosha katika nafasi mbalimbali za ajira katika huu mpango wa uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile ningependa kutahadharisha kwa maana kwamba wakati mwingine huu mpango wa uwekezaji, sisi kama Serikali tunaangalia zaidi kwa wawekezaji wa nje, kwa maana kwamba hatuwajengei mazingira wale wawekezaji wa ndani ambao nao tunadhani wanaweza wakafanya vizuri tu. Mara nyingi hawa wawekezaji wa nje ipo mifano hai kwa maana kwamba wakati mpango umeletwa tumeupokea na tukauruhusu, lakini mwisho tunakuja kujilaumu sisi wenyewe, mfano, kama sasa tunasikia kuna malalamiko mengi kuhusiana na waliowekeza kwenye madini, yako matatizo ya mikataba na vitu kama hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwangu mimi ninachokifahamu ni hivi, si kweli kwamba wawekezaji wote wanaotoka nje ni wawekezaji wenye fedha. Wao ni kwa sababu mipango hii maadam ilianzia huko kwao, wana yale mawazo ya kwa maana ya kwamba mpango wenyewe wanaufahamu, na kwa kuwa wanaufahamu sasa wanakuja kama wawekezaji lakini hata mitaji unakuta hawana.

Kwa hiyo, hili ndiyo maana nasema na sisi tuna haja ya kuangalia kwamba wawekezaji wetu wa ndani hivi tunaweza kuwasaidiaje? Katika kuwasaidia ni pamoja na kuwapa *exposure,* kwa sabau leo kwa kuwa tunawakaribisha wawekezaji wa nje

tukiangalia hapa kuna vivutio vingi ambavyo sasa leo tunaanza kuwaeleza kwamba hivi ni baadhi ya vivutio ambavyo tutakavyowapa kwa maana ya *incentive.* Lakini hivi wale wa ndani ni lini tumekaa nao tukawambia jamani eeh, hebu mkiwekeza katika kilimo kwa mfano, tutaweza kuwasaidia katika utaratibu huu.

Lakini vingine ni pamoja na kuwapa zile exposure, kwa maana wakati mwingine hata Waziri husika, mfano Waziri wa Biashara anapopata leo anasema naenda nje nchi kama China kuangalia labda viwanda vyao vikoje, basi si vibaya kama wangekuwa wanachukua nafasi ya kuwapeleka kwa maana hata baadhi ya Watanzania na kwa gharama za Watanzania hao wenyewe kwa maana wako tayari kwenda kule na wakaangalia na hatimaye wataweza kuja wakafanya vitu vikubwa na vitu vizuri kwa maana ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani hili nalo ni suala ambalo tunapaswa tuliangalie sana kuona kwamba hivi ni kwa namna gani tunaweza kuwasaidia wawekezaji wa ndani na wao nao wakaweza kujikita katika baadhi ya maeneo hasa kuna baadhi ya maeneo ambayo mimi naona inawezekana tu *especially* unapozungumza katika uwekezaji wa  kilimo, maana maeneo tunayo.

Kwa hiyo, ni kwamba kinachotakiwa ni hawa watu kwa maana watu wetu nao waweze kuona kwamba hivi, katika hayo maeneo au katika hizo nchi zingine ambazo zimeendelea kwenye upande wa kilimo, hivi ni mikakati ipi ambayo wao wameitumia na hatimaye wakaweza nao kuwa wawekezaji maarufu katika upande huo wa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, huo ndiyo ulikuwa mchango wangu, lakini na mimi naungana na wenzangu katika kuunga mkono hoja isipokuwa tu natahadharisha kwamba hebu ni vizuri tusiwaangalie tu hao wa nje, lakini tuwaangalie zaidi wawekezaji wa ndani kwa namna ya kuwasaidia ili na wao waweze kufaidika na mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tena tunapata kipande kidogo cha semina. Kwa mujibu wa taratibu zetu, kifungu cha 21(6), Mbunge yeyote anaweza akapata nafasi ya kutoa maelezo binafsi kuhusu jambo ambalo yeye anataka kujieleza hapa. Sasa tukifanya hivyo inabidi mimi nimwite Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayehusika na mambo ya Bunge atoe hoja ya kuahirisha Bunge. Akitoa hoja ya kuahirisha Bunge, mimi nitamwita yule Mbunge ambaye ana maelezo yake binafsi atasoma yale maelezo yake binafsi na inakuwa lazima awe ametoa kwa Spika, angalau siku moja na atasoma kama yalivyoandikwa. Siyo kuanza kutoa maneno yake. Baada ya hapo akishatoa kama ameelekeza kwa Serikali basi Serikali wanaweza kujibu siku hiyo hiyo, lakini wananaweza pia wakasema hawawezi kujibu kwa leo kwa sababu labda hawakujiandaa. Lakini wote hawa lazima watumie nusu saa tu. Yule anayeota hoja maelezo binafsi na Serikali itakapojibu itatumia nusu saa tu. Halafu kama imezidi hapo basi mimi nitasimama tena nitawahoji kuhusu hoja ile ya mwanzo ya Mheshimiwa Waziri aliyeomba kuahirisha Bunge mpaka kesho. Kwa hiyo, hivi ndiyo itakavyotokea sasa. Kwa hiyo, nitamwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu.

## KUAHIRISHA BUNGE KABLA YA WAKATI WAKE

**WAZIRI WA NCHI , OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kifungu 21, kifungu kidogo cha 6, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liahirishwe sasa hadi kesho saa tatu asubuhi. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

## MAELEZO BINAFSI KUHUSU MAZUNGUMZO YA *IGP* KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU CHAMA CHA *CUF*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa idhini yako uniruhusu nitoe maelezo binafsi kwa mujibu wa Kanuni, kifungu cha 21 (9) ya Kanuni za Bunge toleo la mwaka 2004. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa maelezo binafsi kwa mujibu wa Kanuni ya 21(9) ya Kanuni za Bunge toleo la mwaka 2004.

Mnamo tarehe 30 Desemba, 2005 Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu alihutubia Bunge lako Tukufu. Hotuba ambayo mnamo tarehe 07 Februari, 2006 Mheshimiwa Edward Lowassa, Mbunge na Waziri Mkuu alitoa hoja kuliomba Bunge hili katika Mkutano wake unaoendelea hivi sasa tuijadili hotuba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi na Kiongozi wa Upinzani Bungeni, ulinipa heshima ya kuwa Mbunge wa kwanza kuchangia hoja hiyo ambayo niliipongeza na kuiunga mkono pamoja na kutoa mchango katika maeneo mbalimbali likiwemo eneo linalohusu kukithiri kwa ujambazi nchini, eneo ambalo Rais na Waziri Mkuu wamelipa uzito unaostahili kwa mujibu wa matakwa ya Katiba ya kwamba jukumu la ulinzi na usalama wa raia na mali zao ni la Serikali na Jeshi la Polisi ndilo lililokabidhiwa jukumu hilo kwa mujibu wa sheria mbalimbali zilizotungwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maelezo niliyotoa mimi wakati wa kuchangia hotuba hiyo ya Rais na hususan suala la ujambazi nilisema kuwa hatua zinazochukuliwa na Jeshi la Polisi siyo makini na kulitaka Jeshi la Polisi liwalinde watoa habari na kutaka viongozi wa Jeshi hili wasikae muda mrefu ili waweze kushirikiana na majambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu mbali na kuungwa mkono na Wabunge wote waliochangia hotuba hii, Rais katika mkutano wake alioufanya uwanja wa Jamhuri

hapa Dodoma, aliwataka wananchi watoe taarifa juu ya majambazi na kumuarifu yeye mwenyewe, Waziri Mkuu au ofisi ya Usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkuu wa Jeshi la Polisi Omar Mahita, mnano tarehe 09Februari, 2006 magazeti ya Mtanzania toleo la 3568 na *The Guardian* la tarehe 10 Februari, 2006, Alasiri la tarehe 10 Februari, 2006 na magazeti mengine na *television* na redio aliviita vyombo mbalimbali vya habari na vilimnukuu akisema kuwa: "Mkuu wa Jeshi la Polisi, Omar Mahita anakihusisha chama changu cha *CUF* na wizi wa kutumia nguvu na silaha nzito kama vile *sub-machinegun AK 47."* Lakini ushahidi alioonyesha mbele ya Maafisa wake wa Jeshi na vyombo vya habari ni visu vilivyopakwa rangi ya bendera ya *CUF,* visu ambavyo alivionyesha tarehe 13 Desemba, 2005 siku moja kabla ya Uchaguzi Mkuu ambavyo zaidi hutumika jikoni na kwenye soko la samaki. Visu hivyo havitumiki kabisa katika ujambazi aliouzungumzia Rais, Waziri Mkuu na Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo hicho kimedhalilisha sana Jeshi la Polisi na Taifa kwa jumla na hasa Rais wetu ambaye kwa kujali maisha ya Watanzania suala la ujambazi amelipa kipaumbele kama alivyoipa kipaumbele njaa inayowakabili Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba ya nchi na sheria nyingine za nchi yetu mtuhumiwa mara akamatwapo hutakiwa afikishwe mahakamani na siyo kwenye vyombo vya habari. Polisi haina mamlaka ya kutoa hukumu. Hili ni kosa kubwa, ni uvunjaji wa Katiba ya nchi na haki za binadamu na lisingepaswa kufanywa na mtu mwenye wadhifa kama *IGP* ambaye ana wajibu mkubwa sana katika kulinda Katiba ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkuu huyu wa Jeshi la Polisi aliuthibitishia umma wa Watanzania na ulimwengu kwa jumla kwamba yeye Omar Mahita kama Mkuu wa Jeshi la Polisi wakati wote wa kipindi alichokuwa madarakani, karibu miaka kumi alihakikisha kuwa Chama changu cha *CUF* hakipati ushindi na kuweza kuongoza nchi. Huku nako ni kuvunja Katiba ya nchi na kuwanyima raia haki yao ya kuchagua na kuchaguliwa na kwenda kinyume na sheria namba 5 iliyoanzishwa ya vyama vya siasa, pamoja na muafaka wa CCM na *CUF* ambao kiini chake ni kuvurugika kwa Uchaguzi wa mwaka 1995 na mwaka 2000 ambapo mwaka 2001 zilisababisha mauaji ya Watanzania wanaozidi 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari Polisi mmoja alikatwa kichwa yeye akiwa Mkuu wa Jeshi la Polisi. Uthibitisho wa hayo ni kuundwa kwa Tume ya Uchunguzi iliyoongozwa na Brigedia Generali Mstaafu, Balozi Hashim Mbita, tarehe 17 Januari, 2002. Maelezo zaidi kiambatanisho *Tanzanite organization,* chanzo ni gazeti la Majira la tarehe 17 Januari, 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kujiamini *IGP* alisema *CUF* haitatawala mpaka kiama chini ya uongozi wake yeye *IGP* Omar Mahita. Kauli hizi zote ni nzito ambazo

kwa akili ya kawaida hakuna anayeamini kwamba *IGP* Omar Mahita, hakupata maelekezo ambayo kwa wadhifa wake ni Amiri Jeshi Mkuu tu ndiye anayeweza kumuamuru.

Mheshimiwa Spika, lakini Amiri Jeshi Mkuu amekuwa wazi kwetu na kwa umma wa Watanzania kwamba yeye Rais atahakikisha kuwa demokrasia inashamiri nchini na Vyama vya Siasa vitapata fursa ya kufanya shughuli zake bila kubaguliwa ili mradi vinafuata sheria za nchi. Aidha, alibainisha wazi kuwa ujambazi utatokomezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mbali na kukidhalilisha Chama changu na wanachama wake, pia kauli hizi zimejenga fitina baina ya Wabunge na Polisi ambao Waheshimiwa Wabunge wamekuwa mstari wa mbele katika kulitetea Jeshi la Polisi katika maslahi yao, vifaa na marupurupu mengine. Lakini kama hiyo haitoshi, *IGP* amemdhalilisha Amiri Jeshi Mkuu pale Mheshimiwa Rais alipolipa uzito tatizo la ujambazi na kuwapa matumaini Watanzania, lakini yeye akaligeuza kuwa la kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumaliza kwa kunukuu maneno ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere mwezi Aprili, 1982 katika uwanja wa ndege wa Dar es Salaam.

Mwalimu baada ya kupata habari kwamba viongozi wa Jeshi la Polisi waliokuwa katika mkutano wao mkuu katika Chuo cha Polisi Moshi wameigomea hotuba ya Naibu Waziri kwa kuwaambia kuwa wananchi wanalalamika kwamba baadhi ya Maafisa wanapokea hongo ya shilingi 500 ili raia wanaotaka kuvuka mpaka wa Tanzania kwenda Kenya (wakati huo mpaka ulikuwa umefungwa), waweze kuvuka. Mwalimu alituita mimi na Mkuu wa Jeshi wakati huo na kusema: “Hamad, kule Uingereza Serikali inaliheshimu sana Jeshi la Polisi, lakini na Jeshi lenyewe linajiheshimu maana polisi ni kioo cha nchi na kioo kikiingia vumbi hupanguswa, kikivunjika huondolewa.” *(Makofi)*

Kwa kuwa *IGP* huyu ni mteuliwa wa Mheshimiwa Rais;

Na kwa kuwa kiongozi huyu wa ngazi ya juu kabisa kwenye Jeshi la Polisi amekuwa akitoa kauli mbalimbali kukituhumu Chama cha *CUF* kwamba kinahusika na ujambazi unaofanyika sehemu mbalimbali hapa nchini, naomba nipate maelezo kutoka Serikalini kuhusiana na kauli hizo za mteuliwa huyu wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Ni mimi Hamad Rashid Mohammed, Mbunge wa Jimbo la Wawi na Kiongozi wa Upinzani Bungeni. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imesikia hoja ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Kiongozi wa Upinzani Bungeni. Suala hili liko ndani ya uwezo wa Serikali. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali italifanyia kazi suala hilo. Napenda tu kurudia kauli yangu kwamba mtu yeyote ambaye ana taarifa kuhusu uhalifu na hasa ujambazi

asisite kutoa taarifa kwa vyombo vya usalama na mimi nitaendelea kuzifanyia kazi taarifa hizo zitakapokuwa zimenifikia.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mmesikia maelezo binafsi siyo hoja. Ingekuwa hoja angetakiwa kwanza aungwe mkono. Kwa hiyo, amejieleza na Serikali imejibu. Sasa nawahoji kutokana na hoja aliyouliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu Kuahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. Hiyo ndiyo hoja ninayohoji. Siwahoji ile aliyosema Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, wala siwahoji hii ya Waziri.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.33 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi Tarehe 16 Februari, 2006 saa tatu asubuhi)*